**27 JANUARI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA PILI

### Kikao cha Kwanza – Tarehe 27 Januari, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

### D U A

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

### TAMKO LA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE WOTE

**SPIKA:** Mimi Mussa Azzan Zungu…, wote tunasoma kwa pamoja.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wote walitamka Ahadi ya Uzalendo)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE

Katibu.

**27 JANUARI, 2026**

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

1. Mhe. Asha Hussein Saleh
2. Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel
3. Mhe. Zulfa Mmaka Omar

*(Wabunge waliotajwa hapo juu waliapa Kiapo cha Uaminifu na Kutamka Ahadi ya Uzalendo)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Taarifa ya Spika chini ya Kanuni ya 41(2) ya Kanuni za Bunge 2025. Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo mtakumbuka mara baada ya kuahirisha Mkutano wa Kwanza wa Bunge yametokea matukio ya kuhuzunisha kwa Bunge na Taifa kwa jumla.

Waheshimiwa Wabunge, mnamo tarehe 11 Desemba, 2025 tulipata msiba mkubwa wa Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama. Marehemu Jenista Mhagama alifia Jijini Dodoma katika Hospitali ya Benjamini Mkapa, alipokuwa akipatiwa matibabu. Aliagwa rasmi tarehe 13 Desemba, 2025 katika Kanisa Katoliki Kiwanja cha Ndege, Jijini Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli hiyo iliongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na mazishi yake yalifanyika tarehe 16 Desemba, 2025 katika makaburi ya Kijiji cha Luanda Wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma. Makamu wa Rais, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi aliongoza mazishi hayo na mimi Spika wenu pia nilihudhuria pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Wabunge kadhaa.

Waheshimiwa Wabunge, aidha, mnamo tarehe 18 Januari, 2026 tulipata msiba wa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), Mheshimiwa Halima Idd Nassor. Marehemu Halima Idd Nassor alifia katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete Jijini Dar es Salaam alipokuwa akipatiwa matibabu na kuzikwa siku hiyohiyo ya tarehe 18 Januari, 2026 katika makaburi ya Kibada kwa Dole Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Baraka Leonard aliongoza mazishi hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo desturi yetu na kwa heshima kwa waliokuwa Wabunge wenzetu (Marehemu Jenista Joakim Mhagama na Marehemu Halima Idd Nassor) ninaomba tusimame kwa dakika moja ili kuwakumbuka na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awapokee na kuwapumzisha kwa amani. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. Amina.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa muda mfupi kama ishara ya kuwambuka Wabunge tajwa waliofariki dunia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa ahsanteni.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE URATIBU NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, leo ni siku ya kuzaliwa ya Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kuwa nimeanza kusimama hapa bila shaka kwa niaba yenu tunamtakia kila la kheri kwa siku yake hii ya kuzaliwa, Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 14 Novemba, 2025.

**SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mwenye swali tuko Wabunge wengi wapya na siyo rahisi kuwajua wote kwa majina. Kanuni zetu za Bunge zinaeleza wazi ili uweze kuzungumza, *you have to catch the Speaker's eye* kwa hiyo mpaka nikuone ndiyo na wewe nikwambie useme. Pia Kanuni hiyo nayo inasema unaweza ukamwandikia ki-*note* Spika kwa jina lako kuwa unaomba kuuliza swali namba fulani na nikakupa nafasi. Kwa wale Waheshimiwa Wabunge wetu wageni basi tumieni fursa ya kuandika jina lako ili nikutambue na nikishaliona mara moja nitalikumbuka.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbunda.

Na. 1

### Mradi wa *TACTIC* Jimbo la Mbinga Mjini

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa *TACTIC* katika Jimbo la Mbinga Mjini?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwape tahadhari kila swali ni dakika nne na nusu. Kwenye nyongeza ya maswali itakuwa ni ndogo sana kwa sababu swali moja kujibiwa ni dakika nne na nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa ufadhili wa Benki ya Dunia imeanza utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC* katika Jimbo la Mbinga Mjini, ambapo sasa Mradi huu upo hatua ya usanifu chini ya Mhandisi Mshauri aitwaye *Bosphorus Technical Consulting Corporation* ikishirikiana na *Building Design Authority Limited* pamoja na *Masterpiece Consult Limited*. Mara baada ya kukamilika usanifu huo ujenzi utaanza mara moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini pia niishukuru Serikali kwa kuanza mchakato wa kutekeleza Mradi wa *TACTIC* ambao ndani yake kuna ujenzi wa barabara kilometa 12, lakini pia ujenzi wa soko la kisasa na ujenzi wa stendi. Ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; baada ya mchakato huo kuanza ni lini sasa kazi ya usanifu itakuwa imekamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; baada ya usanifu kukamilika ni lini Serikali itaanza kutekeleza hatua nyingine za kuhakikisha kwamba, mradi huo unaanza kutekelezwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini.

Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu kwenye Mradi huu wa *TACTIC,* Awamu ya Tatu, inafanyika kwenye miji 18. Mara tutakapokamilisha kwenye miji yote usanifu huu, kati ya mwezi huu unaoisha na mwezi wa pili, tutaendelea na hatua zinazofuata za kutangaza zabuni ikiwa ni kwa ajili ya kuendelea kumpata mkandarasi mjenzi kwenye maeneo mbalimbali, pamoja na mkandarasi mtaalam mshauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, ajiandae Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Jimbo la Kilombero pia, lina Miradi ya *TACTIC* ya soko, stendi na barabara za mitaa. Je, ni lini mradi huu utaanza katika Jimbo la Kilombero? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kilombero ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wetu wa *TACTIC,* Awamu ya Tatu na hivi sasa tuko kwenye kukamilisha usanifu kwenye hii miji yote 19 ya Awamu ya Tatu. Mara tutakapokamilisha usanifu na gharama kubainika mradi utaanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji wa Bunda, Jimbo la Bunda Mjini ni miongoni mwa miji 18 ambayo na yenyewe inatakiwa itekelezwe Mradi wa *TACTIC* kwa kujengwa kilometa 25 za lami, stendi ya kisasa, machinjio na soko la kisasa. Ni lini sasa mradi huo utaanza katika Jimbo la Bunda Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, Mji wa Bunda ni miongoni mwa Awamu ya Tatu ya utekelezaji wa Mradi huu wa *TACTIC*. Mara tu baada ya Serikali kukamilisha usanifu tutakwenda kuanza hatua za ujenzi mara moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

Na. 2

**Ujenzi wa Barabara ya Mshangano-Legele-Mlete**

**MHE. JACQUELINE K. NGONYANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mshangano - Legele hadi Mletele yenye kilometa 9.2?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Profesa Shemdoe, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa Barabara ya Mshangano - Legele hadi Mletele, kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami ambapo, shilingi bilioni 2.51 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa awali wa kilometa 5.0 za barabara hiyo. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuweza kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, wakati tunasubiri upatikanaji wa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026, barabara hiyo

imetengewa shilingi milioni 20, kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo ya kawaida. Vilevile, kwenye mwaka wa fedha ujao wa 2026/2027, Serikali imepanga kutenga shilingi milioni 250, kwa ajili matengenezo ya barabara hiyo ili kuhakikisha inapitika muda wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swali, ninaomba jina langu lisomeke Jacqueline Ngonyani Msongozi kwa maslahi ya Wanaruvuma.

Mheshimiwa Spika, swali la (a); kwa kuwa, Barabara hii ya Mletele – Mshangano ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi katika Manispaa ya Songea. Je, Serikali inapochelewesha ujenzi wa barabara hii haioni kwamba, inadumaza uchumi wa Manispaa ya Songea?

Mheshimiwa Spika, swali la (b); Barabara hii ni *bypass* ambayo inatumika kwa Barabara ya *Mtwara Corridor* kwa hiyo, kutoka Mletele kwenda Mshangano kwenda Njombe ni barabara muhimu sana, kwa ajili ya kuondoa msongamano wa magari katika barabara kuu hiyo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, barabara hii inajengwa kwa haraka ili kuondoa changamoto iliyopo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, Serikali haicheleweshi ujenzi wa Barabara hii ya Mshangano - Legele – Mletele, ndiyo maana imekamilisha; imetenga na imeweka fedha ikakamilisha usanifu wa barabara hii. Kinachofuata sasa, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi,

ni kwenda kuijenga barabara hii, kwa awali, kilometa tano kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hii pia, tunatambua kwamba, huwa inatumika kama *bypass* kwenye barabara kuu ya Songea - Tunduru. Sisi Serikali mwaka ujao wa fedha wa 2026/2027, tutakapotenga milioni 250 barabara hii itakuwa inapitika wakati wote na itaendelea kutimiza jukumu hili la kuwasaidia wananchi kama *bypass* wakati panapokuwa pamehitajika.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Johnston.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninapenda kuuliza swali la nyongeza kuhusu barabara zangu za Jimbo la Bukoba Mjini. Barabara ya kutoka Chemba kwenda Rugambwa, yenye urefu wa kilometa 1.4 na Barabara ya kutoka Kashai kwenda Mngeza, yenye urefu wa kilometa 7.41 zitaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami, kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, barabara hizi za Bukoba Mjini zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, kama ambavyo imeainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi, mara tu baada ya Serikali kupata fedha na kutenga, kwa ajili ya shughuli hiyo.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Timoth Anyosisye, Kawe.

Na. 3

**Ujenzi wa Kingo za Mto Mbezi**

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kingo za zege za Mto Mbezi ili kuzuia kusombwa kwa nyumba na kusababisha maafa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Profesa Shemdoe. Ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Timoth Geofrey Anyosisye, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mto Mbezi ni mto muhimu Jijini Dar es Salaam. Wakati wa msimu wa mvua mto huu huongezeka kina na mara nyingi husababisha mafuriko yanayoathiri miundombinu na makazi ya watu yaliyo kando ya kingo zake.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inakamilisha utaratibu wa kumpata mtaalam mshauri atakayefanya kazi ya usanifu wa kina kwa lengo la kujua gharama halisi za ujenzi wa mto huo. Baada ya gharama halisi kufahamika itatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa kingo za mto huo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali inatambua uwepo wa Mto Nyakasengwe pamoja na Mto *IPTL*. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI namwelekeza Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Dar es Salaam, pamoja na Mratibu wa Mradi wa *DMDP II,* wapitie mito hiyo miwili iliyoongezeka kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge waweze kuona uhalisia na sisi, kama Serikali, tuone namna ya Kwenda nalo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni katika Mto Kikafu, lile daraja, kumekuwa kukitokea ajali nyingi na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa Barabara ya Moshi – Arusha, lakini barabara pekee ambayo ni ya mchepuko na ya mbadala ni Bomang'ombe - Chekimaji *TPC,* ambayo inajengwa kilometa 3.5. Je, ni lini sasa Serikali italeta fedha ya kumaliza barabara hii ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami na taa juu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Barabara ya Bomang'ombe - Chekimaji *TPC*. Kama ambavyo imeanishwa kwenye mipango yetu, Serikali itatenga fedha, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii, kilometa 3.5, kwa kiwango cha lami mara tu baada ya fedha hizi kupatikana.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Hija Hassan Hija, Mbunge wa Kiwani.

Na. 4

**Uhitaji wa Vifaa Tiba Nchini**

**MHE. HIJA HASSAN HIJA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka vifaa tiba vya kutosha, hususan vifaa vya kujifungulia, katika hospitali zote nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. RAJAB S. JAFAR)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri

ninayeshughulikia masuala ya afya, TAMISEMI. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hija Hassan Hija, Mbunge wa Kiwani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi vinavyoendelea kujengwa kote nchini. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano, 2021/2022 hadi 2024/2025, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 285.6, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vikiwemo vifaa vya kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 shilingi bilioni 32 imetolewa, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, ngazi ya msingi. Shilingi bilioni 9.6 imetolewa, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali za halmashauri kote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hija.

**MHE. HIJA HASSAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mwezi Novemba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara kwenye hospitali moja hapa Mjini Dodoma na wananchi, hususan wazazi, waliipongeza Serikali kwa huduma nzuri za matibabu na dawa, lakini walilalamikia ukosefu wa mabeseni na ndoo, kwa ajili ya wajawazito; Mheshimiwa Waziri Mkuu akaagiza jambo hili litatuliwe. Ninaomba kujua limefikia hatua gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. RAJAB S. JAFAR):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hija Hassan Hija. Tunakumbuka ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye kituo chetu, kile cha afya na akatoa maelekezo yale.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo maelekezo ya Serikali. Nami kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninawaelekeza Waganga Wakuu wote wa Mikoa, Waganga wote, ma-*DMO* wa Halmashauri na ma-*MOI* wetu waendelee kutekeleza majukumu hayo, waendelee kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maana kwamba, sasa mambo ya kuwatoza hivyo vifaa kama mabeseni na ndoo visiwe vikwazo kwa mama zetu wanapokwenda kujifungua katika hospitali zetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiza Mayeye.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri na amesema, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo, lakini maelekezo haya mpaka tunavyozungumza huko kwenye vijiji wajawazito bado wanapeleka mabeseni wembe na mipira. Ninataka majibu ya Mheshimiwa Waziri kuanzia sasa, ni lini hii hali itakoma kwa wajawazito kwa sababu, Kigoma Kaskazini na maeneo mengine bado akinamama wanapeleka mabeseni na vifaa vingine? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. RAJAB S. JAFAR):** Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni maelekezo ya Serikali. Ninarudia kwa kwamba, halmashauri zote nchini tunatoa wito kwa Wakurugenzi, Waganga Wakuu na ma-*DMO* watekeleze maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maana maagizo hayo ndiyo maagizo ya Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba.

Na. 5

**Kutenga Maeneo ya Malisho - Igalula**

**MHE. JUMA M. KAWAMBA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga maeneo ya malisho katika Jimbo la Igalula ili kupunguza migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. RAJAB S. JAFAR)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mbunge wa Jimbo la Igalula, Halmashauri ya Uyui, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Igalula limekuwa na migogoro midogo ya wakulima na wafugaji, hususan katika maeneo ya kulishia mifugo. Aidha, migogoro hii imekuwa ikitatuliwa kupitia maridhiano ya mtu na mtu na hata kuwahusisha viongozi wa Serikali, kwa ajili ya kusimamia taratibu za fidia kwa hasara inayojitokeza. Aidha, Serikali imetenga jumla ya hekta 6,226.92 katika vijiji 16 vilivyopo Igalula.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Matumizi Bora ya Ardhi, ikiwa ni pamoja na kuainisha na kutenga maeneo maalum ya wakulima na wafugaji, kwa ajili ya ustawi wa wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui. Pia, Serikali inatoa wito kwa viongozi ngazi ya mkoa na halmashauri kote nchini kuhakikisha wanatatua migogoro ya wakulima na wafugaji kwa wakati na kuweka utaratibu mzuri wa matumizi bora ya ardhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Wizara. Kwanza kabisa ninapenda kuwapongeza kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya, lakini ninampongeza Mheshimiwa Rais, wananchi wa Jimbo la Igalula wanamshukuru kwenye chanjo ya ruzuku, kuondoa na utambuzi wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza; je, Serikali ina utaratibu gani wa kisheria na kiutendaji, ili kuhakikisha sasa maeneo haya yaliyotengwa hayavamiwi na hayabadilishiwi matumizi ili kuweza kuepuka migogoro kati ya wakulima na wafugaji ndani ya Jimbo la Igalula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. RAJAB S. JAFAR):** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, Mbunge wa Igalula, Halmashauri ya Uyui, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na Sheria mbalimbali ambazo zimekuwa zikitu-*guide* na zimepitishwa na Bunge lako Tukufu. Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, hii ilikuwa inatoa hati ya Hatimiliki ya Kimila, lakini kuna Sheria ya Ardhi Namba Sita ya Mwaka 2007, ambayo imeainisha mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji, lakini kuna maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo, yote yameainishwa katika Sheria hii. Sambamba na sheria hizi pia, kuna Sheria Namba 287, ambayo imewezesha halmashauri kutunga Sheria Ndogo. Kwa hiyo, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaziagiza Halmashauri zote nchini zifuatishe Sheria hizi na kuona zinatatua migogoro ya ardhi katika maeneo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amosy Maganga.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Wilaya ya Sikonge kwa hivi sasa wanakabiliwa sana na ufinyu wa maeneo, kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Wilaya ya Sikonge ina jumla ya mapori tisa na kati ya haya, yaliyo mengi ni mapori ya akiba. Je, Serikali, ni wakati gani sasa haya mapori ya akiba yataanza kutumika, kwa ajili ya hao wananchi, ukizingatia kwamba, kwa kweli wananchi wanahitaji kuendesha shughuli zao za kiuchumi na hasa kilimo, ufugaji, pamoja na urinaji wa asali na kwa hivi sasa, hata viashiria vya uvunjifu wa amani vinaanza kuonekana?

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako limeshaeleweka. Ahsante.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. RAJAB S. JAFAR):** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mbunge wa Sikonge, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Utakumbuka Bunge lako hili kipindi cha Mwaka 2021 mpaka 2025 iliundwa Kamati ya Mawaziri Nane, ambayo ilizunguka nchini kote kuainisha maeneo haya na kufanya tathmini. Hivyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tathmini ikikamilika kwa wakati watatengewa maeneo ili wapate kufanya shughuli za uzalishaji mali, kilimo na ufugaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Marwa.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuwatengea maeneo wananchi wa Wilaya ya Bunda, Nyatwali, kwa ajili ya ufugaji ambapo maeneo hayo yalitwaliwa na Serikali kurudishwa hifadhini. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuwatengea wananchi, hasa wananchi wa Mkoa wa Mara kwa ujumla, maeneo ya kulishia wanyama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. RAJAB S. JAFAR):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu hapo awali, swali hilo linaenda sambamba na swali la Mbunge kutoka Sikonge kwa maana ya kwamba ile Kamati ya Mawaziri Nane bado wanafanya kazi na tathmini ili tuweze kuwatengea maeneo wananchi wetu waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji.

**SPIKA:** Ahsante. Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali.

Na. 6

**Kipaumbele cha Wizara kwa Vijana**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, kipi kipaumbele cha Wizara ya Vijana kwa vijana wa Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Pia kwa namna ya kipekee kwa kuunda Wizara mpya inayoshughulikia maendeleo ya vijana ikiwa ni dhamira yake ya kuwaweka vijana katikati ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kikuu cha Wizara ya Maendeleo ya Vijana kwa vijana wa Tanzania ni kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa lengo la kuboresha ustawi wao na kuchangia kwa tija katika maendeleo endelevu ya Taifa. Katika kutekeleza kipaumbele hicho, Wizara inajielekeza katika maeneo makuu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara inaendelea kuimarisha uwezeshaji wa vijana kiuchumi kwa kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa mitaji, mafunzo ya ujasiriamali, ukuzaji wa biashara na ajira. Pili, Wizara inaweka mkazo katika uendelezaji wa ujuzi kwa vijana ili kuwaandaa kukabiliana na mahitaji ya soko la ajira na kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara inaendelea kuimarisha ushiriki wa vijana katika maamuzi na masuala ya utawala bora, kwa kuanzisha na kusimamia majukwaa rasmi ya ushiriki wa vijana. Mwisho, Wizara inatekeleza afua za ustawi, malezi na ulinzi wa vijana, ikijumuisha masuala ya afya ya akili, maadili, uzalendo, amani na mshikamano wa kitaifa, kwa kushirikiana na Wizara, taasisi pamoja na wadau mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Latifa.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanalenga kuwatia moyo vijana, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mheshimiwa Waziri ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kupitia Mfuko huu wa Maendeleo wa Vijana Taifa katika mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ili kuwasaidia na kuweka ahueni kwa vijana, Wizara haioni haja sasa ya kuya-*hold* hayo mashirika na maeneo mbalimbali ambayo wanataka kuwasaidia vijana ili waanzishe *SACCOS* maalum kwa vijana wa nchi hii na kupunguza zile afueni kwa ajili ya vijana ikiwemo riba? Ahsante.

**SPIKA:** Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Latifa, Mbunge wa Viti Maalum kwamba Serikali kwa miaka yote kupitia Idara ya Vijana iliyokuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya uwezeshaji wa vijana, lakini utakumbuka kwamba Mheshimiwa Rais alielezea dhamira yake ya kuona namna anavyoongeza mitaji kwa ajili ya vijana katika kuwawezesha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira hiyo ipo na Serikali muda mfupi ujao itatoa mpangilio wa namna ambavyo vijana wa Tanzania watanufaika na mitaji ambayo itatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pili Wizara yetu itaendelea kuratibu, kushirikiana na mashirika na wadau mbalimbali ambao wanajishughulisha na shughuli za vijana, nia na dhamira ikiwa ni kukusanya nguvu za pamoja kuwawezesha vijana katika nchi yetu sawasawa na Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 ambayo uliboreshwa mwaka 2024. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Je, ni kwa namna gani Serikali imejipanga kuhakikisha vijana wa mijini na vijijini wanashiriki kikamilifu katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Mahawanga. Serikali kupitia Sera ya Maendeleo ya Vijana imeweka mkakati maalum wa utekelezaji wa ushiriki wa vijana wa mijini na vijijini pia rika zote na wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza afua hizo na kuhakikisha kila kijana wa Tanzania anakuwa sehemu ya mambo muhimu yanayofanywa katika Taifa letu. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume.

Na. 7

**Athari za Uchimbaji Madini Mto Mvuha na Mfizigo – Morogoro Kusini**

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME** aliuliza:-

Je, hatua gani zimechukuliwa za uchafuzi wa Mto Mfizigo na Mhuva zitokanazo na shughuli za madini na kubaini kemikali zilizopo na athari zake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, pili kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuru ya Muungano wa Tanzania, kwa dhamana kubwa aliyonipa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Ninaomba nimuahidi Mheshimiwa Rais kwamba nitafanya kazi kwa juhudi, maarifa na weledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mito ya Mfizigo na Mhuva iliyopo katika Jimbo la Morogoro Kusini ni moja ya maeneo ambako hufanyika shughuli za uchimbaji mdogo wa madini katika maeneo ya pembezoni mwa mito hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha mito hiyo inatunzwa na kuzuia uchafuzi wake kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini, Serikali mwaka 2025 ilichukua sampuli za maji ya mito hiyo kwa ajili ya kupima ikiwa kuna uchafuzi wa kemikali zitokanazo na uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Matokeo ya vipimo vya sampuli hizo vilionesha kuwa kuna kemikali za chuma na manganizi. Kemikali zilizobainika kuwepo zinatokana na miamba iliyokuwa inachimbwa na siyo kwamba zinatokana na matumizi ya kemikali za kuchenjua madini kama zebaki.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua kulinda vyanzo vya maji na mito ikiwemo Mito ya Mfizigo na

Mhuva katika mazingira ya Morogoro Kusini kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Sheria ya Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, shughuli hizi za madini ni shughuli zinazowaendeshea maisha wananchi wenzetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa sasa elimu ya utunzaji wa mazingira ili wananchi wenzetu waendelee na shughuli zao za kujipatia kipato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba shughuli za madini ni shughuli muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na wananchi na sisi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Madini na Wizara zote zenye nasaba na masuala ya mazingira na madini tutaendelea, kwanza kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa wananchi na wachimbaji wote wa madini kuzingatia sheria na taratibu za uhifadhi wa mazingira ili kuwa na uchimbaji wa madini na uhifadhi wa mazingira endelevu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Alan Mvano.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kakonko Mkoa wa Kigoma tunao uchimbaji wa madini ya dhahabu Kata ya Nyamtukuza, Vijiji vya Nyamtukuza maeneo ya Nyamwilonge. Tarehe 10 Disemba tulikwenda na Mkuu wa Mkoa pale na akazuia shughuli za uchimbaji kwa sababu zilikuwa zinakiuka sheria za mazingira na zinaathiri wananchi wa Vijiji zaidi ya saba vya Kihomoka, Kumwiyando na Vijiji vingine vya Bwera mpaka Nyamwilonge. Je, ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali ili

kunusuru maisha ya wananchi hao kwa sababu mto ule haufai kabisa kwa matumizi ya binadamu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la uchimbaji wa madini linaendeshwa kwa mujibu wa sheria na suala la uhifadhi wa mazingira linasimamiwa kwa mujibu wa Sheria, Sura ya 191.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kakonko kwamba kipaumbele cha kwanza ni kutunza mazingira, lakini Serikali itaendelea kuhakikisha inaweka mazingira wezeshi kwa wachimbaji wa madini ili kunufaika na rasilimali za madini vilevile kutunza mazingira katika maeneo hayo. Tutawasiliana na Ofisi ya Wizara ya Madini ili tuweze kuliweka sawa na wananchi waweze kuendelea kuchimba madini.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Injinia Kija Limbu.

Na. 8

**Mikataba ya wenye Leseni na Wachimbaji Wadogo wa Madini**

**MHE. ENG. KIJA L. NTEMI** aliuliza:-

Je, ni nani anayesimamia mikataba ya wenye leseni na wachimbaji wadogo wa madini wanaovumbua madini na mikataba hiyo ni ya muda gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuwa msaidizi wake kama Naibu Waziri wa Madini, pia wananchi wa Jimbo la Longido kwa mara ya tatu sasa wameendelea kuniamini kuwa mwakilishi wao katika Bunge lako Tukufu, ninaahidi kwamba sitawaangusha wote, siyo Rais wangu wala walionipa ridhaa ya kuwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Kija Limbu Ntemi, Mbunge wa Katoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia marekebisho ya Kanuni za Haki Madini za Mwaka 2018 na marekebisho ya mwaka 2025, Kanuni ya 5(a)(1) imeweka sharti la mwenye leseni ndogo ya uchimbaji ijulikanayo kama *PML,* kuingia mkataba na mchimbaji mdogo atakayefanya shughuli za uchimbaji ndani ya eneo la leseni yake na kuhakikisha mkataba huo unaidhinishwa na kusajiliwa Tume ya Madini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ya Madini imeandaa rasimu ya mkataba kati ya wamiliki wa leseni na wachimbaji wadogo na kuuwasilisha kwa Maafisa Madini Wakazi wote na watausimamia pindi unaposainiwa na kusajiliwa. Mikataba hiyo itadumu kipindi cha miaka mitatu na huruhusiwa kuhuishwa kwa kipindi kingine kulingana na makubaliano ya wahusika. Ahsante sana.

**SPIKA:** *Engineer* Kija.

**MHE. ENG. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru kwa majibu ya Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ninapenda kufahamu huu mkataba utaanza lini, kwa sababu watu wameshaumizwa na wameshafungiwa mikataba ambayo inaonesha ni mkataba wa miezi minne, hauna malipo, lakini watu wamelipa fedha nyingi kwa ajili ya hii mikataba. Unafungiwa mkataba wa miezi minne kila duara moja inalipa shilingi milioni kumi kumi, zaidi ya maduara 100 watu wamelipa fedha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, hawa watu waliolipishwa hizi fedha ndani ya miezi minne na miezi mitatu kuna uwezekano wa kurudishiwa fedha zao ili huu utaratibu utakapoenda kuanza, hawa watu wawe wamesharudishiwa fedha zao na utaratibu ufuatwe vizuri kwa sababu wameonewa na zile fedha wamelipa pasipo na utaratibu na hazina mfumo wowote.

**SPIKA:** Mheshimiwa maswali yako ni mawili tu.

**MHE. ENG. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza *Engineer* Kija, ninapenda kukujulisha kwamba kanuni hizi zilipotungwa au zilipofanyiwa marekebisho mwaka jana tukaweka kipengele kinachohakikisha kwamba hakuna mwenye leseni anayempangisha mchimbaji mdogo eneo bila kusainiana mkataba. Kwa hiyo, kwa sababu sheria haina tabia ya kurudi nyuma, siyo *retrospective,* kuanzia kanuni hii iliporekebishwa wote wanaoingia katika makubaliano mwenye leseni na anayetaka kupanga eneo lazima wa-*comply.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, kiwango wanachowekeana ni maridhiano yao na sisi kama Wizara wakishasajili mkataba tunausimamia, yale yaliyopita wahenga wanasema si ndwele tugange yaliyopo na yajayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Injinia Mwita Chacha.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Nianze kwa kuipongeza Wizara ya Madini, ndugu yangu Mavunde kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, lakini pamoja na hayo ninaomba kuuliza swali moja.

Mheshimiwa Spika, tunajua kabisa kwamba suala zima la *double taxation* limekuwa halikubaliki lakini kwenye Wizara hii ya Madini suala zima la mrabaha tumeona *double taxation* mara kadhaa ikifanyika. Kuna baadhi ya mikoa ambapo tuna-*charge* mara mbili. Mara moja tuna-*charge* wakati mchimbaji anavyokuwa anagawa mawe pia wakati mwingine mchimbaji huyu aki-*process* akipata dhahabu akifika kule sokoni tena anatozwa mrabaha. Je, Wizara imejipanga vipi au ina mpango gani kuhakikisha kwamba suala zima hili la *double taxation* tunaliondoa na huyu mchimbaji aende kulipa kodi moja kwa mara moja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba kodi zilizoidhinishwa rasmi na Wizara ni kodi ya mrabaha, kodi ya ukaguzi wa leseni na ile ya *service levy* inayokwenda kwenye halmashauri. Hizi tozo anazoongelea Mheshimiwa ni tozo ambazo watu wanapotoa madini mgodini na wakati huo ni mawe tu, anayetoa mawe mgodini, anapoyapandisha pale siyo yeye anayepeleka sehemu ya kuchakata yale madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna namna sisi tunaweza tukasubiri yaende mpaka kule mwisho wa eneo itakapotumika kuweza kuchaji. Kwa hiyo, anatozwa kwa asilimia ya mawe aliyogawa pale baada ya kutoa na yule anayekwenda kuchakata anawekewa kiwango ambacho kinalingana na zile tozo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tuko katika mpango wa kuhakikisha kwamba katika migodi yote uchenjuaji ufanyike palepale ili mawe yotozwe kodi ya Serikali baada ya kuwa yameshachakatwa.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara.

Na. 9

**Kubadili Kanuni za *CSR* kwenye Migodi**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini Kanuni za *CSR* kwenye migodi zitabadilika ili miradi ya maendeleo isimamiwe na halmashauri kwa mtindo wa *Local Fund* badala ya mwekezaji?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini ilitunga Kanuni za Wajibu wa Wamiliki la Leseni kwa Jamii *(CSR/Corporate Social Responsibility)* na kuanza kutumika mwezi Juni, 2023 zikiwa na lengo la kusimamia utekelezaji wa *CSR* ili kuhakikisha jamii zinazozunguka migodi zinanufaika ipasavyo na uwepo wa migodi husika. Kanuni hizo zimeeleza bayana wajibu pamoja na majukumu ya wadau muhimu wanaohusika na *CSR* ambao ni mmiliki wa leseni au mgodi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (halmashauri).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Miradi ya *CSR* Kanuni ya 15(1) imeeleza mmiliki wa leseni ya madini atawajibika kutekeleza mpango wa wajibu wake kwa jamii kwa kuzingatia taratibu na ununuzi na anaweza kumwajiri mkandarasi au mtu mwingine yeyote katika utekelezaji wa miradi iliyopo katika mpango. Aidha, Wizara ya Madini imeendelea kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuboresha kanuni za *CSR* zilizopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Halmashauri ikiendesha utaratibu wa manunuzi, darasa ambalo tunajenga kwa shilingi milioni 25 mkandarasi akiwekwa na mgodi unatumia shilingi milioni 32, nyumba *single* ya shilingi milioni 50 mkandarasi anaweka kwa shilingi milioni 85, nyumba pacha

ambayo tungetumia shilingi milioni 70 kwa halmashauri, mkandarasi ni shilingi milioni 125. Bweni la shilingi milioni 130 wanapiga mpaka shilingi milioni 230.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza; ni kwa nini fedha ile isibaki kwenye mgodi, lakini mchakato wa manunuzi ufanywe na halmashauri ili kuokoa fedha hizo na tupate miradi mingi zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kanuni hizi zimetoa *provision* ambayo inaonesha kwamba kuna *team* ya wataalam ya kuibua miradi. Mbunge hayupo mle ndani kwenye hiyo *team,* wala Mwenyekiti wa Halmashauri, wameshachakata, wamepanga miradi yao, wanaleta kwenye Kamati ya Fedha au Baraza la Madiwani unakuta hata Mbunge hayupo, unatakiwa uende kuunga mkono kitu ambacho hukijui. Je, kwa nini, katika mchakato wa kuibua miradi ile Mwenyekiti wa Halmashauri au Mbunge asiwekwe ili waanze pamoja kupanga miradi ya maendeleo ya halmashauri husika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la manunuzi kutokana na fedha za *CSR* limebainishwa vizuri sana kwenye kanuni hizi ambazo tumezitunga mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuibua miradi unaanzia kwenye ngazi ya kijiji, inaenda ngazi ya kata inaenda kwenye halmashauri na Mbunge pia ni Mjumbe katika Halmashauri ya Wilaya yake au Jimbo lake. Kwa hiyo, miradi inapokuwa imeibuliwa, inapokwenda kwenye ngazi ya kutenga fedha na utekelezaji, Kamati ya Wataalam hukaa ambayo Mwenyekiti wake ni Mkurugenzi wa Halmashauri na Katibu wake Afisa Mipango, kuna mwakilishi wa Tume ya Madini na kuna wawakilishi wawili wa mwenye mgodi.

Mheshimiwa Spika, ule mchakato wa manunuzi hufanyika kwa uwazi kabisa na anachoongelea Mbunge ni zamani kabla hatujawa na kanuni. Sasa hivi miradi yote japokuwa mwenye

kutoa fedha ndiye anayesimamia akishirikiana na ile Kamati ya Wataalam, lakini Mbunge ameachwa pembeni ili awe sehemu ya *check and balances,* kufuatilia kama wajibu wake ulivyo kuona kwamba fedha ile imeenda kutekeleza miradi iliyokusudiwa kwa usahihi.

Mheshimiwa Spika, Mbunge anapoongelea suala la fedha hii kwa nini manunuzi yasifanyike moja kwa moja na halmashauri ni suala ambalo limefungwa kikanuni, lakini kuhusu uibuaji wa miradi ni suala ambalo linaanzia kwenye jamii, kwa hiyo hakuna kinachofanyika na mwekezaji bila ushirikishwaji wa jamii, ahsante sana.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mattar Ali Salum.

Na. 10

**Safari za Ndege Zanzibar – Dodoma**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza: -

Je, kwa nini Shirika la Ndege la Tanzania lisianzishe safari za ndege za moja kwa moja toka Zanzibar mpaka Dodoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nisimame na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kwa nafasi ya Naibu Waziri wa Uchukuzi. Ahadi yangu kwake ni kuendelea kufanya kazi hii kwa uaminifu, uzalendo na uadilifu mkubwa huku nikiwaahidi Waheshimiwa Wabunge ushirikiano wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa hili ni Bunge letu ni la kwanza tangu nchi yetu ifanye tukio kubwa la kihistoria kule Mwanza, ninatumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa

kuzindua rasmi meli ya *MV Mwanza*, meli kubwa ya kwanza katika nchi yetu ambayo inabeba abiria 1,200, tani 400 na magari makubwa na madogo ya kutosha, itakayokuwa inaunganisha nchi yetu pamoja na nchi jirani. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuzindua meli hii kubwa kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ndege Tanzania kwa sasa inafanya safari za ndege kutoka Zanzibar mpaka Dodoma kupitia Dar es Salaam. Uamuzi wa kupitia Dar es Salaam ni wa kibiashara ili kuhakikisha ndege inakuwa na ujazo wa kutosha. *ATCL* inaendelea kuangalia fursa ya kuanzisha safari za Zanzibar na Dodoma punde idadi ya abiria itapoongezeka na kuwezesha ndege kuwa na ujazo wa kutosha angalau wa 80%.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa; lakini nina maswali mawili ya nyongeza, la kwanza; ninaomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge na Watanzania kuhusu mafanikio ya *ATCL* tangu Serikali ianze kuwekeza fedha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni upi mpango wa *ATCL* kushika soko la kimataifa likawa kama mashirika mengine makubwa ya duniani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI**: Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge na Watanzania tuna mengi ya kujivunia kwa *ATCL*. Tumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa kuamua rasmi kuliboresha shirika letu la ndege la Tanzania. Katika miaka hii mitatu au minne ambayo Mheshimiwa Rais ameamua kuwekeza tumeona mabadiliko mengi. Kwanza, idadi ya ndege imeongezeka.

Mwaka 2016 tulikuwa na ndege moja, ilipofika mwaka 2021 tukawa na ndege tisa. Mheshimiwa Rais ameongeza ndege ziko 16 ikiwemo na ndege kubwa ya mizigo; na hivyo imepelekea mzigo unaosafirishwa kuongezeka kutoka tani 1,290 hadi tani 6,900, haijawahi kutokea. Hata idadi ya abiria imeongezeka mara dufu kutoka abiria 537,000 sasa wako abiria 1,100,000.

Mheshimiwa Spika, hata mtandao wa ndege umeongezeka, hapo awali tulikuwa tunakwenda vituo vichache na leo ninapozungumza *Air Tanzania* inakwenda vituo takriban ukanda wote wa kusini; inakwenda takriban mikoa yote Tanzania ambapo viwanja imekamilika. vilevile Inakwenda kwenye maeneo ya kimataifa kama Guangzhou, Mumbai na Dubai; hayo yote ni mafanikio. Fedha za kigeni zimeongezeka zaidi kutoka takriban fedha iliyokuwepo mwanzoni dola milioni 43 hadi 157. Kwa hiyo, tunayo kila sababu na sifa ya kujivunia maboresho makubwa ya shirika letu la *Air Tanzania*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ametaka kufahamu, kwamba je, ni mipango gani ambayo shirika inayo ya kuhakikisha kwamba linakuwa *competitive* na kushindana na mashirika makubwa duniani. Kwanza kabisa ni kuongeza idadi ya ndege. Ukimsikiliza Mheshimiwa Rais alipokuwa anahutubia Bunge na mara kwa mara akizungumzia sekta hii ya uchukuzi, anataka kuongeza ndege. Ukisoma Dira 2050 na Ilani ya CCM kwa umoja wake ifikapo 2030 zitaongezeka zaidi ya ndege nane hadi 10 ukilinganisha na zilizopo sasa hivi. Pili, pamoja na kuongeza ndege ambazo pia tunakwenda kuongeza vituo vya kimataifa, sasa hivi tuna vituo vitatu kama nilivyosema, *ATCL* ina mpango wa kuongeza vituo vingine saba na kwenda juu ili iende Ulaya, Asia na maeneo mengine ya dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, *ATCL* iliyojipanga kufanya majukumu yake kibiashara inakwenda kukodi ndege. Mashirika mengi duniani pamoja na kumiliki inakodi ndege zingine ili kuweza kushika soko la kimataifa; na sisi tunatengeneza *balance sheets* zetu vizuri ili tuongeze ndege nyingi zaidi, twende duniani kote tuweze ku-*compete* kama mashirika kwa mengine yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, tulikuwa na changamoto ya wataalam, sasa hivi tunamiliki ndege 16 lakini changamoto kubwa ni marubani. Tuna upungufu wa marubani 61 pamoja na wahandisi, *(professional engineers)*. Ni nini tunakifanya kama shirika? Kwanza ni kuhakikisha tunajenga Chuo Kikuu cha Anga pale *KIA* ambacho kitajengwa hapo baadaye. Pili, kuboresha chuo chetu cha *NIT*. Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi ili marubani wapate vifaa na utaalam wa kutosha. Kama hiyo haitoshi, tunatoa rai kwa Watanzania kupeleka vijana wetu kwenda kusoma kwenye kada ya urubani pamoja na uhandisi wa ndege kwa sababu huko hawatoshi, tunahitaji wengi waende huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi ni kuimarisha diplomasia yetu. Kama ambavyo Wabunge wanafahamu, Mabalozi wetu katika dunia hii wanafanya kazi nzuri sana na ninatumia nafasi hii kuwapongeza sana kwa sababu ndio ambao wametupatia masoko. Hivi ninavyozungumza mwezi huu tunakusudia kuongeza kituo kingine Accra, Ghana. Hii ni kazi nzuri ya wanadiplomasia wetu wanayoifanya huko duniani. Kwa hiyo, kote huko tutakwenda kufika na hii yote inafanywa na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, tunakamilisha uwanja wa Msalato. Uwanja huu ni wa kimataifa, maana yake unapoongeza viwanja vya kimataifa shirika lako la ndani linapata nguvu na uwezo wa kuongeza *scope* ya kutoka hapa na kwenda kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, mipango ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye sekta ya anga hususan kuboresha shirika letu la *ATCL* ni mikubwa, tumwombee Rais wetu afya njema ili maono yake yaweze kutimia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwanza hongera. Nilikupa muda mwingi sana kwa sababu nilikuwa ninajua ndiyo unachangia na hotuba ya Rais. Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Ritta.

Na. 11

**Ujenzi wa Barabara ya Kibaoni – Dabaga na Idete**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Kibaoni – Dabaga na Dabaga hadi Idete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako ninaomba kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kumsaidia kwenye nafasi hii ya Naibu Waziri wa Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuhakikishia na Waheshimiwa Wabunge hawa kwamba nitatoa ushirikiano kwa 100%. Baada ya kusema hayo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kibaoni – Dabaga na Dabaga hadi Idete ni sehemu ya Barabara ya Ipogolo – Idete yenye urefu wa kilometa 67.47. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii umeanza kwa sehemu ya Ipogolo – Kilolo yenye urefu wa kilometa 33.61 chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Programu ya *RISE* ambapo utekelezaji wake umefikia 98%. Sehemu iliyobaki ya kutoka Kilolo – Idete yenye urefu wa kilometa 33.86, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza ninaomba kuishukuru Serikali kwa majibu

na ujenzi wa barabara ya kilometa 33.6 kutoka Ipogolo – Kibaoni. Ninamwomba Mwenyezi Mungu ambariki sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; changamoto kubwa ya Wilaya ya Kilolo ni barabara zake hazipitiki kabisa kipindi cha mvua. Tuna barabara inayotoka Kilolo – Kising'a – Ukwega – Wotalisoli – Mlafu – Ilula. Hii barabara ni ya kiuchumi mkubwa kabisa lakini haipitiki wakati wa mvua. Je, Serikali ipo tayari sasa kufanya upembuzi yakinifu kwa maeneo korofi tu ili kuweza kujengwa kwa kiwango cha zege ili barabara hizi ziweze kupitika mwaka mzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Barabara ya Kitonga ni barabara ya kiuchumi na kimataifa, lakini kuna eneo kama la kilometa 7.6 ambalo linatakiwa kufanyiwa upanuzi. Tunashukuru Serikali imeshatupatia fedha ya kilometa 1.6 na upanuzi unaendelea. Je, Serikali iko tayari sasa kwa kilometa hizi sita iweze kutoa fedha ili lile eneo korofi lote lipanuliwe ili magari yasiendelee kukwama na kupata ajali kubwa katika Mlima Kitonga? Ikiwezekana Mheshimiwa Waziri aje aone adha kubwa ya wananchi inayotokea katika Mlima Kitonga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara aliyoitaja ya Kilolo – Watalisoli – Ilula kwa sasa Wizara kupitia *TANROADS* inafanya upembuzi yakinifu kwa barabara yote. Pia, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba mpango wa Wizara sasa hivi, maeneo yote ambayo ni korofi kwenye miinuko na yale ambayo yanakwama, mpango sasa ni kuyadhibiti kwa kujenga ama lami ama zege ili iweze kupitika kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake namba mbili ambalo linahusu Barabara ya Kitonga. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hii ni barabara ya kitaifa na ndiyo barabara ambayo ninadhani ni kubwa kuliko zote katika nchi hii *(T1)*. Serikali tumeshaanza kufanyia marekebisho eneo la Kitonga ambalo

lilikuwa linakwamisha mizigo mingi sana ambayo inaenda DRC na Zambia. Tumeshaanza na tumeshamaliza kilometa 1.7. Katika mwaka huu tunategemea kwamba tunaweza tukaikamilisha yote ili tusiweze kupata changamoto ya magari mengi ambayo yanapita katika barabara hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Nsekela.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaungana na wenzangu kumtakia heri ya kuzaliwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaishukuru Serikali kwa kutuletea mkandarasi wa kujenga Barabara ya lami kutoka Kyerwa kwenda Omurushaka, kilometa 50. Hata hivyo, *speed* yake ni ndogo sana. Je, Serikali ina mkakati na maelekezo gani ya kumsimamia mkandarasi huyu ili amalize barabara hii ili kukidhi kilio cha wananchi wa Kyerwa? Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli mkandarasi huyu anakichofanya ni sanifu jenga Barabara ya Kyerwa kwenda Omurushaka. Nimwagize Meneja na Mhandisi Mshauri anayemsimamia ahakikishe kwamba huyu mkandarasi, kwa sababu alikwishalipwa fedha ya awali, aweze kwenda kwa kasi inayotakiwa kulingana na mpango wake wa kazi ambao ameupanga na tumeukubali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru. Barabara ya kutoka Omugakorongo – Kituntu – Rwambaizi – Igurwa – Murongo ipo katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, imekuwa kwenye manunuzi kwa muda mrefu, ni barabara muhimu kwani

inaunganisha nchi yetu na nchi za Afrika Mashariki; na kujengwa kwa kiwango cha lami kutainua uchumi wa Kagera pamoja na Taifa letu. Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni kati ya zile barabara zetu kuu, inaunganisha Uganda na Tanzania kupitia Daraja la Murongo. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba hii barabara ilikuwa imetangazwa na tulipata mkandarasi, lakini tukashindwana naye kimkataba. Hivyo, hii barabara imetangazwa tena, iko kwenye hatua za manunuzi kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Tunaanzia Murongo kuja Omugakorongo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Baba Levo, Waheshimiwa Wabunge, Baba Levo ni jina lake rasmi ambalo tumethibitisha amelifanyia kiapo. *(Makofi)*

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa ni swali moja tu.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Ninaomba majibu kutoka kwa Serikali kuhusiana na Barabara ya Kasulu, barabara ambayo itakwenda kuwasaidia wananchi wa Kata za kama Machinjioni, Rubuga, Kagera pamoja na Kata ya Majengo. Barabara iliyopo sasa hivi inawalazimisha wananchi hawa wakitaka kwenda kwenye kata zao lazima wafike mjini halafu warudi nyuma. Ikijengwa Barabara hii ya Kasulu kuanzia pale Msimba kuelekea Ujiji itasaidia wananchi hawa wasiingie mjini wapate *shortcut* ya kwenda kwenye makazi yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge Baba Levo, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuna wakala mbili za barabara, *TANROADS* na *TARURA*. Mheshimiwa Mbunge, Barabara tunazozijenga sisi ni kuanzia Ujiji hadi Kigoma Mjini, Mwanga kwenda Mwandiga, pale kwenye Sanamu ya Sokwe kwenda Simbo na Mwandiga. Hizi barabara nyingine tutahakikisha kwamba tunawasiliana na wenzetu wa *TARURA* ili kuhakikisha hizo barabara zinajengwa na wananchi wasipate changamoto kama alivyozielezea Mheshimiwa Mbunge. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Barabara ambayo inaanzia *keep left* inakwenda mpaka Mogabiri yenye kipande cha takriban kilometa 9.3 iliyopo Tarime Mjini imeharibika sana kiasi cha kupelekea ajali mbaya sana na wakati mwingine vifo. Hata hivyo, kwa sababu tayari mkandarasi yupo na yupo tayari kuanza kazi anasubiri tu malipo ya awali, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kupeleka fedha hizi ambazo ni takriban shilingi bilioni 7.9 ili barabara hii iweze kutengenezwa na kuunganishwa na ile barabara inayoenda mpaka Nyamwaga ambayo tayari imeshakamilika? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kipande hicho ni kweli kimeharibika, kilikuwa na lami, lakini barabara ilitangazwa yote. Ilibidi tuanze mbele ili baadaye tuweze kufumua kipande hiki ambacho amekiongelea Mheshimiwa Mbunge. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunajua kwamba hatuwezi tukatoka na barabara ya vumbi kutoka Tarime halafu tukaenda kuipata lami mbele. Kwa hiyo, nimhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tunaandaa

malipo ili mkandarasi aweze kulipwa na kuanza kuikarabati, ambayo ni sawa na kuijenga upya hiyo barabara ambayo ina zaidi ya kilometa tisa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, Mbunge wa Ngara.

Na. 12

**Ujenzi wa Barabara ya Nyakahura – Rulenge – Murugarama (Ngara)**

**MHE. DOTTO J. BAHEMU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Nyakahura – Rulenge – Murugarama kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nyakahura – Rulenge – Murugarama yenye urefu wa kilometa 85.6 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sasa maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kuanzia Keza yanaendelea, ambapo tayari mkandarasi amepatikana na taratibu za malipo ya awali zinaendelea ili aweze kuanza kazi. Mara baada ya taratibu za malipo ya awali kukamilika kazi za ujenzi zitaanza. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara yote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dotto.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vile vile, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini majibu kama haya si mara ya kwanza kuyasikia hapa Bungeni kwa sababu mwaka jana mwezi Aprili wakati Mheshimiwa Waziri akijibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ngara aliyepita, alisema kwamba Serikali tayari ilikuwa katika

hatua za mwisho za kumlipa mkandarasi ili kazi ianze kufanyika. Sasa leo, majibu ni kama yale yale ya mwaka jana. Sasa ningependa kupata kauli ya Serikali katika maswali yangu mawili.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; je, ni lini sasa kazi rasmi ya ujenzi itaanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, katika eneo la Keza ambalo amesema ndiyo ujenzi utaanza; wanaanza kutoka Keza kwenda Nyakahura au Keza kwenda Murugarama kwa sababu Keza ni katikati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi yetu inachukua muda mrefu na ndiyo maana bado hatujasimamisha, tunaendelea na utaratibu wa kuijenga. Pia, kama nilivyosema kwamba barabara hiyo itajengwa, itaendelea kujengwa na bajeti yake imeshakamilika na ndiyo maana tayari tumeshapata mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo tutajenga kuanzia Keza – Nyakahura kwa hatua ya kwanza wakati tunasubiri *lot* ya pili kutoka Keza – Rulenge – Murugarama. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, barabara hii inayoongelewa na Mbunge wa Ngara, inaunganisha Jimbo la Biharamulo na Jimbo la Ngara. Kwa hiyo Nyakahura iko kwangu lakini baadhi ya wananchi waliosimamisha shughuli zao kupisha ujenzi wa barabara hii hawajalipwa fidia mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa ninataka kujua kauli ya Serikali, wana mpango wa kujenga bila kulipa fidia au *plan* ya fidia ni miongoni mwa hiyo *process* ya kujenga ili wananchi wangu

wanaofuatilia hapa waweze kujua ni lini wananchi waache shughuli zao za maendeleo waweze kuwapisha wajenge hiyo barabara? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita haiwezi ikabomoa nyumba za wananchi kabla ya kuifidia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pale tutakapoanza kuijenga ni pale ambapo tumelipa fidia kwa wananchi ambao wanastahili fidia kwa mujibu wa sheria. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kija.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nina swali moja kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni lini Barabara ya *STAMICO* – CCM – Ushirombo itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuondoa adha ya wananchi kwa sababu barabara ilishaandaliwa katika mfumo wa kuwekewa lami, lakini sasa hadi leo haijawahi kujengewa lami na watu walibomolewa nyumba kusogea ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami? Ni lini Serikali itaamua kujenga kutoka *STAMICO* – CCM – Ushirombo kwa kiwango cha lami ili kuondoa vumbi na kero inayowapata wananchi wa Jimbo la Katoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashirikiana na wenzetu wa *TARURA* kama Serikali kuhakikisha kwamba kama tayari wameshabomolewa watu, basi mpango upo. Hata hivyo, tutashirikiana na wenzetu wa *TARURA* kuhakikisha kwamba hiyo barabara inajengwa. Kwa sisi *TANROADS*, barabara yetu ni kutokea Ushirombo kuja Katoro (ile barabara kubwa ambayo ndiyo tunashughulikia).

Mheshimiwa Spika, hiyo barabara nyingine, tutaongea na wenzetu wa TAMISEMI kupitia *TARURA* tuone wamefikia hatua

gani ama baada ya hapa nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuje tukae tuone ni barabara ipi hasa anayoisemea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninaomba kufahamu ni lini Serikali itakamilisha rasmi taratibu za awali ambazo zimesuasua kwa muda mrefu ili ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba uweze kuendelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara aliyoitaja tulishapata mkandarasi na bahati nzuri siku za karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea na alitoa maelekezo mahsusi kwa Wizara ya Ujenzi kuhakikisha kwamba mkandarasi yule ambaye anatakiwa kulipwa shilingi bilioni 3.7 ziweze kutafutwa. Tayari Wizara imeshaanza kutafuta hizo fedha kama yalivyokuwa maelekezo mahususi ili barabara hiyo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Neema Mwandabila.

Na. 13

**Kuupatia Fedha Mfuko wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuupatia fedha za uendeshaji Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ili kuwafikia wananchi wengi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, na ahadi yangu kwake ni siku zote tu kazi itaendelea na tutaifanya kwa uaminifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha ili kuuwezesha Mfuko wa Pembejeo za Kilimo kupata fedha za uendeshaji na mitaji kwa wakulima hususan vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali iliidhinishiwa na Bunge shilingi bilioni 10 kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa vijana na wanawake. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi bilioni sita kwa ajili ya kukopesha wakulima kupitia Mfuko huo. Hadi Desemba 2025, jumla ya mikopo 27 imetolewa yenye thamani ya shilingi bilioni 5.49. Kati ya mikopo hiyo, mkopo wa shilingi bilioni tano ni mkopo uliotolewa kwa Benki ya Ushirika *(Coop Bank)* ambapo vijana na wanawake wanaojishughulisha na kilimo katika Ushirika wanakopeshwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo, 13% ni kwa ajili ya usimamizi wa mikopo ikiwemo kutembelea wateja na kufanya ukaguzi. Serikali itaendelea kuuwezesha Mfuko wa Pembejeo za Kilimo fedha za uendeshaji kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake ili kuhakikisha kilimo kinafanyika kwa tija. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Niseme tu, kutokana na kwamba Benki ya Ushirika kuweza kupata shilingi bilioni tano kutoka kwenye Mfuko wa Pembejeo, ni wazi inaonyesha yenyewe kama yenyewe haina mtaji. Swali la kwanza; ninataka kufahamu, kitendo cha Mfuko wa Pembejeo kutoa shilingi bilioni tano kwa Benki ya Ushirika, hawaoni kwamba Mfuko umepoteza mantiki ya kuwafikia wananchi wanyonge?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; 13% ya shilingi bilioni sita ni shilingi milioni 780, hii inaenda kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko. Sasa ninataka kufahamu, kitendo cha kuweka shilingi milioni 780 kufuatilia madeni ambayo yameenda kwenye mikopo 27 tu, hawaoni kama haya yatakuwa ni matumizi mabaya ya rasilimali za Taifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake na ninamthibitishia tu kwamba Serikali ambayo ni Wizara ya Kilimo kutumia Benki yake ya Ushirika *(Coop Bank)* na Serikali kutoa fedha kutoka *AGITF* kupeleka *Coop*, lengo ni kuongeza wigo mpana kwa ajili ya kuwafikia wakulima na hicho ndicho ambacho tumekifanya kwa sababu Ushirika inawagusa wakulima moja kwa moja kupitia maeneo ya Vyama vya Ushirika *(AMCOS)* pamoja na *SACCOSS* zake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tumefanya hivyo kwa lengo la kuboresha ili tuweze kuwafikia wakulima wengi na mikopo yote hii inayotolewa, inatolewa kwa asilimia saba, asilimia ambayo haiko katika benki nyingine yoyote inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, suala la usimamizi. Fedha yoyote inahitaji usimamizi na ni lazima tufuate sheria za nchi na sheria zinazohusiana na usimamizi wa fedha ili kuhakikisha kwamba kila kinachotolewa lazima kifikie malengo yake. Hili lililowekwa ni lengo na siyo kwamba fedha zote ambazo zimetajwa hapa zinatumika kwa 100% kama ambavyo tumeainisha. Kwa hiyo ni kama *target* tu katika mwaka, lakini kiukweli katika matumizi inakuwa ni pungufu na hicho ambacho Mheshimiwa Mbunge amekiainisha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Salma.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaomba kukupongeza na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri ambazo amezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo tuko kwenye Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Rais wetu amejipambanua vyema kabisa katika eneo la kilimo kuhakikisha kwamba anaongeza bajeti kubwa na ya kutosha ili Tanzania iweze kujilisha yenyewe hatimaye Afrika na tuweze kuilisha dunia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tunazungumzia suala la pembejeo, pembejeo hizi ni muhimu sana kwa kuwa bila pembejeo uzalishaji unakuwa ni chini. Sasa swali langu ni kwamba, Wizara tuliomba na walitupangia kutupatia pesa shilingi bilioni 31.3 kwa ajili ya bonde letu la Kinyope. Je, Serikali lini mtatupatia hizi pesa shilingi bilioni 31.3 ili tuendeleze kilimo na kilimo hiki kitaleta manufaa kwa vijana pamoja na wanawake?

Mheshimiwa Spika, ninaomba jibu la Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge mama Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga, anafanya kazi nzuri sana katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, ninamthibitishia tu kwamba maelekezo ambayo Serikali imeshatoa katika hili bonde ambalo ameliainisha na maombi ya fedha ya shilingi bilioni 31.3, tayari Wizara ya Kilimo tumeshayapeleka Wizara ya Fedha na tunasubiri tu taratibu zikamilike ili tuhakikishe bonde lile linakamilishwa na linaanza utekelezaji wake kama tulivyoainisha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana.

Na.14

**Kufufua Viwanda vya Kuchakata Samaki Mwanza**

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Sekta Binafsi kufufua Viwanda vya kuchakata samaki ili kuongeza ajira na mapato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kumsaidia kama Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Ninamuahidi kwamba nitafanya kazi hii kwa weledi, nguvu, bidii kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa John Fransisco Nzilanyingi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mpango kabambe wa kuendeleza Sekta ya Uvuvi wa mwaka 2021 – 2037 ambapo kipaumbele ni kuendeleza, kuanzisha, kuimarisha na kufufua viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi nchini ili kufikia kwenye uchumi wa viwanda unaoongozwa na sekta binafsi kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha viwanda vyetu vinafanya kazi kulingana na matarajio ya Serikali, Wizara ipo katika hatua za maamuzi kulingana na taratibu za Serikali kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi na kupambana na uvuvi usiozingatia sheria ili kuongeza upatikanaji wa samaki na hivyo kuwezesha viwanda vyetu kupata malighafi za kutosha. Kwa hatua za awali Wizara imeweka maboya 32

yenye thamani ya shilingi milioni 224 kwa ajili ya kulinda mazalia ya samaki katika eneo la Luchelele - Ziwa Victoria, Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi, Wizara imeanzisha Dawati la Mitaji na Uwekezaji kwa lengo la kufuatilia kwa ukaribu changamoto zinazoikabili Sekta Binafsi (vikiwemo viwanda hivi vya samaki), kuzitafutia ufumbuzi na kuongeza uwekezaji na uchangiaji kwenye pato la Taifa ili kufikia azma ya Serikali ya kuelekea kwenye Uchumi wa Viwanda. Aidha, mipango mingine ya Wizara ni pamoja na kuhamasisha ufugaji wa samaki kwa vizimba ili kuwezesha upatikanaji wa samaki kwa wingi. Mpango huu utasaidia kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda. Ninashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Fransisco.

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi nyingine ili niweze kupata kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni nini mpango wa Serikali wa kupambana na uvuvi haramu ambao unatajwa ndicho chanzo cha uhaba wa samaki na hivyo kupelekea viwanda vingi vifungwe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika majibu ya Serikali, pamoja na jitihada ambazo inafanya za kuhamasisha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba, Serikali bado haioni kwamba tutaendelea kuwa na changamoto ya upungufu wa samaki kwa sababu viwanda vyetu havitumii samaki aina ya sato ambaye ndiye hasa anafugwa kwenye vizimba vya samaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri. Katika swali la kwanza, Serikali inatambua uzito wa changamoto ya uvuvi usiozingatia sheria na athari kubwa ambazo uvuvi huu umeleta katika uchumi wetu na ndiyo maana mpaka sasa

tunaendelea na jitihada mbalimbali na mipango ya kupambana na uvuvi huu haramu ikiwemo kuunda Mamlaka ya Uvuvi ambayo iko katika hatua mbalimbali na Mamlaka hii itapewa nguvu ya kisheria na kikanuni ya kupambana na uvuvi huu haramu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea na doria mbalimbali za ulinzi kwa kushirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ikiwemo Jeshi la Polisi na Jeshi letu la Ulinzi wa Wananchi ili kuhakikisha tunaendelea kupambana na uvuvi huu usiozingatia sheria. Serikali pia inaendelea kushirikisha jamii zetu katika kulinda rasilimali hizi za uvuvi kupitia *BMU* zetu ambazo tunazo katika mialo yote nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kutoa elimu kwa wavuvi wetu lakini pia tunaendelea kudhibiti uingizwaji na uuzwaji wa zana mbalimbali ambazo zinachochea au kuchangia katika uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, tunatambua pamoja na kwamba Serikali na kwa jitihada za Mheshimiwa Rais, tunaendeleza programu mbalimbali za kuwezesha Watanzania yakiwemo makundi mbalimbali ya vijana, wanawake na vyama vya ushirika kushiriki katika uvuvi kupitia uvuvi wa vizimba. Hata hivyo bado tunatambua kwamba uvuvi huu hauwezi kuwa mbadala wa uvuvi wa asili.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, ndiyo maana tunaendelea na jitihada mbalimbali za kupambana na uvuvi usiozingatia sheria, kuu zaidi ikiwa ni uundwaji wa Mamlaka hii ya Uvuvi ambayo utaratibu wake katika Mpango wetu wa Serikali unaendelea vizuri. Tunawaomba tu Waheshimiwa Wabunge kwamba pindi tutakapokamilisha taratibu zetu za kiserikali na kuleta mpango huu wa uundwaji wa Mamlaka hii, basi watuunge mkono ili tuweze kuipa nguvu hii ya kisheria na kikanuni kupambana na uvuvi huu usiozingatia sheria. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Yannick Ndoinyo.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla sijauliza kwa kweli ninatoa shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza ile ahadi yake ya kutujengea Barabara ya Gamba Gumu kutoka Ngorongoro kwenda kule mbugani Serengeti kwa kuwa ile barabara imeanza. Kwa kweli tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza kwa Wizara hii ya Mifugo, kama ambavyo tunatambua, viwanda ni nyenzo muhimu sana ya kuongeza thamani ya mifugo na kuongeza masoko na kipato cha wananchi wafugaji. Wilaya yangu ya Ngorongoro wananchi wakazi karibu 98%…

**SPIKA:** Mheshimiwa nenda kwenye swali moja kwa moja.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Spika, je, Wizara hii ina mpango gani wa kutujengea kiwanda cha nyama cha kusindika mazao ya mifugo ili kuongeza kipato kama vile inafanya kwa samaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika utaratibu wa kufanya mambo yafuatayo ili kuhakikisha tunaongeza uwekezaji wa viwanda vya nyama na kuongeza tija kwa wafugaji wetu. Kwanza ni kuendelea kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ili waweze kuwekeza katika sekta hii ambayo kwa kiasi kikubwa ina uwezo wa kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili, tunaendelea kuwahamasisha wafugaji wetu ili kuendelea kufanya ufugaji wa kisasa kuongeza tija na ubora wa mifugo yao ili pindi tunapofanya uwekezaji huu, basi mazao haya tunayoyapata katika mifugo yetu yaweze kuwa na ubora mzuri ili kukidhi soko la ndani na nje katika nchi yetu. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Serikali ilikuja na mpango mzuri sana wa kuwakopesha wavuvi vizimba vya kufuga samaki ndani ya Ziwa Victoria. Tatizo limekuwa usambazaji wa vifaranga pamoja na chakula kwa wale wazabuni ambao wanatakiwa kufanya hivyo. Mfano mzuri wa kuchelewesha usambazaji wa vifaranga na chakula, ni kwa huyu mvuvi anaitwa Japhet Moya Rogombero Ngeresi Nyamuguru ambaye alipata vifaranga baada ya miezi tisa wakati vizimba vilikuwa ndani ya maji.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hizo kero zinaondolewa ili mikopo hii iwe na tija kwa ajili ya Taifa letu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Serikali pamoja na kutoa uwezeshaji huu, tunaendelea kufanya tathmini ya karibu sana kuona changamoto zote tulizonazo katika uvuvi huu wa vizimba. Moja ya changamoto ambayo wavuvi wetu wamekutana nayo ni ucheleweshwaji wa vifaranga pindi wanapolipia kwa wale wazalishaji. Tayari tumeshaanza kufanyia kazi changamoto hii, moja ikiwepo sisi wenyewe kuanzisha na kuendeleza vituo mbalimbali vya uzalishaji wa vifaranga bora ili pale ambapo wavuvi wetu wanavihitaji, waweze kuvipata kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hata kwa wale ambao wanazalisha kama sekta binafsi, tunaendelea kuwafuatilia na kufanya nao kazi kwa karibu ikiwepo kuwaratibu ili pale mfugaji au mvuvi anapolipia vifaranga vyake, kwanza aweze kuvipata kwa wakati, lakini pili aweze kupata idadi sahihi aliyolipia.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja.

Na. 15

**Udhibiti wa Tembo – Mkinga**

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA** aliuliza:-

Je, ni lini Tembo wanaojeruhi na kuharibu mali majumbani na mashambani maeneo ya Mwakijembe, Bwiti, Daluni na Duga watadhibitiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaomba kumshukuru sana sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na kuingia katika awamu hii tukiwa salama.

Mheshimiwa Spika, pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini. Ninatoa ahadi kwamba nitafanya kazi kwa weledi mkubwa, uadilifu pamoja na ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga. Mkakati huu unajumuisha kuweka vikosi vya kudumu vya askari katika Kata za Bwita na Mwakijembe kwa ajili ya mwitikio wa haraka wa matukio ya wanyamapori katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea pia kutumia teknolojia za kisasa hasa visukuma mawimbi *(GPS Collars,* ndege nyuki pamoja na mabomu baridi katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo katika Wilaya ya Mkinga. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA S. MWAIKOJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Taasisi zetu za Serikali za *TANAPA, NCAA* na *TAWA* zinabaki na mapato ili kuweza kutoa huduma mbalimbali. Pamoja na kubaki na mapato (*retention)* bado tumekuwa na changamoto ya kuwapa waathirika hawa wanaokumbana na majanga haya ya wanyamapori kifuta jasho ambacho ni kidogo na kiwango hiki ni cha muda mrefu sana. Je, Serikali haioni haja sasa ya kufanya mapitio juu ya viwango hivi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; utaratibu wa kufanya uthamini kwa wananchi wanaopata majanga umekuwa na urasimu mkubwa sana na kusababisha baadhi ya wananchi kushindwa kufuatilia na kuendelea kuilalamikia Serikali yetu. Je, Serikali haioni haja sasa ya kufanya mapitio juu ya mchakato huu ili uwe rahisi na kuwaletea tabasamu wananchi wetu na hususan wananchi wa Jimbo la Mkinga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kabla ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Twaha Mbunge wa Mkinga, ninaomba nimpongeze sana pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishafanya marekebisho ya Kanuni ya Mwaka 2011, kanuni hiyo ilionekana ni kweli kifuta jasho ni kidogo imefanyiwa marekebisho mwaka 2024 kwa Tangazo la Serikali Na. 440, mwaka 2024, tarehe 31 Mei na imefanya marekebisho makubwa. Kwa sasa waathirika wale ambao watakuwa na ulemavu wa muda mfupi yaani majeraha ya muda mfupi watalipwa 50%, vifo vya mifugo 50%, uharibifu wa mazao 50%. Pia lipo ongezeko kubwa la vifo na ulemavu wa kudumu kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali tayari imeliona hilo suala la urasimu na kwa sasa tunatumia mfumo maalum unaotambulika kwa jina la *PAIS* yaani *Problem Animal Management Information System* ambao sasa urasimu hautopatikana, maana yake inarekodi moja kwa moja na kuhakiki taarifa zile na kupelekwa kwenye kanzidata. Nina imani kabisa kwamba urasimu huo sasa utakuwa umepata mwarobaini wake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ado Shaibu.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Kwa vile tatizo hili la tembo kuvamia vijiji na kuharibu mazao, kuuwa binadamu ni tatizo kubwa sana katika Jimbo la Tunduru Kaskazini na Wilaya ya Tunduru kwa ujumla wake. Ambapo kwa msimu wa kilimo wa 2025/2026 peke yake jumla ya waathirika 1791 wameharibiwa mazao yao na askari wa vijiji mpaka sasa wako 23 tu. Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa waathirika wote na kuongeza idadi ya askari wanyamapori wa vijiji *(VGS)*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeshaweka fedha na zimeshaingia na sasa tunafanya utaratibu wa kulipa kupitia mfumo. Kilichocheleweshа ilikuwa tunalipa *manual,* unaenda kijijini unaenda kulipa, pengine unaenda kulipa milioni tano unatumia gharama ya milioni nne, lakini kwa sasa tunatumia mfumo na mfumo huu umetuwezesha. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira hawa watu wetu watapata malipo yao.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini.

Na. 16

**Fidia kwa Waliopisha Uwekezaji wa Kitalu cha *Makere Forest Reserve***

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia Wananchi wa Kitongoji cha Katoto waliopisha Mradi wa Kitalu cha *Makere Forest Reserve?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya wananchi wa Kitongoji cha Katoto kuhama yalitolewa mwezi Oktoba, mwaka 2022 na Kamati ya Mawaziri Nane wa kisekta baada ya kubaini kuwa wananchi hao walikuwa nje ya mipaka ya Kijiji Mama cha Kagera. Serikali ilifanya tathmini ya kaya na makazi na kugawa eneo la ukubwa wa Hekta 4,446 katika Kitongoji cha Nyantuku, Kijiji cha Kagerankanda ambapo kila kaya ilipewa eneo la kujenga la ukubwa wa mita 32 kwa 64 na hekari tatu kwa ajili ya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali kupitia Kamati ya kisekta ya Mawaziri Nane, wananchi wa Katoto waliohamishwa walishapatiwa fidia ambayo ni ardhi kwa ajili ya makazi, kilimo na mifugo ikiwa ni pamoja na Serikali kuwapatia usafiri wa mali zao kipindi walichokuwa wanahama. Hadi kufikia mwezi Oktoba, 2025 uongozi wa Mkoa wa Kigoma kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Kasulu ulifanikiwa kuhamisha wananchi wote kutoka Kitongoji cha Katoto na kwenda Kitongoji cha Nyantuku, Kijiji cha Kagerankanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kinyoma.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, bado nina swali moja la nyongeza la kuiomba

Serikali kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari tuambatane naye kuelekea jimboni akaone na kujidhirisha namna zoezi lilivyotekelezwa na kusaidia kutatua migogoro inayoambatana na kitalu hiki cha *Makere Forest Reserve Uvinza Open Area.*

Mheshimiwa Spika, kitalu ambacho kinasabaisha mgogoro wa wananchi; wananchi kufyekewa mazao, kupigwa na kuna mgogoro wa kimapato na halmashauri kwa mfano kwa *DCC* ripoti tuliopata wanapata kama 1,900,000 tu. Pia kuna mgogoro wa Kacheri na Luguvu Relini ambao nao wameambiwa kuhamishwa, kuna mgogoro wa wananchi wenyeji nao wamechukuliwa maeneo yao na wakati walikuwepo pale tangu miaka ya 70.

Mheshimiwa Spika, pia kuna mgogoro wa *TFS* na wananchi wa kimpaka, wananchi wamewekewa *beacon* mpaka katikati ya vijiji. Ninaomba ikiwezekana Mheshimiwa Waziri aambatane nami twende jimboni kupunguza changamoto zinazokabili jimbo langu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unatakiwa uende jimboni jibu hilo tu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi niko tayari hata tukimaliza Bunge twende kwa wananchi wetu kuweka tabasamu kuondoa migogoro ambayo inawakabili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati Mheshimiwa Joseph Kamonga.

Na. 17

**Fidia kwa Wananchi wa Kijiji cha Liugai – Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini fidia kwa wananchi wa Kijiji cha Liugai Kata ya Luilo zitalipwa ili wapishe Mradi wa Umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nami ndio mara yangu ya kwanza kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu tokea kuteuliwa kuwa Waziri wa Nishati, ninaomba nitumie nafasi hii kipekee kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu na kuniteua kuweza kumsaidia katika sekta hii ya Nishati na ahadi yangu kwake kwamba sitomwangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niahidi Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wote kuwapa ushirikiano wa hali ya juu katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharious Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba, 2025 kazi ya uthamini wa fidia kwa wananchi wa Vijiji vya Lifua, Liugai, Masimavalafu katika Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe imekamilika ikiwa tayari kwa zoezi la uhakiki *(verification)* pamoja na uwekaji wazi jedwali kwa wafidiwa *(disclosure)*. Aidha, shilingi 6,025,053,947.72 zinatarajiwa kulipwa kwa wananchi 347 waliopisha utekelezaji wa mradi katika Vijiji vya Lifua, Liugai na Masimavalafu na malipo ya fidia kwa wananchi hao yanatarajia kufanyika mwaka wa fedha ujao wa 2026/2027.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Awali nianze kwa kuipongeza na kuishukuru sana Serikali kwa kutoa kiasi cha shilingi bilioni sita kwa ajili ya kurekebisha miundombinu ya umeme uliokuwa wa Madobe. Ahsante sana wananchi wa Ludewa wanaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niombe sasa niiulize Serikali. Swali la kwanza; Serikali itufahamishe wananchi wa Ludewa tunavyo viwanda vitatu ambavyo vinakusudiwa kujengwa kuanzia hivi sasa, lakini kituo cha kupoozea umeme kinatoka Madaba ambako ni mbali na hii inasababisha umeme kukatikakatika sana. Je, nini mpango wa Serikali kuweka bajeti kwa sababu tunaenda Bunge la Bajeti kwa ajili ya kutengeneza kituo cha kupooza umeme Ludewa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Ludewa ikihitajika kurekebishwa nguzo moja wanategemea gari kutoka mkoani. Sasa nini mpango wa Serikali kupeleka gari la kubebea nguzo Ludewa ili changamoto za wananchi ziweze kutatuliwa kwa wakati? Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid. *Aah! sorry.* Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Zacharious Kamonga Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza juu ya umeme wa uhakika katika Wilaya ya Ludewa na vile ambavyo amesema kwamba kuna viwanda vinaenda kujengwa. Nitoe taarifa mbele ya Bunge lako kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba sio Ludewa peke yake bali kila wilaya katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapata *substation* yake na tayari kuna mradi wa gridi imara ambapo tunamalizia hatua ya kwanza. Tutakapokwenda hatua ya pili kuna wilaya nazo zitapata *substation* hizo na katika hatua ya tatu Ludewa na yenyewe ipo itapata *substation* yake ili kuweza kuwa na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nitakaa pia na Mheshimiwa Mbunge ili kuona viwanda hivi vinaenda kuwekwa wapi kuona maeneo ambapo vinakwenda kuweka walau kwa hatua za mwanzo tuweze kuweka transfoma ili kuwa na umeme ambao ni wa uhakika kwa ajili ya wawekezaji hao wa Ludewa wakati

tunaendelea na Mradi wa gridi imara kuhakikisha umeme unapatikana.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la gari la nguzo. Ni majuzi tu Shirika letu la *TANESCO,* Tanzania limenunua magari ya nguzo zaidi ya 270 na hivi ninavyozungumza magari haya yameshapokelewa 200 na yameanza kusambazwa katika wilaya mbalimbali hapa nchini kwetu na nitaangalia Wilaya ya Ludewa na yenyewe iweze kupata gari lake kwa haraka ili nguzo ziweze kuwafikia wananchi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid.

Na. 18

**Maslahi kwa Walimu Wanaosahihisha Mitihani**

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi na stahiki za Walimu wanaosahihisha Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne na Sita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua na kuniamini katika nafasi hii ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Mwera. Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne na Sita ni mitihani muhimu ambayo usahihishaji wake hufanyika kwa baadhi ya walimu

kukusanywa katika vituo maalum kwa ajili ya jukumu hilo unaozingatia muda maalum, usalama, usiri, mazingira wezeshi na ubora wa kazi.

Mheshimiwa Spika, stahiki za Walimu wanaosahihisha Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne na Sita hulipwa kwa kuzingatia miongozo ya usahihishaji wa Mitihani kwa kipindi husika. Ili kuleta ufanisi wa kazi hiyo, miongozo hiyo imeendelea kuboreshwa mara kwa mara. Serikali itaendelea kuboresha maslahi na stahiki za walimu katika usahihishaji wa mitihani ya Taifa ili kuimarisha na kuongeza ufanisi wa kazi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Mohamed.

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini pamoja na majibu hayo nina swali la nyongeza. Serikali haioni haja kuandaa mwongozo wa dharura wa uboreshaji ambao utaweza kuzingatia kulipwa kwa posho ya kujikimu pamoja na posho maalum kwa walimu ambao wanasahihisha mitihani hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiboresha maslahi ya walimu wanaosahihisha mitihani kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo pamoja na posho wanazolipwa Serikali pia hulipa malazi, chakula, matibabu wakati wote wa kazi. Hata hivyo, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeupokea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Condester.

Na. 19

**Kupunguza Gharama za Vifurushi vya Simu**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali kupunguza gharama za vifurushi kwa Kampuni zote za simu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile nami ni mara yangu ya kwanza, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu na kuniteua kuwa msaidizi wake kama Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ninapenda niahidi kwamba nitafanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa kwa weledi kwa nguvu zangu zote na akili yangu yote.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa gharama nafuu kwa wananchi. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* na Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha huduma za simu, intaneti na data zinakuwa rafiki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spka, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kusimamia ushindani wa haki miongoni mwa Kampuni za simu ili kuchochea ubunifu na upatikanaji wa vifurushi vya gharama nafuu vinavyokidhi uwezo wa wananchi;

(ii) Kufanya mapitio ya gharama na tozo mbalimbali ili kuhakikisha utozaji unazingatia gharama halisi za huduma na kumlinda mlaji wa mwisho;

(iii) Kuhimiza matumizi ya miundombinu ya pamoja ili kupunguza gharama za uendeshaji;

(iv) Kuendelea na Ujenzi wa miundombinu ya Mawasiliano ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, minara ya mawasiliano maeneo ya vijijini na yasiyo na mvuto wa kibiashara pamoja na ujenzi wa vituo vya kuhifadhi *data*. Hatua hii inachangia kushuka kwa gharama za huduma, hususan intaneti ya faiba majumbani na maofisini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufuatilia mwenendo wa soko na kuchukua hatua stahiki za kisera na kikanuni ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za mawasiliano kwa gharama nafuu na sekta inaendelea kuchangia maendeleo ya uchumi wa kidijiti nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru nimepata majibu ya Serikali yamejieleza kwa kina, lakini tunapoongelea uchumi wa kidijiti *component* mojawapo kubwa ni intanenti ndio kufikia huo uchumi wa kidijiti. Kwa sasa hivi ukiangalia watumiaji wengi wa intanenti ambao inawasaidia kwenye biashara gharama imekuwa ni kubwa sana. Maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Wizara ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Vijana ni upi mkakati wa kuwafikia vijana kwenye makundi mbalimbali ambao wanatumia intanenti mfano vyuo vikuu, watumiaji wa kusafirisha abiria mtandaoni mfano *Uber* na *Bolt*, wauza nguo wadogowadogo ambao

wanafanya biashara zao kupitia *online* wakae nao katika hayo makundi waelezee uhalisia na makundi mengineyo namna ambavyo wanapata changamoto kubwa kupitia intanenti na watumiaji wengine?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali inaonaje ikae na taasisi binafsi ambazo zinatoa huduma hizi kwa ajili ya kuwaomba kupunguza gharama za *internet*, mfano Kampuni ya *Vodacom* na kampuni nyingine, kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kupunguza gharama za vifurushi ili ambao wanajiajiri kupitia sekta hii iweze kuwasaidia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wake wa kukaa na vijana kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Vijana, tumeupokea na tutakutana na vikundi mbalimbali vya vijana ili kujua mahitaji yao na changamoto zao wanazozipata katika upatikanaji wa *internet* katika shughuli zao. Kwa hiyo, tutawasiliana na wenzetu wa Wizara inayohusika na Maendeleo ya Vijana kwa ajili ya kulishughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukaa na taasisi binafsi kwa ajili ya kupunguza gharama za vifurushi, mwaka jana (2025) Serikali ilikaa na taasisi binafsi na tukapunguza bei za vifurushi vya *internet* na kwa sasa katika Afrika Mashariki ukiiondoa Rwanda, Tanzania ndiyo nchi yenye vifurushi nafuu kuliko nchi nyingine zote, zaidi ya Rwanda. Kwa hiyo, tutaendelea pia kukaa na hizi taasisi binafsi tuangalie namna gani tunavyoweza kuboresha zaidi gharama za vifurushi ili tuweze kufikia lengo la kuwa na Uchumi wa Kidijiti. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tumepokea ushauri wako na tutaufanyia kazi kwa kadiri inavyowezekana ili tufikie hilo lengo. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, gharama za vifurushi siyo muhimu sana kama makusanyo ya vifurushi hivi hayasimamiwi vizuri. Nchi ya jirani, *penetration* ya *mobile* iko chini ya Tanzania. Mapato ya *revenue* kwenye simu ni mengi zaidi ya Tanzania. Nchi za jirani zina *dividend* kwenye masuala ya simu, Tanzania hatuna. Kwa hiyo, *there is something wrong* katika makusanyo ya usimamizi wa *revenue* kwenye masuala ya simu. Serikali iwe na mkakati maalum wa *Digital Sovereignty* ya Tanzania. Dunia sasa inaendeshwa na mtandao. Ninamwomba sana Mheshimiwa, hana haja ya kujibu, walichukue wakalifanyie kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule.

Na. 20

**Kudhibiti Mikopo yenye Riba Kubwa**

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kudhibiti mikopo hatarishi yenye riba kubwa inayotolewa na baadhi ya Taasisi zisizo rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. Pita tu, pita tu. Mheshimiwa Waziri pita tu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nami nichukue wasaa huu kuweza kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Fedha. Pia nimwahidi pia kwamba nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote, nguvu zangu wote na akili zangu zote kulitumikia Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho basi niwashukuru pia Wananchi wa Jimbo langu la Kavuu kwa kura nyingi kwa Mama Samia na mimi mwenyewe. Baada ya hapo, basi ninarudi kwenye swali la

Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha nitajibu swali hili. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania na wadau wengine, imechukua hatua mbalimbali za udhibiti wa mikopo hatarishi yenye riba kubwa inayotolewa na baadhi ya taasisi zisizo rasmi. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuwa utoaji wa mikopo unapaswa kufanywa na watu wanaotoa huduma wenye leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)*, kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, pamoja na Sheria ya Huduma Ndogo za fedha ya mwaka 2018;

(b) Kuwatambua na kuchukua hatua za kiutawala dhidi ya watoa mikopo wasioidhinishwa. Katika kutekeleza hatua, programu zaidi ya 69 za mikopo ya kidigiti zilizobainika kutoa mikopo bila leseni zilisitishwa na programu 126 zilifungiwa;

(c) Pamoja na mwongozo maalum wa utoaji huduma za mikopo ya kidigiti ili kuhakikisha uwazi, uendeshaji wa kimaadili, utoaji wa taarifa kamili kuhusu gharama za mikopo, pamoja na ulinzi wa watumiaji wa huduma za kifedha; na

(d) Kuandaa rasimu ya kanuni za kusimamia mikopo ya kidigiti, ambazo zinatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2026/2027. Kanuni hizo zinalenga kuimarisha udhibiti wa wakopeshaji wa kidijiti nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Neema.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri kijana kabisa. Nina maswali ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kutambua umuhimu wa sekta ya fedha, Serikali imeandaa au kusimamia miongozo ipi ya kuhakikisha wananchi hususan wanawake na vijana wanapata elimu ya fedha ili kuchochea jitihada za ukuaji wa kiuchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali imechukua gani sasa kwa hao watu ambao wamejinufaisha sana kwa mikopo hii yenye riba kubwa? Waingereza wanasema *Predatory Loans,* lakini sisi tumeitafsiri kama 'Mikopo ya Kausha Damu'. Kwa maana kwa namna walivyofanya wameweza kabisa wenyewe kujinufaisha na kupunguza kabisa jitihada ya Serikali ya kuwakwamua wananchi kiuchumi hususan wanawake na vijana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Neema Peter. Kwanza ninakushukuru kwa maswali mawili ya nyongeza, maswali mazuri, lakini hii inamaanisha kwamba wanawake wa Dodoma hawakukosea kukuchagua. Kweli *Ph.D* kichwani ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa, niseme tu kwamba, Serikali imeendelea kuandaa na kusimamia miongozo na utekelezaji wa sekta ya fedha ili kuchochea uchumi wa wananchi, hasa vijana pamoja na wanawake. Serikali imekuja na mkakati maalum ambao unaitwa Programu ya Elimu ya fedha ya mwaka 2020/2021 – 2025/2026, ikiwa ni mpango maalum wa kutoa elimu kwa wananchi (wanawake wanaume na makundi mengine) ambayo inalenga zaidi kuwawezesha Watanzania kupata uelewa, maarifa na kuwajengea kujiamini katika kusimamia mapato na matumizi na kufanya maamuzi sahihi katika kutumia huduma rasmi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, ninyi mnaweza mkawa ni mashahidi ya kwamba kama Wizara ya Fedha tumekuwa kila mwaka tukiadhimisha maadhimisho ya Huduma ya Wiki ya Kifedha; ambapo tumeanza mwaka 2021 – 2026 (ambapo yamefanyika rasmi tarehe 21 mwezi huu, 2026). Mimi binafsi nikimwakilisha Waziri wa Fedha nimeenda kufungua rasmi maadhimisho hayo ambayo yamefanyikia nchini (Tanga) ili wananchi waweze kupata elimu ya kifedha. Kweli wananchi wa Tanga waliyapokea kwa hali ya juu, walikuwa ni wengi. Hii ni mikakati maalum ya Wizara ya Fedha kuhakikisha ya kwamba wananchi wanapata elimu ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, maadhimisho haya yameanza muda kidogo, tangu mwaka 2021. Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na mikoa mingine imeendelea kunufaika na elimu hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, zaidi ya mikoa 16 mpaka sasa hivi tumeweza kufikisha huduma hiyo ya fedha, kuwapa elimu ambapo zaidi ya wananchi 64,000 ikiwemo wanawake 40,000 na wanaume 24,000 wamepata elimu hii kuhusu elimu ya fedha. Vilevile, zaidi ya halmashauri 94 nazo tumepita kuhakikisha kwamba wanapata elimu ya fedha ili waweze kufanya maamuzi sahihi katika uwekezaji wao, katika uwekezaji na kuingia sasa kuwekeza kwenye mambo yetu ya kifedha ikiwemo uwekaji akiba, mikopo, uwekezaji, bima, Bima-amana, kodi, hati fungani na mengineyo mengi, kwa sababu sisi kama Wizara ya Fedha tumejipanga ipasavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, lililenga zaidi kwamba sasa sisi kama Wizara ya Fedha tumejipanga kwa namna gani kuhakikisha kwamba wale wanaokiuka taratibu zilizowekwa sasa wanaweka riba kubwa ili kujinufaisha wao.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, katika mkakati ambao tumesema kwamba tumeandaa rasimu ya kusimamia

mikopo ya kidijiti ambayo inatarajiwa kuanza mwaka 2026 na 2027, sisi kama Wizara ya Fedha tumejipanga kuhakikisha ya kwamba taasisi zote zinazotoa mikopo zinafuata taratibu zote. Yeyote anayekiuka tayari tumeshaanza msako huo kuhakikisha kwamba tunasitisha leseni na kufunga kabisa, kwa sababu anakiuka taratibu ambazo Serikali imeziweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nyongeza tu kwa niaba ya Waziri wa Fedha, tunaiagiza Benki Kuu ya Tanzania kuendelea kuongeza juhudi zaidi katika udhibiti wa mikopo hii, kuhakikisha kwamba wananchi hawa ambao sasa wanatuamini na Serikali yetu hii ya Awamu ya Sita wanapata mikopo ambayo sasa inawanufaisha na wala si ile wanayoiita 'Kausha Damu' na sisi tumejipanga kuhakikisha kwamba tuko pamoja kuwasaidia wananchi kwa sababu ndiyo wananchi wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwapongeze Wabunge wapya kwa maswali mazuri. Inaelekea elimu imewaingia vizuri sana kwenye semina na semina nyingi mtapewa zaidi. Vilevile, ninawapongeza na Mawaziri wapya; kwa kweli mmejibu vizuri sana leo, hongereni sana. Wengine niliwapa muda mwingi kwa sababu mlikuwa mnazungumza hotuba, ambayo ndiyo tutaijadili baadaye. Mambo muhimu sana mmeyasema ya maslahi makubwa sana ambayo Rais ameyafanya kwenye nchi yetu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Spika: Balozi wa *Norway* Nchini Tanzania, *Her Excellency Tone Tinnes*, *Ambassador of Norway in Tanzania*. Karibu. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Victor Mlunde, *Senior Advisor – Governance and Political Affairs*. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Zungu, wapigakura kutoka Jimbo la Ilala Jijini Dar es Salaam: Ndugu Zeenat Willimohamed - Katibu wa CCM Kata ya Kisutu; Ndugu Tousif

Mohamedali - Diwani Kata ya Kisutu; Ndugu Sayyada Komal - Diwani Viti Maalum; Ndugu Mohamedali Versi - Mwenyekiti Wazazi Kata ya Kisutu; Ndugu Komali Rizwan - Mwenyekiti wa UVCCM Kata ya Kisutu; na Ndugu Abidhussein Norbhaiuseli- Mjumbe Kamati ya Siasa ya Kata. *(Makofi)*

Hiyo ndiyo Ilala hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

**TAARIFA YA UCHAGUZI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kuwafahamisha kuwa, tarehe 5 Februari. 2026 siku ya Alhamisi kutakuwa na chaguzi mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge;

(ii) Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika *(Pan-Africa Parliament – PAP)*;

(iii) Uchaguzi wa Wajumbe wa Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC Parliamentary Forum)*;

(iv) Uchaguzi wa Wajumbe wa Umoja wa Mabunge Duniani *(Inter-Parliamentary Union – IPU)*; na

(v) Uchaguzi wa Wajumbe wa Jukwaa la Kibunge la Nchi za Maziwa Makuu *(Forum of Parliament of the Great Lakes Region)*.

Katibu wa Bunge ameshatoa tarifa rasmi ya uchaguzi huu ambayo inapatikana kwenye vishikwambi vyenu, ikieleza kwa kina nafasi zilizopo na sifa zinazotakiwa kwa wagombea. Hivyo, Wabunge wanaopenda kuchaguliwa katika nafasi hizo wachukue fomu za maombi kwa Katibu wa Bunge ambazo zinaanza kutolewa leo Jumanne tarehe 27 Januari, 2026 na mwisho kuzirejesha ni Jumanne tarehe 3 Februari 2026, saa 10 jioni.

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, kutakuwa na Bonanza litakalofanyika tarehe 31 Januari, 2026. Bonanza hili litafanyika katika Viwanja vya Shule ya Sekondari ya John Merlini iliyopo Miyuji Jijini Dodoma. Bonanza litahusisha michezo mbalimbali ya burudani ya mashindano ya timu za watani wa jadi, Simba na Yanga. Litaanza kwa maandamano yatakayoanzia Chuo cha Mipango Dodoma, saa 12 asubuhi.

Mgeni rasmi katika Bonanza hilo atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. Baada ya Bonanza, jioni kutakuwa na tafrija itakayoanza saa 12:30 jioni na kuendelea. Kaulimbiu yetu ya bonanza hili ni Umoja Wetu ni Nguvu Yetu. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* imeanza kutoa huduma za afya kwa umma wote na taasisi zote nchini kuanzia tarehe 26 Septemba, 2025. Kliniki za matibabu ziko katika ofisi za *BOT* nchi nzima (Ofisi Kuu Dodoma, Ofisi ya Dar es Salaam, Ofisi ya Zanzibar na matawi yake Arusha, Mbeya, Mtwara na Mwanza).

Kwa sasa wanapokea Bima ya *NHIF* na wanaendelea kujadiliana na kampuni nyingine za bima ili kuongeza wigo wa bima. Kliniki zote zina vifaa vya kisasa na madaktari wabobevu. Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla mnaombwa kufika katika kliniki hizi ili kupata huduma za matibabu kwenye matawi yote ya *BOT* nchini.

Ninaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa leo tarehe 27 Januari, 2026 saa 5.35 Asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi kitakachofanyika katika Ukumbi wa Spika *(Speaker's Lounge)* nyuma yangu hapa. Kikao hiki kitawajumuisha pia Makamu Wenyeviti wa Kamati zote. Waheshimiwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote mnaombwa kuhudhuria kikao hiki bila kukosa.

Taarifa nyingine ya Spika; chini ya Kanuni ya 41 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ya mwaka 2025, Waheshimiwa Wabunge,

ninapenda kutumia fursa hii kuwataarifu kuwa Ofisi yetu ya Bunge imepata Tuzo ya Mshindi wa Pili wa Taarifa Bora ya Hesabu za mwaka 2024 *(Second Winner for the Best Presented Financial Statement Award for the Year 2024)*. Tuzo hii imetolewa tarehe 4 Disemba, 2025 na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi *(The National Board of Accountancy and Auditors – NBAA)*, wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wahasibu na Wakaguzi uliofanyika Jijini Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge tuzo hii ya utayarishaji bora wa hesabu ambao sisi pia tumepata, hutolewa kila mwaka na *NBAA* kwa lengo la kuhamasisha Wizara, Idara, taasisi, mikoa, mashirika, na kampuni binafsi kuzingatia viwango vya Kimataifa katika uandaaji wa hesabu. Kwa maana hiyo, Mhimili wa Bunge umeonesha mfano bora wa kusimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi katika kusimamia mali za umma kwa kuzingatia pia Bunge letu lina jukumu la kusimamia taasisi nyingine za umma.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kulipongeza Bunge kwa kazi nzuri iliyofanyika na waandaaji bora wa hesabu, ninatoa rai kwa wahasibu na wakaguzi wote nchini kuendelea kufanya kazi zao kwa ufanisi kila mwaka wa fedha, ili kuondoa changamoto za matumizi mabaya ya fedha za umma.

Waheshimiwa Wabunge, nimalize sasa kwa kuonesha tuzo hii ya Bunge ambayo ninayo hapa mezani, inayoitwa Tuzo ya Mshindi wa Pili wa Taarifa Bora ya Hesabu za Mwaka. *(Makofi)*

Ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Katibu wa Bunge kwa mabadiliko makubwa ya usimamizi. Hatujawahi kupata shida ya ukaguzi toka Bunge lianze, hatujawahi kupata. Ofisi ya Bunge, Mhasibu Mkuu, Katibu na watendaji wa Bunge wamekuwa na uzalendo mkubwa sana kuangalia pesa na mali za umma katika Bunge. Hongera sana Katibu na timu yako. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya, sasa ninamwita Naibu Spika, mimi nina kikao kingine na wageni. Kwa hiyo, ninamwita Naibu Spika kuendelea na shughuli hizi mpaka hapo baadaye. *(Makofi)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Daniel S. Baran) Alikalia Kiti*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MWITA M. WAITARA:** *Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 79 na hoja yangu itajikita katika Kanuni ya 56.*

*Mheshimiwa Naibu Spika, wakati swali langu Namba Tisa linapata majibu ya Serikali Wizara ya Madini, wakati Naibu Waziri anatoa majibu alionesha kwamba mimi nipo nyuma ya wakati. Mimi nimeuliza kitu ambacho sasa hivi Kanuni ya CSR inaelekeza kwamba miradi ya maendeleo ya CSR itasimamiwa na kuendeshwa manunuzi na mgodi na siyo halmashauri, hiyo ni kanuni ambayo imetolewa mwaka 2023 na nina ushahidi kwamba tangu mwaka juzi, kama siyo mwaka jana Halmashauri ya Geita imegombana na mwekezaji wa mgodi mpaka leo fedha ile haijawahi kufanya kazi katika eneo lile, wanazo fedha kwenye akaunti.*

*Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, pale wametoa miradi, lakini wanakinzana namna ya kutekeleza miradi kwa sababu mgodi unataka utangaze tender kwa gharama kubwa kama nilivyoonesha hapa na kanuni inazuia hivyo, Mheshimiwa Joseph Musukuma na Mheshimiwa Waja watakuwa ni mashahidi katika jambo hili na eneo hili.*

*Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hiyo hiyo pia ukienda Halmashauri ya Kahama, Kahama wenyewe wamekubaliana Miradi ya CSR inaendeshwa manunuzi na halmashauri na wameokoa fedha nyingi. Kwa mfano, Tarime Vijijini, miradi ya mwaka jana tu kwa mtindo huo wa mkandarasi kutangaza tenda kwa kiwango ambacho nimeonesha, tumepoteza fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.25 kwa mkandarasi, tungetumia local fundi*

*tungepata miradi ya shilingi bilioni mbili, tumetumia mkandarasi zaidi ya shilingi bilioni tatu.*

*Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba mwongozo wako ninapomuuliza swali Mheshimiwa Waziri, ananiambia ni kabla ya kanuni, labda kama ana kanuni nyingine. Ninaomba niseme huu ni mgogoro ninajua upo kule kwetu, upo Geita, upo Kahama, kanuni hii tumetunga sisi na kama kuna mapungufu Bunge hili linao uwezo wa kubadilisha kwa namna bora zaidi, fedha nyingi ziende kwenye miradi ya maendeleo na ili watu waweze kunufaika. (Makofi)*

*Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mgodi wenyewe na wawekezaji jukumu lao mahsusi ni kutafuta dhahabu siyo kuendesha miradi ya maendeleo, kuchimba matundu ya vyoo, kujenga madarasa. Kwa hiyo kipaumbele chao siyo miradi ya maendeleo, kipaumbele chao ni utafutaji wa dhahabu katika eneo hilo. (Makofi)*

*Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako ikikupendeza, ahsante.* **[MANENO HAYA SIYO SEHEMU YA TAARIFA RASMI ZA BUNGE]**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Waitara, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 79 akiomba mwongozo wa Kiti kuhusu swali lake namba tisa ambalo limejibiwa leo asubuhi. Kwa kuwa swali limejibiwa, basi kiti kitafanya rejea kwenye *Hansard* halafu baadaye nitatoa mwongozo wa jambo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimkaribishe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuwasilisha hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa wakati wa kufungua rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mnamo Tarehe 14 Novemba, 2025, hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nitumie nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais, kwa ushindi wa kishindo alioupata katika uchaguzi mkuu kupitia Chama Cha Mapinduzi. Aidha, ninawapongeza tena Waheshimiwa Wabunge wote mlioshinda katika Majimbo yenu na wale walioshinda Viti Maalum pamoja na walioteuliwa kuwa Wabunge katika Bunge hili la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Spika, binafsi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika wa Bunge letu na ninakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliochaguliwa kuwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge,

akiwemo Mheshimiwa Anne Kilango Malecela - Mwenyekiti na Mheshimiwa Christina Mndeme - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Mheshimiwa Mashimba Ndaki - Mwenyekiti na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Deodatus Mwanyika - Mwenyekiti na Mheshimiwa Mariam Mzuzuri - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro - Mwenyekiti na Mheshimiwa Edwin Swalle - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga - Mwenyekiti na Mheshimiwa Paschal I. Chinyele - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Florent Kyombo - Mwenyekiti na Mheshimiwa Jafari Wambura - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Hawa Mchafu – Mwenyekiti na Mheshimiwa Regina Malima - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Jackson Kiswaga - Mwenyekiti na Mheshimiwa Pius Z. Yanda - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Maji na Mazingira.

Mheshimiwa Husna Sekiboko - Mwenyekiti na Mheshimiwa Cornel Magembe - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa Timotheo Mnzava - Mwenyekiti na Mheshimiwa Mary Masanja, Makamu Mwenyekiti Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo pia Mheshimiwa Dkt. Johannes L. Lukumay - Mwenyekiti na Mheshimiwa Zeyana Hamid - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Mheshimiwa Selemani Kakoso - Mwenyekiti na Mheshimiwa Abubakari Asenga - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Mheshimiwa Subira Mgalu - Mwenyekiti na Mheshimiwa Simon Songe - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Cecilia Paresso - Mwenyekiti na Mheshimiwa Mfaume Y. Zuberi - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Masanja Kadogosa - Mwenyekiti na Mheshimiwa Dougras Massaburi - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Mheshimiwa Devotha Minja - Mwenyekiti na Mheshimiwa Aeshi Khalfan - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Hesabu za Serikali. Mheshimiwa Ado Shaibu, Mwenyekiti na Mheshimiwa Abdallah Chikota - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuunda Baraza la Mawaziri katika Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha pili. Uteuzi wao ni ishara ya imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais, kwamba wanao uwezo wa kutekeleza yale yote tuliyowaahidi wananchi katika kipindi hiki. Kama Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, wito wangu kwenu tekelezeni wajibu wenu kwa kushirikiana kwa karibu sana na Waheshimiwa Wabunge katika kufanikisha utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali kwa lengo la kuleta ustawi na kubadilisha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyote mtakubaliana na mimi kuwa hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais hapa Bungeni, ilikuwa nzito inayoonesha umakini, umahiri na yenye kutoa mwelekeo na dira ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Kipindi cha Pili. Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ilitoa maelekezo na kubainisha changamoto pamoja na majukumu yanayopaswa kutekeleza katika kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais, imetuonesha bayana na kwa uwazi maeneo ambayo Serikali ya Awamu ya Sita itazingatia ili kufanikisha utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi waliotuchagua. Utekelezaji wa maelekezo haya kwa ufanisi ndicho kipimo tutakachopimwa nacho na wananchi waliotupatia ridhaa ya kuwawakilisha katika kipindi cha miaka mitano hii ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais, imegusa maeneo mbalimbali nasi Wabunge tunatakiwa

kushirikiana na wananchi na wadau wengine wa maendeleo kuyatekeleza. Kwa kutukumbusha maeneo ya jumla aliyoyazungumzia Mheshimiwa Rais, yalihusu Uchaguzi Mkuu, Muungano, uchumi na uwezeshaji wananchi, kukuza sekta binafsi, wanawake, huduma za kijamii, afya na elimu, sekta za uzalishaji yaani kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, madini, utalii na uwekezaji. Sekta wezeshi yaani nishati, ujenzi, uchukuzi, TEHAMA, mazingira, habari, utamaduni na michezo. Pia mambo ya nje, ulinzi, usalama, uwajibikaji na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji Serikalini ni miongoni mwa jambo ambalo limezungumzwa kwa kina kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais, tunapozungumzia utendaji Serikalini msisitizo ni uadilifu na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi waliotuchagua ili kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na rasilimali za nchi pamoja na kupata huduma wanazostahili. Serikali itawajibika na kuendelea na mageuzi ya sera zinazogusa moja kwa moja maslahi na ustawi wa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kusisitiza kuwa, Serikali haitavumilia watendaji au viongozi wanaotoa visingizio na wasiowajibika. Huluka ya utendaji wa kazi wa mazoea, ujanja ujanja na kutoa taarifa za michakato badala ya majawabu havitavumiliwa hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la marekebisho ya Katiba ambalo ni mojawapo ya ahadi ya Chama Cha Mapinduzi kupitia Ibara ya 47(2) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2025, Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa Serikali itafanyia kazi suala hili kwa kuanza kwanza na kuunda Tume Huru ya uchunguzi wa matukio ya uvunjifu wa amani yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu na kufuatiwa na kuunda Tume ya Usuluhishi na Maelewano na kuanzisha mazungumzo ya maridhiano na upatanishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imejipanga kikamilifu kutekeleza vipaumbele vyote vilivyoainishwa. Serikali imeainisha maeneo mbalimbali ya utekelezaji na kupanga mpangokazi wa utekelezaji

wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu na tayari utekelezaji wake umeshaanza kutekelezwa kwenye maeneo kadhaa. Hivi sasa Serikali kupitia Wizara za Kisekta imeanza kutoa taarifa kwa umma kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji na zilizokamilika zinazohusiana na ahadi za Mheshimiwa Rais za siku 100 baada ya kuunda Serikali ya Awamu ya Sita kwa kipindi cha pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru sana na kuwapongeza sana Watanzania wote kwa kuendelea kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa ambao ni tunu adhimu ya nchi yetu. Amani tuliyonayo ni matokeo ya kuheshimiana, kuzingatia misingi ya haki, wajibu na kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake kwa wajibu wa Katiba kama ambavyo umeelezewa kwenye Katiba, Sheria na Mila zetu. Ni muhimu tukaendelea kukumbushana kwamba, haki na wajibu ni pande mbili za sarafu moja, hakuna haki bila wajibu na hivyo basi ni wajibu wa kila Mtanzania kulinda amani yetu kwa vitendo na kuheshimu sheria, kuvumiliana, kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wa vyama vyote kutumia fursa hii adhimu kutoa michango yao itakayosaidia Serikali katika utekelezaji wa mambo mbalimbali yaliyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Pamoja na ukweli kwamba tayari utekelezaji wa mambo mbalimbali umeshaanza, wito wangu kwenu ni kuwa hotuba hii ichochee mjadala utakaoibua mawazo mapya na mikakati mipya ya kutuwezesha kubadilisha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba michango yenu itaheshimiwa, itathaminiwa na itafanyiwa kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena ninashukuru kwa fursa hii na ninaomba sasa kutoa hoja.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza kuchangia hoja hii na tayari nimeshapokea orodha hapa ya wachangiaji na kila atakayepewa nafasi atachangia kwa dakika 10, kwa hiyo naomba mtumie vizuri muda wa dakika 10 katika kutoa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nitaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Injinia Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa kwanza. Ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturejesha wote hapa pamoja tukaanza kipindi hiki cha mwaka wa 2026 niwatakie wote heri ya mwaka mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kushinda kwa kishindo uchaguzi wa Oktoba, 2025 na hasa nirudi ndani ya Jimbo langu Mheshimiwa Rais, nimpongeze sana kwa sababu alishinda kwa kishindo mno Jimboni kwangu, hii imetokana na miradi ya maendeleo aliyowaletea wananchi kipindi chake cha miaka minne pamoja na ahadi alizozitoa wakati anaomba kura alipofika Same. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, ninaomba uniruhusu nimwongelee Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kama kiongozi wa Taifa letu. Watanzania wote wafahamu kwamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ni Rais anayeongoza Taifa kubwa sana ndani ya Afrika ya Mashariki. Sitasema tu ninaomba nitoe takwimu kwa nini ninasema kwamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, anaongoza Taifa kubwa ndani ya Afrika ya Mashariki kuliko mataifa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye eneo la Nchi ya Tanzania ni *Square Kilometre* 947,303; eneo la nchi ya Kenya ni *square kilometre* 582,640; eneo la nchi ya Uganda ni *square kilometre* 241,550; eneo la nchi ya Burundi ni *square kilometre* 27,830; eneo la Rwanda ni *Square Kilometre* 26,338. Ukiangalia jumla ya eneo la nchi nne za Afrika Mashariki hizo nilizozitaja za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi ni *square kilometre* 878,364 ambazo ni chini ya eneo la nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ningependa Watanzania tuelewe kwamba Mheshimiwa Rais Samia anaongoza Taifa kubwa. Nisiishie hapo niende kwenye wingi wa watu *(population)*. Tanzania *population* yake ni zaidi ya milioni 71, nime-*google,* Kenya ni zaidi ya milioni 58, Uganda milioni 51, Rwanda milioni 14.7, Burundi milioni 14.5. Niseme ukweli Watanzania tujue kwamba Rais Samia anaongoza Taifa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uniruhusu nianze kuchangia hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, hapa Bungeni alipokuwa anazindua Bunge hili, tarehe 14 Novemba. Mimi naanza kuzungumzia upande wa huduma za jamii ipo ukurasa wa 17 wa kitabu cha hotuba ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Samia, alianza kuongoza Taifa letu tarehe 19 Machi, 2021. Alipoanza kuongoza Taifa hili, ndani ya jimbo ambalo mimi ni mwakilishi wa wananchi wale tulikuwa na kituo cha afya kimoja, Mheshimiwa Rais Samia kwa miaka yake minne aliweza kuongoza Serikali ikatujengea vituo vya afya vinne, vikiwemo Vituo vya Afya vya Vunta, Mtii, Myamba na Vuje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais anaingia madarakani nilikuwa na Kituo cha Afya cha Ndungu, ndugu zangu kilikuwa hakina hata mochwari, baada ya miezi miwili alipoingia madarakani, kitu cha kwanza alinijengea mochwari ya kuweza kuchukua miili sita kwa wakati mmoja. Kitendo hiki kiliwafurahisha sana wananchi wangu wa Jimbo la Same Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba niseme ukweli kipindi chake cha kwanza kwangu mimi upande wa jamii ya afya huduma ya afya ilikuwa ni nzuri sana, ninamwomba sasa tunavyokwenda kwa sababu anazungumza kwamba anakwenda kuendeleza sana huduma ya afya, ninakiri ameniletea magari ya wagonjwa matatu, lakini ninaomba tafadhali aendelee kunijengea vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Same Mashariki wamempongeza sana kwa hiki kitendo cha kujenga vituo vya afya vinne wakati wa kipindi chake cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye sekta ya ujenzi, kwanza kabla sijasema lolote, ninaomba niseme ukweli Tanzania inajengwa, barabara zinajengwa mno, tujaribu kusema ukweli. Unajua watu wengine wanasema kwa sababu hawajasafiri kwenda nchi zingine. Mtu anasema hajaenda Kenya, Uganda, hajafika Rwanda wala Burundi analalamika ooh! hatujengi, hapana. Serikali ninaomba niseme ukweli Mheshimiwa Rais Samia anajenga sana nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumze upande wa barabara, barabara zinajengwa watu wanaotoka Dar es Salaam, mimi ni mgeni pale Dar es Salaam, lakini nimefika Dar es Salaam ikabidi dereva wangu ashindwe kuendesha gari langu tukaomba dereva mzoefu wa Dar es Salaam, Dar es salaam imejengwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kitu ambacho sisi Wabunge ambao tumetoka kwenye majimbo tuseme ukweli, kwa nini Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amepewa kura zaidi ya 90% Jimboni kwangu, zaidi ya 97% Jimboni kwangu. Jimbo langu linalima tangawizi takribani zaidi ya 72%, lakini Jimbo lilikuwa halina barabara ya lami. Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani ni Rais wa kwanza, nimeanza kuzungumza hapa tangu mwaka 2000 kuomba Barabara ya Mkomazi - Kisiwani –

Same. Yeye alipoingia kipindi chake cha kwanza ndiye Rais aliyenipa Barabara ya lami ya Mkomazi – Kisiwani – Same, akawafurahisha wananchi sana, akawachanganya wananchi mno, siku ya kupiga kura tangu saa 11 walikwenda kwenye vituo kwa sababu ya kufurahia barabara ya lami aliyoijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme ukweli Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mimi kama Mbunge wa Same Mashariki alistahili kura 100% zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mkomazi – Kisiwani - Same inaanzia hapa Mkomazi ambako ni Korogwe Vijijini, inakuja Bendera inakwenda Kihurio, inagusa Kalemawe, inagusa Ndungu mpaka Kisiwani – Same, ni barabara kubwa ambayo inakwenda kuboresha uchumi wa wananchi wangu. Kweli utasema wananchi waache kumpa kura 100%? Haiwezekani! Wananchi wamefurahia sana miradi ya maendeleo na jinsi alivyowajali kwa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba Mheshimiwa Rais sasa, alipokuja kuwaomba wananchi kura alifurahi sana na alisema kwamba yule mkandarasi anajenga sasa ni *lot one* akaahidi wananchi wa Same Mashariki kwamba, atakapoingia madarakani mkandarasi wa *lot two* ataanza kazi. Ninamwomba Mheshimiwa Rais mkandarasi wa *lot two* aanze kazi ya ujenzi wa barabara *lot two. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* inatusaidia sana sisi Wabunge hasa Wabunge wa vijijini, ninasema kwa sababu mimi ni Mbunge wa Jimbo la Vijijini, wananchi wangu Tarafa mbili wanaishi milimani, muda umekwisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia muda wako umeisha.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya. Wanaishi milimani Tarafa mbili lakini, Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani alitoa pesa nyingi kwa *TARURA,* nikajengewa barabara saba mpya. Ninampongeza Mheshimiwa Rais na ninaomba kwa sababu sasa ameongeza pesa *TARURA* zile

barabara saba ziendelee tena kujengwa ili magari yaweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ambayo ni ya ukweli na wananchi wangu Same Mashariki walipo wanajua haya niliyozungumza ni ya ukweli, nisingeomba mtu ambaye siyo wa Same Mashariki aseme lolote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 14 Novemba, 2025 wakati anahutubia na kuzindua rasmi Bunge hili la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru sana mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema na kunipa nafasi nyingine ya kurejea katika Bunge hili kikiwa ni kipindi changu cha pili. Ninawashukuru wananchi wa Biharamulo kwa kuendelea kuweka imani yao kwangu na Chama Cha Mapinduzi hali kadhalika kwa kunipa fursa katika michakato ya ndani na hatimaye nikafanikiwa kurudi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia Wabunge wenzangu ninajua safari ilikuwa ndefu, lakini Mungu katujalia tupo hapa kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. Kwa hiyo, ninaamini katika kukaa kwetu kwenye Bunge hili la Kumi na Tatu tumebeba matarajio makubwa ya wananchi wa Tanzania sawa na hotuba ya Mheshimiwa Rais ilivyosema. Kwa hiyo, ninaamini tutashirikiana vizuri na Serikali kwenye kuyafanya haya maendeleo ambayo wananchi wametuamini kwamba tunaenda kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa na ushindi wa kihistoria alioupata. Maana sote ni mashahidi kwamba siasa ni mchezo wa hadharani siyo wa kujificha chumbani. Tuliona jinsi CCM tulivyokuwa tumejipanga kwa ajili ya uchaguzi huu tukitoa takwimu na mikutano inayojaa kila sehemu Rais alipokanyaga na wagombea wengi. Kwa hiyo, ushindi huu ni dhahiri ni ushindi ulioandaliwa kisayansi na chama hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, si ushindi ambao hata tunahitaji kwenda kujieleza sehemu. Kwa sababu *record* zilikuwa zinatolewa kila wakati tumo na kwenye *TV* kila alipokanyaga mvua inanyesha, jua linawaka watu wamejaa, lakini yote hii ilikuwa ni Watanzania kulipa matumaini makubwa ambayo yalifanyika katika kipindi chake cha kwanza cha miaka minne na miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo ililetwa kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, hilo lazima niliseme, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumpe pole pia kwa kadhia ambayo ilitokea baada ya tarehe 29, ninadhani wakati anahutubia Bunge hapa alisema yeye binafsi mambo haya yalimhuzunisha na akaahidi kuchukua hatua. Ninakuja kwenye kuchukua hatua, tumeona Mheshimiwa Rais amefanya juhudi kubwa kulirudisha hili Taifa likae pamoja tuweze kusonga mbele kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni Wawakilishi wa wananchi madhila haya yalitokea kwenye maeneo yetu, lakini siku Mheshimiwa Rais anahutubia Bunge aliahidi vijana wetu waliokumbwa na kadhia hii akaahidi kuwaachilia, akatoa ahadi ya msamaha aka-*refer* maandiko kutoka Luka 23:34, wote ni mashahidi vijana wale wako nje leo. Tunataka Mama huyu afanye nini zaidi ya upendo huo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliahidi kuunda Tume, tumeona Tume inazunguka huku na huku ikichukua maoni yote hiyo ni juhudi za Mheshimiwa Rais kurudisha hili Taifa pamoja, tumeona ameongea na Mabalozi wanaowakilisha nchi zao hapa na akaahidi baadhi ya vitu havitatokea kwa sababu Serikali

imejipanga kuendelea kushikamana, lakini ametoa ahadi ya kuendelea kutoa mkono wa ushirikiano na kuelekea kwenye maridhiano bila kuchoka. Kwa nini, ninayasema haya, hatuwezi kujenga hili Taifa kama baadhi ya watu wanasimama *the way* wanavyoona na wanaturudisha nyuma.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eng. Ezra, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge.

**TAARIFA**

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Mbunge pale anasema wale waliokuwa magereza wote wameachiwa, siyo taarifa sahihi kwa sababu mpaka sasa kuna watu wako magereza wengi tu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra, taarifa unaipokea?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei na ninaomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninayasema haya, Mheshimiwa Rais aliahidi mambo ya kufanya ndani ya siku 100 na alipotuhutubia hapa alitaja baadhi ya mambo yatakayofanyika ndani ya siku 100. Wote ni mashahidi suala la bima za afya kwa wote Wizara ya Afya imezindua na leo Halmashauri zote nchi hii zimeshatangaza kwamba watu waende wakaanze usajili kwa ajili ya bima za afya, lakini kipindi anatangaza humu alisema ni majaribio akaomba Wabunge tutoe ushirikiano kwa sababu ni majaribio na tutoe maoni pale ambapo tutaweza ili Serikali iweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kuna *package* ya shilingi 150,000 kwa watu sita, hii nilitaka kuomba kidogo Serikali isikilize kwa sababu *we are African families,* ukipiga familia nyingi huko vijijini kwa kweli kuwa na watu sita ukishaweka baba, ukaweka mama, watu sita wanazidi. Kwa hiyo, waone kama wanaweza

wakawa na *package extra* familia zenye watu nane, familia zenye watu 10 ili tuone jinsi ya kuwa-*accommodate* wote waweze kuingia hapo. Ninadhani kwa sababu ni majaribio hili watalichukua waweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine Mheshimiwa Rais ndani ya Bunge hili aliahidi wakati anahutubia Bunge kwamba kutakuwa ajira 7,000 za kada ya elimu kuajiri walimu, lakini kutakuwa na ajira 5,000 za kada ya afya. Leo nimesimama kama shahidi wote wanaelewa. Kwa mfano, jimboni kwangu juzi nimepokea ajira mpya 166, zikiwepo ajira za kada ya afya 110 na elimu zaidi ya ajira 40. Kwa nini, ninayasema haya? Ninayasema haya ili tujue kwamba pamoja na mambo haya yanayoendelea, lakini Serikali haijalala na mama yuko kazini anaendelea kutekeleza aliyoyaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine sisi Wabunge wa vijijini tuna habari ya *REA* watu wanahitaji umeme kila maeneo. Nyote ni mashahidi tumemwona juzi Waziri wa Nishati akisaini mikataba vitongoji 9,009, tayari wakandarasi wanaelekea *site* kwenda kufanya kazi. Kwangu pekee nina vitongoji 67 ambavyo vinakwenda kushughulikiwa na wakandarasi wanaelekea *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninayasema haya? Ninayasema haya ili Watanzania waelewe, Taifa hili na mama anapohangaika huduma hizi zipo zinakwenda kwa wananchi hawa tunaowawakilisha hapa. Kwa hiyo, tunachowaomba watupe ushirikiano tufanye kazi, tusonge mbele hili Taifa ni letu na hatuna nchi nyingine ya kuihudumia zaidi ya Nchi ya Tanzania. Huu ndiyo wito wangu ninaopenda kuutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mambo mengine ni ya kitaalam, mimi kitaaluma ni *Engineer*, niliona juzi kipindi mvua imenyesha *TRC* wakasema wanasitisha baadhi ya safari za Morogoro hapa ku-*anticipate* hali ya hewa, lakini anasimama mtu anaenda *photo shoot* ya ajabu ajabu tu! Hivi kweli tulipata *El-Nino* kubwa sana hapa mwaka juzi mpaka viwanda vyote vikasimama kila eneo likasimama, hakuna nguzo hata mmoja iliyoyumba, juzi Dar es Salaam mvua ya siku mbili ikayumbishe *SGR* kweli?

Unawaza anayeyafanya haya, anayafanya kwa nini na ana shida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kutoa wito kwa watanzania *this is our country we don't have another home rather than* Tanzania. Tumemaliza uchaguzi watupe ushirikiano sisi ndiyo wawakilishi wao ndani ya Bunge, lakini pia waipe ushirikiano Serikali pale tunapokuja hapa kuwawakilisha ili maendeleo yaliyoahidiwa na ambayo yameshaanza kufanyika sasa kwenye maeneo yetu yaweze ku-*flow* vizuri, hii ndiyo nia na kiu ya Watanzania walio wengi huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezunguka vijijini wananchi wanaelewa kazi iliyofanyika, mikutano yetu ilikuwa inajaa sana kwenye kampeni, maana yake wananchi wanayo matumaini makubwa sana na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, wana matumaini na Rais wao, wana matumaini na Madiwani waliowachagua, wana matumaini na Wabunge waliowachagua, tupate nafasi ya kufanya kazi, siasa zimekwisha, tukutane 2030 baada ya hapo tuanze kuulizana maswali mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo niliyotaka kuyachangia, nikisema kwamba hatuna nyumbani kwingine zaidi ya Tanzania, *let's stand for our country*, tu-*support* viongozi wetu, tu-*support* kwa ajili ya hawa watu tuliowachagua, hatimaye Serikali yetu iyatimize haya ambayo imeanza kuyatimiza. Ahadi ya siku 100 imeonekana, kwa hiyo, tunaamini na ahadi nyingine zilizoahidiwa kwenye Ilani na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais zinaenda kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Ezra kwa mchango mzuri.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo tena, Mwongozo, Mheshimiwa Ado.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili ni chombo nyeti sana ni lazima *facts* zake ziwe rasmi, Mheshimiwa aliyetoka kuchangia amesema watu wote ...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Umesimama kwa Kanuni ipi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge taja Kanuni uliyosimama nayo.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niendelee. Ninasema hoja mezani ni kwamba licha ya *progress* iliyosemwa kwamba watu wametoka, si sahihi kubaki kwenye *Hansard* kwamba ni watu wote. Tunaomba mwongozo pale ambapo *facts* zinakuwa tofauti inakuwaje?

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tunaposimama tutaje Kanuni za Bunge ndiyo maana tunazo Kanuni za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa Mheshimiwa Mbunge haukutaja Kanuni, lakini mwongozo wangu ni kwamba mchango wa Mheshimiwa Mbunge ulikuwa sahihi kama alivyotaja. Kwa hiyo, huu ndiyo mwongozo wa kiti.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya

Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wakati Mheshimiwa Rais anazindua Bunge letu kuna mambo alituongoza kama Taifa, nasi Bunge hili kama wawakilishi wa wananchi tunapaswa kwenda kwenye *line* yake ili Taifa letu lisonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wote tulikubaliana yaliyotokea siyo mazuri, lakini si sifa kuendelea kuzungumza kitu kibaya kitakachotugawa na Rais ameonesha nia ya kutatua kwa kuunda Tume na amesema bayana Tume ikileta majibu kama kuna taasisi kuna maeneo ilifanya makosa atachukua hatua ili kwa yale tuliyoyapitia iwe funzo katika chaguzi zinazoenda na katika kuendesha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alisisitiza Waziri Mkuu wetu, hakika umoja wetu wa kitaifa, dhamira ya Rais wetu, tukimuunga mkono tutaenda kuhakikisha Taifa letu linakimbia kwa maendeleo kwa sababu Taifa letu litakuwa moja. Niliyesimama hapa hii ni mara yangu ya pili kuijadili hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mara ya kwanza ilikuwa mwaka 2021 aliposimama hapa kulihutubia Taifa kuna mambo aliyasema atayafanya, leo Watanzania ni mashahidi ameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza alisema ataenda kuendeleza mazuri yaliyofanywa na watangulizi wake, leo tujiulize *SGR* iko wapi? Leo tujiulize Bwawa la Mwalimu Nyerere liko karibu 99%, ameendeleza kasi ya ujenzi wa miundombinu aliahidi alitekeleza. Vilevile, akasema atahakikisha wale ambao wako nje ya nchi wanakuja tushirikiane kujenga nchi yao, ametekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ni Rais ambaye anasema anatenda, nina uhakikia haya aliyoyasema wakati anahutubia Bunge hili yanaenda kutekelezwa kwa sababu kuna mambo aliyasema ameyafanya. Jukumu letu kama Watanzania kumpa ushirikiano ili tuendelee kuijenga Tanzania tunayoitaka. Hakuna mtu mwingine wa kutujengea Taifa hili isipokuwa sisi kwa kusimamia rasilimali zetu, kwa kutumia mikopo ya ndani na nje itumike vizuri ili tuiache Tanzania kwa vijana ambao zaidi ya 60%

kwenye hotuba yake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataja zaidi ya mara tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninataka nizungumze na vijana wa Taifa hili, mimi Ester Bulaya niliingia Bungeni hapa nikiwa Mbunge wa vijana, tuliona hotuba mbalimbali, tuliona kasi za maendeleo ya kutatua changamoto za vijana, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema vijana wa Taifa hili ndiyo wenye nchi yao, hivyo ni lazima kwenye asilimia mbalimbali za bajeti ya nchi hii wapewe kipaumbele. Akasema kwamba kwenye *program* mbalimbali katika Wizara mbalimbali vijana watapewa vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia ripoti hapa, unapozungumzia kuanzisha madirisha ya uwekezaji kwa ajili ya vijana unazungumzia kutengeneza mabilionea vijana watakaotengeneza ajira kwa vijana wenzao. Unapozungumzia kutenga bilioni 200 kwa ajili…

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**TAARIFA**

**MHE. SAASISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninataka tu kumpa taarifa dada yangu *senior* kwa mchango wake mzuri. Kuna maneno ameyaweka pale kwamba mnyonge, mnyongeni haki yake mpeni. Ninataka tu kumpa taarifa, kwamba mama huyu hajawahi kuwa mnyonge ni shupavu kweli kweli; na ninataka tu kumpa taarifa kwamba, kwa kuwa amefanya vizuri tumpe akiwa hivi maua yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninampongeza Mbunge kwa mchango mzuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake inaongeza mchango, lakini huu ni msemo wa kunogesha mambo ya msingi kama anavyoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia kutenga bilioni 200 kwa ajili ya vijana wajasiriamali unazungumza hawa Wamachinga wanaofanya biashara ndogondogo na wao waweze kusimama kiuchumi; nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? Unapozungumzia kutenga maeneo kwa ajili ya kuwajengea mazingira mazuri ya kufanya biashara unawagusa vijana wa nchi hii ambao wengi ndio wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika historia ya nchi yetu kwenye hotuba hii, Mheshimiwa Rais amesema kwamba anakwenda kuanzisha *campus* za vyuo vikuu kwenye kila mkoa. Amesema kwamba anakwenda kuongeza fedha za mikopo, ambapo wote tunajua kwamba kwenye bajeti ya mwaka jana fedha za mikopo peke yake ni bilioni 916. Haya yote yanawahusu vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema anakwenda kuendeleza *program* ya kujenga *VETA* kila wilaya. *VETA* zinawahusu vijana, vijana ndio watakaokuwa wajenzi wa nchi hii. Tumeona nchi zote zilivyofanikiwa kiuchumi kwa kujenga viwanda ambavyo vilikwenda kuwekeza kwenye vyuo vya kati; ambapo unakwenda kuwatengeneza mafundi mbalimbali watakaosambazwa kwenye viwanda mbalimbali kuijenga nchi yao. Hiyo yote unazungumzia vijana wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoweka mkakati wa kuhakikisha kwamba tunaendeleza *economic zone* kwa kujenga viwanda kutokana na malighafi zinazopatikana kwenye mikoa husika, wanufaika ni vijana. Vijana wa Taifa hili wamepata Amiri

Jeshi Mkuu anayewajali, anayewaandalia kesho yenu, hivyo changamkieni fursa. Sisi wawakilishi wao kwenye maeneo yetu tutahakikisha kwamba fedha za mikopo wanapata kweli vijana wa maskini, wafanyabiashara ndogondogo kweli ili neema hii aliyoiweka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, malengo haya ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunawakabidhi nchi yao vijana ili waweze kuijenga wenyewe inafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anawasilisha hoja amesema jambo la msingi sana, kwamba, Serikali ambayo yeye ni kiongozi humu Bungeni watendaji wazembe, watendaji waliozoea kufanya kazi kwa mazoea, sisi kwenye maeneo yetu tutamsaidia. Kwa sababu kumlea mtendaji mzembe ni kuipinga Ilani ya Chama Cha Mapinduzi isitekelezwe kwenye maeneo yetu ambayo msimamizi wake ni Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyekiti wetu aliyeaminiwa na Watanzania kuwaletea maendeleo. Sisi tutaisimamia kwa sababu tunajua ana dhamira, amejipanga; si tu kuleta maendeleo bali pia kuacha tabasamu kwa Watanzania; wamkumbuke kwa mema aliyoitendea haki Taifa hili, sisi tutamsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Amos Bulaya kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Edwin Enos Swale, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema ambaye ametujalia na kutuwezesha sisi sote kuwa humu ndani kufanya kazi ya kuwatumikia Watanzania na kuitumikia nchi yetu. Kipekee nitumie nafasi kumpongeza kwa dhati kabisa kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kura

nyingi za kishindo na wananchi wa nchi hii kuwa Rais wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika nimpongeze Makamu wa Rais Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, lakini pia nimpongeze Waziri Mkuu kwa kupata uteuzi na kuthibitishwa na Bunge letu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vivyo hivyo niwapongeze wengine wote waliopata nafasi mbalimbali za kuitumikia nchi yetu katika nyadhifa na nyanja mbalimbali ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wenzangu wa Jimbo la Korogwe Vijijini kwa kura nyingi za heshima na upendo walizonipa zilizonifanya nije kuwa mwakilishi wao humu ndani. Niwaahidi kwamba nitaifanya kazi yao kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. Tuendelee kuchapa kazi, tuendelee kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapochangia hotuba ya Mheshimiwa Rais leo, kwanza niseme ni hotuba bora, ni hotuba nzuri na ni hotuba ambayo imebeba maono makubwa ya Taifa letu. Kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba hii nzuri ambayo ameitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba hii nzuri, sisi wote tunajua yaliyotokea tarehe 29 Mheshimiwa Rais pia ameyasema kwenye hotuba yake. Niungane na Mheshimiwa Rais na Watanzania wengine wote kutoa pole kwa wote ambao kwa namna moja au nyingine tuliguswa na matukio ya tarehe 29. Nitoe pole kwa ambao wamepoteza ndugu zao na mali, lakini pia kwa taharuki na uvunjifu wa amani uliokuwepo kwenye nchi yetu. Pamoja na hayo tunamshukuru Mwenyezi Mungu kama Taifa tunaendelea kuvuka salama na hakika tutavuka salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ameainisha vitu vingi ambavyo Serikali ya awamu yake inakwenda kuvisimamia na kuvitekeleza ili kuongeza uchumi pamoja na kuendelea kuikuza nchi yetu. Nikisema niijadili yote

sitaweza. Hivyo, ninaomba nichukue jambo moja tu katika mambo yote ambayo Mheshimiwa Rais ameyasema kwenye hotuba yake; nami nitoe mchango wangu na kuendelea kuongeza nyama na kushauri ili tuendelee kuijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais amewaahidi Watanzania kwamba kwa miaka hii mitano inayokuja tunakwenda kukuza uchumi wa Taifa letu; na kwamba ukuaji wa uchumi utaongezeka kutoka asilimia 5.6 iliyopo sasa kwenda asilimia saba. Hali hii ikifanikiwa inakwenda kuukuza uchumi wetu kuendelea kuwa uchumi wa kati, lakini wa kiwango cha juu. Ni matumaini yangu kwamba kwa kasi na *speed* ya Mheshimiwa Rais jambo hili linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wabunge ni lazima tuweke mchango, kwamba tunafikaje kwenye uchumi huu wa juu. Yapo maeneo ambayo Mheshimiwa Rais ameainisha nina uhakika ni maeneo muhimu sana. Ukiangalia takwimu zetu zinazotokana na sensa tuliyoifanya mwaka 2022, ilionekana 77% ya wananchi wa Taifa letu ni vijana na katika hawa vijana 77% ni wananchi walio chini ya umri wa miaka 36 na katika hao vijana wa miaka 15 mpaka 36, ni 34% na katika hawa 21.7% wapo kwenye shughuli au kwenye ajira kwenye sekta isiyo rasmi. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, ni lazima kama Taifa tukasimame kuchochea sekta ambazo zitakwenda kuzalisha ajira kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya eneo hilo ni eneo la kwenye sekta ya kilimo. Katika nchi yetu asilimia kubwa ya Watanzania ni wakulima na Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu tuna ardhi kubwa sana inayofaa kwa ajili ya kilimo. Kwa takwimu za *FAO* za mwaka 1984 tuna eneo la hekta 44,000 zinazofaa kwa ajili ya kilimo. Hata hivyo, eneo linalotumika kwa ajili ya kilimo ni chini ya 35%. Moja ya sababu kubwa ni kwa sababu kilimo chetu kinategemea mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili malengo ya Mheshimiwa Rais ya kukuza kilimo, lakini kukuza uchumi yaweze kufanikiwa ni lazima tukaweke nguvu kubwa na mkazo mkubwa kwenye kuchochea

na kukuza kilimo cha umwagiliaji ili tuongeze ardhi inayotumiwa kwa ajili ya shughuli za kilimo. Tukifanya hivyo maana yake ni kwamba tunakwenda kutengeneza uhakika wa ajira kwa vijana wetu ili vijana wetu waendelee kutoa mchango wao kwenye eneo la uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine ambalo kama nchi na Mheshimiwa Rais ameligusa tunatakiwa tukalisimamie vizuri litusaidie kukuza uchumi wa nchi yetu kufika kwenye viwango ambavyo Mheshimiwa Rais amesema ni eneo la utalii. Mheshimiwa Rais anasema kwamba ana matarajio kwa miaka hii mitano sekta ya utalii itakua mpaka kufikia kuingiza watalii milioni nane kwa mwaka. Tunaweza kama Taifa kufika kwenye idadi hiyo ya watalii. Sekta hii ni muhimu sana kwa sababu 25% ya fedha za kigeni tunategemea kuipata kwenye sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia wapo wenzetu ambao wamefanya vizuri sana kwenye sekta ya utalii ambao hawana mazingira kama ya kwetu na hawana vivutio kama vya kwetu. Ukiangalia mfano wa eneo la Nchi ya Singapore; nchi ya Singapore ina ukubwa wa *square kilometre* 721.5, ukitaka kuilinganisha ni $^{1}/_{3}$ ya kisiwa chetu cha Zanzibar chenye *squire* kilometa 2,461. Kwa takwimu za mwaka 2024, Singapore imepokea watalii milioni 16.5 na fedha za utalii walizoingiza kutokana na utalii ni Singapore dola bilioni 22.4 sawa na trilioni 56.2 ya fedha za Kitanzania. Sisi bajeti yetu kwa mwaka huu tulivyotekeleza ni trilioni 56.4. Maana yake ni kwamba, mapato yanayotokana na utalii peke yake yangeweza kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanyaje tufike kwenye eneo hilo? Kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais, ni lazima tukaweke mkazo kwenye miundombinu. Tuweke mkazo kwenye miundombinu kwa sababu takwimu zinaonesha watalii wengi wanaokuja Tanzania kutoka nchi za Ulaya na nchi nyingine ni watu wazima ambao wanahitaji kwenda vizuri kwenye vivutio vyetu kutalii na kuondoka. Ni lazima tuweke mkazo kwenye miundombinu ili watalii wanapokuja wafurahie mazingira yetu waweze kurudi tena Tanzania na mambo yaendelee kuwa

mazuri. Vilevile ni lazima tuweke mkazo mkubwa kwenye eneo la malazi ili watalii wanapokuja wapate huduma nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, lipo eneo moja ambalo hatufanyi vizuri, ni kwenye sekta ya ukarimu. Ni lazima tukaboreshe vyuo vyetu na kama nchi tuwe na mfumo wa kuthibiti ubora kwenye vyuo vinavyotoa elimu kuhusiana na mambo ya utalii ili tupate *quality* ambayo inatakiwa na tuweze kufanya vizuri kwenye soko la utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ninalotaka kuchangia ambalo ninaliona lina mchango mkubwa wa kutufikisha kwenye maono na ndoto ya Mheshimiwa Rais ni sekta ya utamaduni, sanaa na michezo. Mheshimiwa Rais ametuahidi kwamba anakwenda kuongeza nguvu na kwenda kuiinua sekta ya michezo kwenye nchi yetu. Kipekee nimefurahi sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kututhamini na kutujali vijana. Ametuteulia viongozi vijana kwenye Wizara hii, amemteua Waziri kijana, amemteua Naibu Waziri kijana. Ninaamini kwamba, kwa *combination* yao wanaweza kufanya vizuri. Mheshimiwa Makonda amethubutu kwenye maeneo mengi; tunaamini hata kwenye hili anaweza kuthubutu na kwa ushirikiano na Naibu Waziri na wenzake Wizarani wakafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nchi hatujawekeza vya kutosha kwenye sekta ya michezo, hatujashawishi sekta binafsi kuwekeza vya kutosha kwenye sekta ya michezo. Sekta hii inazalisha ajira, inatoa burudani na kuleta utulivu na usalama kwenye nchi yetu. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, niiombe Serikali tukawekeze nguvu zaidi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumepata bahati ya kuwa wenyeji na wenzetu wa nchi jirani kwa ajili ya mashindano ya *AFCON* yanatarajiwa kufanyika mwakani. Hata hivyo, kiukweli tukiangalia mpaka sasa bado hatuoni amsha amsha za maandalizi ya *AFCON*. Ipo haja ya kufanya zaidi kwenye eneo hili. Niziombe pia Wizara nyingine, TAMISEMI upande wa barabara, ardhi upande wa upangaji, viwanda na biashara, wenzetu wa utalii wote kwa pamoja tuungane pamoja kutoa msukumo na

kuisaidia Wizara ya Michezo iweze kuandaa vizuri mashindano ya *AFCON*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho; mwanzoni wakati ninaanza niliungana na Mheshimiwa Rais kutoa pole kwa Watanzania kulingana na madhara ambayo tuliyapata tarehe 29. Ninatambua, ni hamu ya Watanzania lakini ni hamu ya Wabunge wa Bunge hili kwamba kama sehemu ya wawakilishi wa wananchi tupate nafasi ya kutosha ya kutoa mchango wetu na kujadili kwa kina jambo hili lililotokea tarehe 29 Oktoba. Hata hivyo, hamu hii ya kwetu imeshatanguliwa na busara na nia njema ya Mheshimiwa Rais kwa kuunda Tume ya Uchunguzi ambayo inafanya kazi ya kuchunguza matukio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua huko mtaani na huko nje yapo maoni mbalimbali kuhusu Tume hii. Pamoja na yaliyotukuta lakini ni ukweli kwamba nchi yetu haina obwe la uongozi, nchi yetu ina uongozi. Tunaye Rais ambaye kwa mujibu wa Katiba yetu na kwa mujibu wa sheria zetu ndiye mwenye jukumu la kutoa uongozi kwenye jambo hili na namna aliyoanza kutoa uongozi tumeona alivyolishughulikia jambo hili kwa kuunda tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, niwaombe Watanzania, ni wakati wa kutulia busara ituongoze tusubiri kazi nzuri inayofanywa na Tume na taarifa ya Tume ndiyo itupe mwelekeo wa kutoka kama Taifa tujue tunakwenda wapi katika kuendelea kuiponya nchi yetu na kuendelea kuijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba hii na ninaunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Timotheo Mnzava. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa

Rais. Awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kibali cha kuwa Mbunge wa Bunge lako la Kumi na Tatu. Pili, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kuridhia jina langu kuwa mgombea na hatimaye kuwa Mbunge wa Bunge hili la Kumi na Tatu. Ahadi yangu kwa Chama Cha Mapinduzi ni kuendelea kuwa mtii na kuheshimu misingi ya Chama changu Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nitumie pia nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Lupembe kwa Imani yao kubwa kwangu na kunirejesha kwa mara ya pili kwa kishindo ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninawaahidi nitaendelea kuwa sauti yao ndani na nje ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba hii ninaomba niweke rekodi sawa. Wakati akichangia Mheshimiwa *Engineer* Ezra wapo Wabunge wenzangu wachache nadhani hawakusoma hotuba ya Mheshimiwa Rais wamesema kuna jambo halikuwekwa sawa kuhusu msamaha wa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa baadhi ya vijana wa matukio ya Oktoba 29. Ninaomba warejee ukurasa wa nane wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais hakutoa msamaha kwa kila mhalifu, alitoa msamaha kama mama, kama mlezi, kama Amiri Jeshi Mkuu alisema, ninaomba kumnukuu; "Kwa wale ambao wanaonekana walifuata mkumbo na hawakudhamiria kufanya uhalifu wafutiwe makosa yao." Kwa hiyo kama kuna mhalifu, hakufutiwa makosa na Mheshimiwa Rais. Nilitaka niweke sawasawa rekodi hiyo kwa ajili ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Ukisoma kitabu hiki vizuri kwa umakini kuanzia *page* ya kwanza mpaka ya mwisho, kwa mtazamo wangu unabainisha sifa mahususi za kiongozi bora Dkt. Samia

Suluhu Hassan. Kama ambavyo Wabunge wa kwanza wameanza kusema, ukisoma hotuba hii utabaini Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mtu msikivu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilio cha Watanzania wengi kwamba kuwepo na mkakati wa kuwa na katiba mpya, Rais ameahidi kuandika katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kumekuwa na kilio cha kuwa na Wizara ya Vijana, Mama Samia ameunda Wizara ya Vijana na imeanza kufanya kazi vizuri sana. Ombi langu kwa wadau na wananchi wa Tanzania, ahadi hii ya kuwa na katiba mpya haitaweza kufikiwa kama tutaendelea na mtindo wa mwaka 2014 wa watu kususa, kukejeli na kutokuheshimiana. Ili kufikia lengo hili ni lazima tujenge umoja wa Taifa letu, tuwe na msingi, tuheshimiane ili tuweze kuandika katiba ambayo Mheshimiwa Rais ameahidi kwenda kuiandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ukisoma hotuba hii utabaini kwamba Rais wetu ana sifa ya kuahidi na kutenda. Kila alichoahidi kwenye Bunge ameanza kutekeleza. Yamesemwa na Wabunge wenzangu hapa, aliahidi kwenda kutoa ajira kwa Watanzania, ajira zaidi ya elfu kumi na mbili zimetangazwa na juzi Wabunge wameshuhudia kwenye halmashauri zetu, tumepokea watumishi wapya. Mimi kwangu zaidi ya wafanyakazi 83 wameripoti Njombe *DC*; ninamshukuru sana Mama Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, Rais wetu ni mvumilivu sana. Tunaye Rais ambaye yupo tayari kusikiliza kila maoni. Wapo watu kwenye mitandao wanaandika kejeli, wengine wapo nje ya nchi wanaandika mambo mbalimbali, lakini Rais wetu amekuwa mtu msikivu sana, amekuwa mvumilivu sana kusikiliza maoni na kuhakikisha kila mmoja apate nafasi ya kujenga nchi yake. Kwenye hotuba yake amesema, kwamba hata kule nyuma mwaka wa fedha 2025/2024 wapo watu walipuuza mkono wa Mheshimiwa Rais wa kuweka mshikamano kupitia *4R*; kwenye hotuba yake Mheshimiwa Rais amesema, pamoja na wadau kuutupa mkono wa kujenga umoja na maridhiano, Rais wetu ameutoa mkono tena wa maridhiano kwa ajili ya kujenga nchi yetu. Huu ni uvumilivu wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne; Rais wetu ni mlezi, na ni mtu mwenye huruma na upendo mkubwa sana kwa Watanzania. Ukisoma hotuba hii, utabaini kule nyuma kulikuwa na kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi juu ya kikokotoo. Rais wetu aliongeza mafao ya wafanyakazi ambao wanastaafu. Huyo ndio Rais, Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imesemwa kwenye hotuba, Rais wetu alipoona wako vijana ambao waliingia kwenye machafuko yale kwa mkumbo, kwa kushawishiwa, na kwa kutokujua, kwa sasabu ya huruma na upendo wake, akaamua kuwasamehe. Huyo ndio Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine; Rais wetu ni muumini wa Utawala wa Sheria, Demokrasia na Umoja wa Kitaifa. Nimemsikia rafiki yangu Mheshimiwa Ado Shaibu kabla hajawa Mbunge hapa akiwa kule nje akimsihi Mheshimiwa Rais aweke msingi mzuri wa uchaguzi ili haki itendeke kwa kila mtu na hatimaye Ado Shaibu ameshinda kwa upinzani yuko ndani ya Bunge. Huyo ndio Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wito wangu kwa Wabunge tuliopo humu ndani, tutumie nafasi hii kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumtie moyo afanye kazi, na tulinde nchi yetu kwa sababu Rais anampenda kila mmoja wetu ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninaomba niliseme pia mchana huu, Rais wetu ni mpole, lakini mwenye msimamo mkali. Kwenye hotuba aliyoitoa hapa alisema bayana kwamba linapokuja suala la kulinda maslahi ya Taifa, hakuna mbadala. Alisema wazi kwamba ni lazima tulinde utu, uhuru na misingi ya nchi yetu. Huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, ukisoma hotuba hii utabaini Rais wetu anatambua mchango wa kila jinsia kuchangia uchumi wa nchi yetu. Ndiyo maana utaona ndani ya Bunge lako idadi ya Wabunge wanawake imeongezeka. Hii ni kwamba

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anathamini mchango wa kila jinsia katika ujenzi wa nchi yetu. Leo Bunge limependeza, wakina mama wapo wengi na wanaume tunakwenda kujenga nchi yetu. Hongera sana Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho kwa mchana huu, ninaomba nitoe wito kuwa ziko siasa zinaendelea kwenye ukanda *(geopolitics)* na kuna watu ambao ni Watanzania wapo nje ya nchi wanaendesha siasa huko. Rais wetu ameshaweka msimamo kwamba linapokuja suala la maslahi ya Taifa, sisi kama Watanzania tusiwe na mbadala. Tutajenga msingi wa mahusiano, tutajenga msingi wa kushirikiana, lakini kamwe kwenye maslahi ya Taifa tusiyumbe wala kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, nitumie nafasi hii tena kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Lupembe, waendelee kuniunga mkono, waendelee kuniombea; na kipekee tarehe 29 walimpa kura za heshima kumlipa wema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi ya aliyopeleka ya maji, umeme, na barabara. Mheshimiwa Dkt. Samia alistahili kushinda 98% Jimbo la Lupembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, ahsante na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle kwa mchango wako. Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo alihutubia wakati akifungua Bunge tarehe 14 Novemba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, aliyetujalia leo kuwepo ndani ya Bunge lako Tukufu. Pia nikushukuru wewe kwa

kunipa nafasi ili niweze kuchangia hatuba ile adhimu ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuanza na jambo la msingi katika maisha ya Watanzania. Tutakubaliana sote afya ndiyo kitu cha msingi katika maisha ya mwanadamu. Wote tuliokuwa humu ndani na waliokuwa nje wanahitaji afya iliyo kamili na iliyokuwa madhubuti ili maisha yaweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linajidhihirisha katika kurasa za mwanzo za hotuba ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pale aliposema, ninaomba nimnukuu; "Tunajiandaa kuanza kwa majiribio ya Bima ya Afya kwa Wote, Serikali itakuja kwenu Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo ya namna ya kufanikisha majaribio haya, na niwaombe muunge mkono mapendekezo hayo ambayo yatakuwa mwanzo wa mageuzi katika upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wote nchini." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kutaka kuhakikisha Watanzania wanapata afya iliyokuwa bora. Nitakopa maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema kwamba, utekelezaji wa mambo mbalimbali tangu hotuba ya Mheshimiwa Rais ilipohutubiwa ndani ya Bunge hili, mpaka sasa tayari umeshaanza, na katika suala hili la bima ya afya tayari miongozo mbalimbali ya kuelekea huduma hiyo kwa Watanzania imeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa kitita tayari umeshakamilika, mwongozo wa kuwatambua wanufaika wote tayari, mwongozo wa malipo kwa rufaa na halikadhalika, mwongozo wa namna gani ya kugharamikia bima ya afya kwa Watanzania tayari imeshakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kufurahisha na jambo la kupendeza, tunafahamu tuna *TASAF* ambayo katika kanzidata yake inawatambua watu wenye kaya za kuhitaji kupatiwa huduma hii ambao ni 868,200 lakini kwa mujibu wa *NBS*

Watanzania wenye kaya maskini wanaohitaji huduma hii ni takribani 3,900,017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *TASAF* wanaendelea na zoezi la kuzitambua kaya hizi. Zoezi hilo la utambuzi likishakamilika, zoezi la majaribio lianze kwa zile kaya zilizotambuliwa awali na hatimaye Mheshimiwa Rais azindue rasmi bima ya afya kwa Watanzania. Mheshimiwa Rais alituambia hapa anataka kuleta tabasamu kwa Watanzania na dalili zimeanza kuonekana mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha jambo hilo la Bima ya Afya kwa Wote ambalo linaenda vizuri, kitu kinachonifurahisha kwa upande wa Wizara yetu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, ni dhahiri tunayo makazi ya wazee na makazi ya watoto ambao wote wameshatambuliwa katika Bima ya Afya kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakubaliana sote hapa Wabunge wote waliotangulia kusema, wamezungumza dhamira njema ya Mheshimiwa Rais juu ya vijana wa Taifa hili. Ninapenda kumnukuu Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ukurasa wa 13 alisem: "Kwa kuwa zaidi ya 60% ya watu wa nchi hii ni vijana, tutaweka kipaumbele kwenye sera na programu zitakazopanua fursa za kiuchumi, kutengeneza kazi na ajira, kuongeza wigo hifadhi za jamii na kuwajengea vijana kesho iliyo bora." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni pana, halionekani katika Wizara moja ambayo Mheshimiwa Rais alisema, ataiunda na tayari ameshaiunda. Nikianza tu katika hii Wizara, tayari Wizara imeshundwa, lakini tumemwona Mheshimiwa Waziri Ndugu yangu Nanauka jinsi alivyokuwa akizunguka nchi hii ya Tanzania kuhakikisha anaanzisha majukwaa ya programu za vijana kwa nchi nzima. Jukwaa hilo tayari limeshazinduliwa tarehe 10 Januari, 2026. Hii ni kudhihirisha kwamba kazi tayari imeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema kwa vijana wa Kitanzania, Mheshimiwa Rais kwa nia na dhamira njema kama

alivyozungumza kwenye hotuba yake, kutakuwa na shilingi bilioni 200 kwa ajili ya vijana na wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri katika Wizara hii ya Vijana tayari mchakato wa kuzipeleka shilingi bilioni nane umeshaanza kwa ajili ya vijana wetu, na nitaomba mnisikilize vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi shilingi bilioni nane ni kwenye Wizara moja tu ya vijana mbali na ile 10% za katika halmashauri yetu. Kwa hiyo, kama unakosa mkopo ama fursa kama kijana katika halmashauri zetu, utageukia katika Wizara ya Vijana katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kwenyewe kuna fursa ya shilingi bilioni nane kwa ajili ya mkopo kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kusema, fursa ya vijana haiko katika Wizara hii tu, ipo pia katika Wizara ya Madini, Wizara ya Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mawasiliano. Kwa hiyo, vijana wa Taifa la Tanzania kaeni mkao wa kula, kazi kwenu. Mheshimiwa Rais alichokihutubia hapa ameshaanza kukitekeleza karibia katika kila Wizara ambayo kwa namna moja ama nyingine inahusiana na vijana na fedha hizi tayari zimeshakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuelekea kwenye upande wa maendeleo ya jamii. Leo hapa ninataka tu kuonyesha dola ambazo Mheshimiwa Rais amezitawanya sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, niwaombe sana vijana na wanawake muweze kuangalia fursa hizi. Tuzitumie simu zetu, hizi simu janja kwa manufaa kabisa kwa sababu Serikali imetawanya fedha kila mahali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaenda kwenye upande wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto; na kwenyewe huko mambo ni mazuri. Fedha kwa ajili ya wawezeshaji na wajasiriamali wadogo wadogo nikimaanisha bajaji, bodaboda, wasusi, washonaji, Mama Lishe na Baba Lishe na kwenyewe kuna fursa, ambapo Wizara yetu ya Wanawake na

Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum tayari zimeshakwenda shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya makundi haya niliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwaambie, fedha hizi ama jukumu hili wamekabidhiwa *NMB* kwa riba ya asilimia saba tu. Kwa hiyo, niwaombe sana vijana popote mlipo, wakinamama popote mlipo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akiwajali vijana na watoto wa Taifa hili bila kuwasahau wakinamama. Kwa hiyo, fursa ni hiyo, asilimia ni ndogo tu. Achaneni na mikopo ya kausha damu, achaneni na mikopo ya nguo mkononi. Tayari shilingi bilioni 10 ziko *NMB* kwa riba ya asilimia saba tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuizungumzia hotuba ya Mheshimiwa Rais na mambo makubwa na mazuri aliyoanza kuyafanya katika jamii yetu ya Kitannzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuendelea kukushukuru, kwa upande wa wenzetu wafanyakazi, sote tulimshuhudia Mheshimiwa Rais akitangaza kima cha chini cha shilingi 350,000 kwa Watanzania. Vilevile, Mheshimiwa Rais hakuwaacha tu wale ambao wako kwenye sekta rasmi, akaenda hata kwa wale waliokuwa katika sekta binafsi na kwenyewe pia ametangaza kima cha chini kulingana na sekta, na amesisitiza kwamba hilo jambo lianze haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaona ni jinsi gani Rais huyu ambaye amekuwa akisema na akitenda. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri aliyoanza kuifanya na inayoendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, na pia ninapenda kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Pwani kwa kunipa heshima hii ya kuwawakilisha tena ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawaambia tunaendelea pale tulipoishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mchafu.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwakumbushe kuwa hairuhusiwi kupita katikati ya mchangiaji na Kiti.

Tunaendelea na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetujalia siha njema na kuweza kutufikisha katika viunga hivi kwa ajili ya kujadili hatma ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, maana yake yeye ndiye pekee anayeweza kuamua jambo liwe ama lisiwe, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais pia kwa hotuba yake njema, yenye matumaini, hotuba yake ambayo imetuleta Watanzania pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maisha yetu sisi binadamu, hakuna binadamu yeyote mwenye uwezo wa kujiamulia jambo lake mwenyewe na likawa bila ya Mwenyezi Mungu kuamua na kuweza kulifanikisha likawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninasema hivi? Ninatamani tu kujaribu kurudi nyuma, kuangalia mazingira aliyoingilia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mimi binafsi sikuwahi kukaa ama nikalala usingizi nikaota ndoto kwamba ipo siku Rais wa nchi hii Mwenyezi Mungu atamchukua halafu msaidizi wake atakuja kushika hiyo nafasi. Sikuwahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu, yeye alipanga na kila binadamu ndani ya dunia hii

Mwenyezi Mungu amemwandalia riziki yake na siyo vinginevyo. Kwa hiyo, nasi leo Wabunge tuliopo hapa ndani, siyo kwa uwezo wetu, bali ni kwa kudra za Mwenyezi Mungu, ndiye aliyeweza kutusababisha tuweze kuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote yaliyotokea, Waswahili wanasema, "yaliyopita si ndwele, tugange yajayo." Hata hivyo, ninaomba nisisitize, sisi sote ni Watanzania na hakuna Mtanzania mwingine mwenye Tanzania yake nyingine. Wote tuna Tanzania yetu moja tu, hii tuliyonayo leo hapa. Kwa hiyo, yeyote kwa dhamira yake njema ama kwa dhamira yake nyingine yoyote itakayoweza kumsukuma kujaribu ama kuthubutu kuweza kupoteza na kuiondoa amani tuliyonayo hapa, haitaishia tu kwa sisi tulioko hapa, bali itatembea kizazi na kizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao watangulizi wetu, viongozi wetu na Watanganyika wenzetu ambao walipigania uhuru wa Taifa hili, wakaamua kutuweka Watanganyika na kwenda kwenye Muungano, tukaungana na Zanzibar leo tunaitwa Tanzania, siyo kwa sababu hawakuyaona hayo yote, lakini walitamani watusogeze karibu ili tuweze kuwa Taifa lenye upendo, amani na mshikamano na hatimaye tuweze kujisimamia sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe Watanzania wenzangu, hii lulu tuliyonayo siyo kitu cha kubeza wala siyo kitu cha kutikisa na kwenda kujaribu. Waswahili wanasema, "sumu haijaribiwi kwa kuonja." Tumejionea sisi wenyewe yaliyotokea, wapo walioathirika hata ambao walikuwa hawahusiki na hayo mambo, lakini tumeenda kuangamiza watu wasiokuwa na hatia kwa tamaa zetu, ama mambo yetu ambayo tunayatamani kwenye maisha yetu ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba lulu tuliyonayo, nirudie, ni heshima kwetu, ni pendo kubwa la Mwenyezi Mungu alilotujalia tuweze kuwa nalo Tanzania na siyo mahali pengine popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Rais ana maono ambayo Watanzania wenzetu pamoja na mimi pia ninayo hayo hayo, ya kutoka kwenye uchumi wa chini na kuja kwenye uchumi wetu wa kati. Vilevile, kwenye Taifa letu, zaidi ya Watanzania 65% ni wakulima na mapato yetu kwenye maeneo mengi tunategemea kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliona kwamba ili yote haya aweze kuyatimiza jambo la kwanza ni kuwasaidia wananchi wetu na Watanzania wenzetu walioko huko chini vijijini tuanze kuboresha miundombinu bora ya elimu kwa Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna kipindi ambacho shule zimejengwa kuanzia awali mpaka sekondari na vyuo kama kipindi cha Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata hivyo, haijaishia kujengwa majengo yakatelekezwa, Mama huyu kajenga majengo, na pia katupatia na watumishi wakasaidie kuinua kiwango cha elimu kwa Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hajaishia hapo tu, elimu ya juu kwa maana ya vyuo vikuu, yeye kaamua kushuka mpaka vyuo vya kati. Leo tunavyozungumza, bajeti ya mwaka 2025/2026 tumepitisha zaidi ya shilingi bilioni saba kwa ajili ya vyuo vya kati ili watoto wetu na vijana wetu waende wakapate ujuzi na waweze kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni matamanio ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Watanzania kuimarisha sekta ya elimu ili Taifa letu liweze kuwa na Watanzania walioelimika, waweze kusimamia na kujiendesha wenyewe ndani ya Taifa lao katika miradi yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Naibu Waziri wa Uchukuzi wakati anajibu hapo, ametuambia tuna upungufu wa wataalamu kama marubani, lakini hiki ndicho Mheshimiwa Rais alichokiona kwamba tupeleke mikopo, tupeleke fedha, tuongeze wataalamu wetu, tusisubiri wataalamu kutoka nje. Tufundishe sisi wenyewe kwenye vyuo vyetu na hatimaye tuweze kuwapa

Watanzania wenzetu ajira kwenye taasisi zetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, nimesema sisi Watanzania zaidi ya 65% ni wakulima. Mheshimiwa Rais baada ya kuingia madarakani ndani huku na wakulima wote nchi nzima tulikuwa na kilio cha mbolea. Mama huyu baada ya kuingia madarakani, leo Mbunge anayetoka jimbo lolote lenye wakulima, nani analalamika suala la mbolea leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea inapatikana kwenye maeneo yetu kwa wakati tena kwa gharama nafuu kwa ruzuku ya Serikali aliyoiweka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mama huyu kwa namna moja ama nyingine ni Rais ambaye hatakuja kutokea katika maisha yetu ndani ya Taifa letu. Ametutoa mbali sana mpaka hapa leo tulipo, tuna kila sababu ya kumwombea Mwenyezi Mungu amjalie hekima na busara, uvumilivu, lakini aendelee kuwa na utumishi huo huo uliotukuka ili Watanzania waweze kunufaika na uwepo wake ndani ya Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri mambo machache. Maswali yameulizwa hapa na Waheshimiwa Wabunge, ninaomba katika nia na dhamira hiyo hiyo njema kwa ajili ya kukuza uchumi wetu niseme, kumekuwa na migogoro mingi ndani ya nchi yetu isiyomalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu tukuombe, migogoro isiyomalizika inayopoteza muda na gharama nyingi Watanzania wanatumia kwenda kutafuta suluhu ya migogoro hii tuombe Taasisi na Wizara zinazohusika ikiwemo Wizara ya Mifugo, Wizara ya Maliasili, Wizara ya Kilimo, na TAMISEMI, twendeni mkaunganishe hizo Wizara, tatueni migogoro ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka iliyopita tuliunda Tume ya Mawaziri Nane ambayo mpaka leo taarifa yake bado.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuomba Tume ya Mawaziri Nane watoe hatma ya migogoro kwenye maeneo mbalimbali nchini, ili wananchi wetu waondokane na migogoro ya wakulima na wafugaji pamoja na hifadhi na waweze kutumia ardhi ile kwa kuweza kuzalisha na hatimaye kuweza kupata tija kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninatamani kulisema, tunatamani pia na ni matamanio ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwenye hotuba yake pia ametuambia. Tunatamani kutoka kwenye kilimo sasa cha kusubiri mvua ya Mwenyezi Mungu kwenda kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hiyo dhamira njema, tunaomba iambatane na uwepo wa mbegu zilizo bora pamoja na viuatilifu, lakini ambavyo vitapatikana kwa gharama nafuu ili tuweze kutimiza ndoto ya Mheshimiwa Rais ya kufika uchumi wetu wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Taifa tumeendelea, ndani ya Taifa letu mazao yetu mengi tunayauza kama nafaka. Niombe Wizara ya Viwanda sasa ione namna bora ya kuhakikisha tunawekeza kwenye ujenzi wa viwanda ile tusiyauze mazao yetu kama nafaka na hatimaye tuyachakate na tuweze kuuza bidhaa ambayo imechakatwa ili kupata tija ndani ya Taifa letu, lakini na kukuza uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa muda wako, Mwenyezi Mungu akubariki sana. Ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti, ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga na tutamalizia na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo aliitoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba ulinzi wa Taifa letu na ulinzi wa kila Mtanzania umeendelea kusimamiwa na hatimaye kuendelea kuleta umoja wa Kitaifa ambao tumekuwa tukiendelea kushuhudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninapenda kumpongeza Mheshimwia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya, kuzunguka maeneo mbalimbali kuendelea kuhamasisha na kusemea kuhusu umuhimu wa Taifa letu kulinda amani na mshikamano wa Kitaifa ni jambo kubwa sana ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelifanya na lina tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninapenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Makete ikiwa ni mara ya kwanza nasimama kwenye Bunge la Kumi na Tatu kwa kunirudisha tena kuendelea kuwa Mbunge wa Jimbo la Makete. Niwahakikishie kwamba, nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wa dhati kabisa na kuhakikisha kwamba majira yatakapofika wawe hawana nafasi ya kwenda kwingine zaidi ya kumchagua Mheshimiwa Festo Sanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Comrade* wa *ANC* anaitwa Walter Sisulu ambaye alifariki, anasisitiza mambo matatu katika uongozi. Jambo mojawapo analolizungumza ni suala la *Integrity*, *Vision*, na *Resilience*. Haya mambo matatu kati ya huyu mwanasiasa mashuhuri wa Afrika Kusini ni moja ya mambo ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akiyafanya kwenye Taifa letu; *Integrity*, *Resilience,* na *Vision* ya Taifa letu linakoelekea ni jambo ambalo kwa Mheshimiwa Rais limekuwa ni maono, yamekuwa ni malengo na misimamo yake kuhakikisha Taifa lake pendwa la Tanzania linasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Rais amezungumza mambo mengi kwenye hotuba yake, lakini Watanzania tunapozungumza nao lazima tuweze kuwakumbusha Taifa hili katika sekta yoyote ya ukuaji wa Taifa kimaendeleo kuna maeneo matatu lazima yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, lazima wafahamu Taifa letu lilikuwa halina *access* ya mambo mengi, hakuna *stage* ilikuwepo, lakini baadaye tukapata *the access stage* ya mambo tofauti tofauti, lakini sasa hivi the *quality of the service*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati nchi yetu upatikanaji wa elimu ulikuwa haupo katika wingi ambao sasa tunao. Tukaja tukapata hatua ambayo nchi yetu imefikia hatua upatikanaji wa elimu na *infrastructure* za sekta za afya, umeme na nini imekuwa ni kwa kiwango kikubwa hususan kupitia Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suhulu Hassan tumeshuhudia ukuaji wa sekta mbalimbali kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kwenye ombwe ambalo tulikuwa nalo la kukosa kabisa hizo huduma ambapo mtu alikuwa akipata shida ya kiafya kuwaza kuhusu zahanati alikuwa anaona kilometa nyingi sana, lakini leo akiwaza shida ya zahanati anafikiria kilometa tano, sita anapata huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Taifa letu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais tumefikia kwenye *stage* ya *quality of the service* (ubora wa huduma unaotolewa kwenye maeneo mbalimbali). Hili niendelee kuiomba Serikali yetu, msimamo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, msimamo wa Mheshimiwa Rais kwa Watumishi wa Umma kuendelea kusimamia maono ya Mheshimiwa Rais katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna vituo vya afya, elimu, barabara, na usambazaji wa umeme maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Rais anasisitiza kwenye usimamizi bora wa huduma kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa kuona maeneo mbalimbali yakishuka na huu umekuwa ni msimamo wa Serikali kuhakikisha kwamba, maeneo haya huduma inaboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kuangalia kwenye maeneo mbalimbali Mheshimiwa Rais kuonyesha kwamba huduma zinaenda kupatikana zinalingana na mahitaji ya Watanzania, Mheshimiwa Rais ameenda kufanya baadhi ya *reform* katika kuhakikisha kwamba anawasaidia Watanzania kupata maendeleo yao. Mfano wa *reforms* ambazo amezifanya ni *reforms* ambazo anazifanya kupitia *TRA* kupitia mpango unaitwa MKUBI (Mpango wa Kuboresha Biashara kwa Watanzania).

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilio kikubwa sana cha Watanzania ukusanyaji wa kodi kwa mazingira ambayo ni tatanishi, lakini Mheshimiwa Rais amekuwa akiweka msimamo hata kwenye hotuba yake kwamba ataboresha mazingira hayo na tumeshuhudia akiboresha mazingira ya ukusanyaji wa kodi kwa Watanzania na ikiwemo pia ule msimamo wa Serikali ambao ulitoa ya kwamba *chain* ya Watumishi wa Serikali kumfuata mfanyabiashara lazima ikatwe ili mfanyabiashara apate kazi ya kufanya biashara na kuihudumia Serikali yake katika mazingira salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuiomba Serikali, mlundikano wa Watumishi wa Serikali kwenda kumfuata mfanyabiashara wa *OSHA*, *TRA*, *Service Levy* na watu wengine, mwendelee kuukata huu mnyororo hadi ifikie Mtanzania awe na uwezo wa kulipa kodi moja ambayo *distribution* yake inaenda mbali, atumie muda mwingi kuwahudumia Watanzania na kufanya biashara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeona ongezeko la ajira, tumeona kabisa Mheshimiwa Rais akiboresha mitaala ya elimu hii yote ni kwa ajili ya ku-*accommodate*. Kubwa zaidi ni namna ambavyo Mheshimiwa Rais amechukua namna ya kuboresha kwenye sekta ya vijana. Vijana kama eneo ambalo ni mtambuka

zaidi ya 60% kwenye hotuba ya Rais anazungumza, Mheshimiwa Rais amechukua taratibu za makusudi kabisa kuboresha mazingira ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya eneo lake ni kuunda Wizara ya Vijana ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Nanauka amekuwa akiihudumia na tumeona akifanya jitihada zake kwenye sekta ya vijana. Hili vijana wa Tanzania ni lazima wafahamu, Rais anafanya haya yote makusudi ni kusaidia vijana hawa. Nusu au robo tatu ya Bunge hili tumejaa vijana ukienda nje huko walioteuliwa kwenye nafasi mbalimbali za Ukurugenzi ni vijana, lakini zaidi angalia wizara ambalimbali zinavyojipambanua kuhakikisha kwamba zinawa-*support* vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wa Taifa la Tanzania, sisi ambao ni vijana wenzao tunawaomba lazima waiunge Serikali mkono kwa sababu mazingira mazuri yanatengenezwa kuhakikisha wao wanaenda kuisaidia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Wizara ya Madini, juzi Waziri alikuwa anazungunguza kwamba wameenda kuzuia sasa *material* ambazo zinapatikana nje zenye thamani ya zaidi ya trilioni moja ziuzwe na Watanzania kama sehemu ya kulinda *local content* ambazo ni kuwasaidia vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Wizara ya Mifugo sasa hivi wana *project* kuhusu vizimba. Hii yote ni katika ku-*support* vijana lakini zaidi ukienda vijana wa Vyuo Vikuuu wamekuwa wakiangaika na maeneo ya kufanyia *field* Serikali imetoa mwongozo kwamba vijana wote ambao wanamaliza vyuo Vikuu au wako Vyuo Vikuu wanatakiwa kufanya *field* inatakiwa waelekee kwenye maeneo ambapo ni ofisi za Serikali na wapate kufanya *field* kwa bure kuliko mihangaiko waliyokuwa wanaifanya. Hii yote ni jitihada za Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba anaunga mkono na kuwasaidia vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Wizara ya Viwanda chini ya dada yangu Mheshimiwa Judith Kapinga tayari kuna uelekeo

wa Kongani ya Viwanda kwenye kila wilaya. Hii yote ni kwa ajili ya ku-*support* vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa vijana wa Tanzania jukumu letu ni moja kumwombea Rais, kuiunga mkono Serikali, kuhakikisha haya yote yanatimizwa. Duniani haipo Serikali inayogawa fedha mtaani kwa wananchi wake ila inatengeneza mazingira rahisi kwa vijana kuweza kufanya kazi na hiki ndicho ambacho Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakifanya na anakitendea haki kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niendelee kuwasisitiza na kuwaomba vijana wa Taifa letu, sisi ndiyo Tanzania ya sasa na ndiyo Tanzania ya kesho lazima tujue kusimamia misingi na kulinda amani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais analifanya ambalo Watanzania lazima wafahamu kwa muda mrefu *in a record* pato la Taifa kwenye mchango wa sekta ya madini ilikuwa ni 10%, lakini toka mwaka 2025 hadi tunavyozungumza leo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mchango wa sekta ya madini umeenda kwenye *GDP* karibia 12% kwenye mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa sana katika nchi yetu. Katika *records* tumeingia chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Tanzania ilikuwa haiwezi kuwa na *gold reserve,* lakini *this time around* Tanzania ina *gold reserve* ya zaidi ya tani 17 na kuingia kwenye *records* ya kuwa ni moja kati ya mataifa 10 bora Afrika yenye *gold reserve* nyingi, na sisi tuko kwenye nafasi ya sita na sasa tunaelekea kwenye nafasi ya tano kuwa na *gold reserve*. Unapokuwa na *gold reserve* maana yake uchumi wako ni imara hata kunapotokea *crisis* unakuwa umeisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maono ya Rais hafanyi kwa ajili ya familia yake anafanya kwa ajili ya Taifa la Tanzania, anafanya kwa ajili ya vijana wa Tanzania, anafanya kwa ajili ya

kuhakikisha kwamba nchi yetu inazidi kukua *stage* kubwa zaidi ya kiuchumi kwenye mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi kwamba kwa sisi wananchi wa Makete, lakini kwa vijana wengine ambao sisi wengine tumekuwa tukiwasemea tutaendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. Tuendelee kuomba taasisi mbalimbali, sekta mbalimbali na wadau mbalimbali, wadau kutokea kwenye sekta za dini, lakini kwenye *civil society* waendelee kuiunga Serikali hii mkono kwa sababu hatuna Serikali nyingine mama, Serikali mama ni Tanzania ambayo sisi kama vijana tunatamani iendelee kuwa bora na Mheshimiwa Rais amekuwa akiitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kuiomba Serikali tunavyoelekea kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais ni muhimu sana Waheshimiwa Mawaziri tusijikite zaidi kuongeza miradi mingine mipya, lakini tujikite pia kuboresha na kukamilisha miradi ambayo imesalia. Mathalani, kwa upande wa Makete tuna barabara kipande cha kutoka Makete kuelekea Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambapo kumekuwa na changamoto ya barabara kutokukamilika ningetamani Serikali isimamie maeneo hayo yakamilike kabla hatujaanzisha *project* nyingine, kwa sababu kuanzisha *project* nyingine mzigo utakuwa ni mkubwa na hizi nyingine zitakuwa bado hazijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuombe Mawaziri, lakini na mipango ya Serikali ambayo inakusudia kwenda mbele, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwanza hii miradi inakamilika ili kuwasaidia Watanzania kwamba hii miradi iweze kufanya kazi, ikiwemo mojawapo sisi wana Makete tumeshapokea zaidi ya vitongoji 68 vinaenda kupata umeme, lakini katika kuhakikisha kwamba ajira zinapatikana; tumepokea watumishi wapya zaidi ya 101 kuhakikisha wanaenda kuunga mkono kwenye utendaji kazi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni jitihada za wazi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba nchi

yetu ya Tanzania inaendelea kuimarika katika utoaji wa huduma na katika kuhakikisha maendeleo yanasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua muda umeisha, lakini ninawaomba watumishi wa Serikali ambao wanamkwamisha Mheshimiwa Rais, hawamkwamishi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wanakikwamisha Chama Cha Mapinduzi na wanaikwamisha Serikali. Nasi kama Wabunge hatutokuwa tayari kwa watumishi waovu na wazembe kukaa nao, sisi tutaendelea kuwafunua na tutaendelea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. FESTO R. SANGA:** …kuwaonyesha kwamba hawa ni matatizo ili kuhakikisha kwamba Serikali yetu inakuwa salama na Rais anatimiza azma yake kwamba Tanzania inakuwa ni sehemu salama ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia siku ya leo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Tumalizie na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kutupa uhai na pia kutufanya kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikushukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuwa leo ni mara ya kwanza kusimama katika Bunge hili la Kumi na Tatu, kwa kufanya jina langu litokee kwenye uchaguzi na ninawashukuru sana wananchi wa Jang'ombe wapiga kura wenzangu, wananchi wenzangu wa Jang'ombe kunirejesha sana na nilisema kwamba hiki kiti ni kiti cha mzungu

wa nne, na mzungu wa nne siku zote huwa anarudi pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa hii nafasi, nami nitachangia kama walivyochangia wengi. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ukurasa wa 14 alielezea malengo ya kiuchumi, ambapo alisema "Tunataka kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka 5.6% mpaka kufikia 7%. Akasema, malengo kwa nini uchumi huu ukue hivyo kwa kasi hii? Rais ana hamu sana ya kuhudumia watu katika nchi hii na yeye ndio maono yake, anasema "Ukuaji huu utawezesha Serikali kuboresha huduma za kijamii."

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukitazama kuanzia ukurasa wa 15, 16 huko mpaka kwenda mbele zimetajwa huduma za kijamii ambazo Rais amekusudia kuboresha. Ataboresha huduma za elimu, maji na maeneo tofauti tofauti ambapo yapo yametajwa katika hotuba yake hii yale maono yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi, Mheshimiwa Rais alisema kati ya mikakati itakayofanyiwa kazi ni kuweka zaidi kwenye sekta zinazoajiri watu wengi, kuwekeza zaidi kwenye sekta zinazoajiri watu wengi na miongoni mwa sekta hizo akasema ni kilimo, utalii, viwanda, ujenzi, na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais maono yake ni kwamba awekeze kwenye hizi sekta, kilimo kinaajiri zaidi ya watu 63% ya Watanzania, kwa maana hiyo uwekezaji katika kilimo unaweza ukatupatia tija zaidi na uchumi ukakua kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliposema utalii, kwanza tumshukuru yeye mwenyewe Mheshimiwa Rais kwa kufanya *Royal Tour*. Leo tumepata zawadi tofauti tofauti katika nchi yetu kutokana na utalii na hili litaongeza namba ya watalii. Tunalishukuru Shirika la *Air Tanzania* na lizidi kufanya mipango mizuri zaidi ya kutoka nje ili ile Tanzania yenyewe ionekane, lakini pia hata kila wanaoshiriki kushawishi watu wakaja wakaijua

Tanzania yetu na wakaja tunawashukuru sana kwa kufanya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alisema sekta ya viwanda, ukuaji wa sekta ya viwanda pia ameusema Mheshimiwa Rais. Pia ukuaji wa Sekta ya Ujenzi na Madini. Sasa nami hapa nitoe rai, sekta hizi zinakuwa vizuri endapo tutakuwa tunawekeza katika *skills* vinginevyo kama kwenye *skills* itakuwa bado tupo chini hizi sekta kukua kwake zitakuwa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Maendeleo ya 2050 inasema hivyo na imetaja kuwekeza huko katika sekta hizi. Kwa mfano, nikichukulia kwenye viwanda kama hatutokuwa na watu wenye *skills* ina maana kwamba hivi viwanda, huu uchumi utakapokuwa utakuwa hauwezi kukua ukarudi kwa wananchi kwa sababu bado itakuwa unafanywa na wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye ujenzi, tunajenga *Standard Gauge Railway* na vitu vingine na ujenzi wa vitu vingine ambavyo tunavijenga. Kama sisi wenyewe tutakuwa tuna *skills* za kutosha na hiki ndiyo kiwe kipaumbele, kwa sababu utakapowekeza *skills* ndipo tutapata kile ambacho Mheshimiwa Rais alisema kwamba, "Tutawekeza kwenye sekta zinazoajiri watu wengi," na Mheshimiwa Rais alimalizia katika ukurasa huu wa 14 alisema, "Mwelekeo wetu ni kukua kwa pamoja kwa uchumi unaogusa maisha ya mtu mmoja mmoja *(micro economy)* na uchumi jumla *(macro economy)*."

Mheshimiwa Naibu Spika, ili hivi vitu vikue uwekezaji wake unahitaji yale mambo yarudi kwa watu. Yale mambo yakiwa yanarudi kwa watu, uwezeshaji wa kiuchumi umefanyika umerudi kwa watu hapa tutakuwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kitu kimoja, tumelenga uchumi wa 5.6 kwenda kasi ya 7% ni lazima tujaribu kuambatanisha na viashiria vingine vya kiuchumi navyo viweze kukua kama viashiria vingine havitokua navyo, pia vinaweza vikaja vikafanya mdororo katika ukuaji wa kasi hii ambayo labda pengine Mheshimiwa Rais ndiyo aliyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimalizie na neno moja ambalo Mheshimiwa Rais alilisema na sote tunalikumbuka, Mheshimiwa Rais alisema haya yote aliyoyasema hapa kwamba wale atakaowateua kuwa Mawaziri, nao pia sasa wafunge mkanda kwa maana yake hayuko pekee yake. Hapa tupo katika Bunge, Waheshimiwa Mawaziri wakati ule bado hamjala kiapo, lakini Mheshimiwa Rais alisema tufunge mkanda, sote kwa pamoja ili tuweze kufikia malengo haya ambayo yanalenga kuifanya Tanzania yetu ing'are."

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja nipende kulizungumza, uwekezaji kwa vijana. Mheshimiwa Rais ameunda mpaka Wizara ya Vijana na sisi ilikuwa tunasema hapa Bungeni kwamba vijana, vijana, vijana, leo imeundwa Wizara *investment* kwa vijana ni kitu kimoja kizuri sana na tumeona *investment* zimetajwa zaidi ya shilingi bilioni 200 zitakuwepo kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vijana watumie hii fursa. Vijana wetu sasa waachane na mambo ambayo hayana maana, kwa sababu nchi iko tayari kuwahudumia ili tupate kujenga nchi yetu, hii ni nchi ya kwetu sote siyo nchi ya mtu mmoja, utakapoiharibu huiharibu nchi ya fulani, tunaiharibu nchi yetu, na itakapotengenezwa, tunakuwa tunatengeneza nchi yetu na maslahi yatakuja kwetu sisi na vizazi vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *investment* kwenye vijana, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuunda Wizara na kuweka hiyo *investment* kwa vijana jambo maalumu litakuwa linashughulikiwa na vijana katika Wizara pekee yake. Mwanzo Wizara hii ilikuwa iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa kuna vitu vingi Ajira, Walemavu, Uwezeshaji sasa hivi iko pekee yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna fursa kubwa sana kwa vijana na humu Wabunge vijana wapo, kwa hiyo, wao Wabunge vijana ndiyo watatoa tafsiri ya mahitaji vijana wenzao humu ndani ya Bunge hili, ili wale vijana nao washughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kupata hii nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan King, kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana kwa waliopata nafasi ya kuchangia mchana huu, lakini tutaendelea na uchangiaji jioni ambapo tutaanza na Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa, Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mheshimiwa Ngayiwa Benjamin Lukubha, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, na Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, nimetangaza machache ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.59 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hotuba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi Rasmi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala. Tunaanza na Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa

atafuatiwa na Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, na Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela ajiandae.

**MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Spika, wewe Naibu Spika, pamoja na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania kwa kuaminiwa na kwa kazi kubwa na nzuri ambayo mnaendelea kuifanya katika kututumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue fursa hii kuwashukuru sana, vijana kutoka mkoa wa Kaskazini Pemba na pia Kamati ya Utekelezaji ya UVCCM Taifa kwa kunichagua, pia, Kamati Kuu kupitia Mwenyekiti wetu wa CCM ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kunithibitisha kuwa Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwaahidi vijana, nitaendelea kuwa msemaji wao, daraja lao na Serikali, lakini kuhakikisha changamoto zao tunazifikisha na zinapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma *Surah Ar-Rahman, Aya 55:60* inasema: "*Hal jaza ul ihsan illal ihsan.*" Je, kuna malipo ya wema kwa mtu anayekutendea mema zaidi ya wewe kumtendea mema. Ukisoma Zaburi 136:1 inasema, "Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema kwa maana Fadhili zake ni za milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa niaba ya vijana, kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anayoifanya kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu, na kwa kasi kubwa ya miradi ya maendeleo katika Taifa letu. Leo sisi ni mashuhuda, hakuna kijiji, hakuna kata, na hakuna wilaya utakayoenda usikute miradi iliyoachwa kama alama na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iwe kwenye elimu, iwe kwenye afya, iwe kwenye maji, iwe kwenye miundombinu ya umeme, barabara, mawasiliano, Uchumi wa Buluu, utalii, kila sekta kama hujakuta alama ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, basi wewe utakuwa hujaizunguka Tanzania na hujatembelea vijiji kuona hayo maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwanadiplomasia na nimekuwa nikifuatilia hotuba za viongozi mbalimbali ndani ya Afrika na hata nje ya Afrika. Ninataka niwathibitishie Wabunge kwamba hotuba ambayo ameiwasilisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025 ni kati ya hotuba bora kabisa kuwahi kutokea ndani ya Bara la Afrika. Mheshimiwa Rais ana mapenzi makubwa sana na Watanzania. Mheshimiwa Rais kupitia hotuba ile ameonesha uzalendo na utu wa kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama kijana ninapata faraja kwa sababu hii inaonesha kwamba Mheshimiwa Rais anatambua kwamba 76% ya Watanzania iko chini ya umri wa miaka 36 ambao ni vijana. Kupitia hotuba ile Mheshimiwa Rais ameonesha mahaba na mapenzi makubwa sana kwa vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hotuba ile, kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu, Mheshimiwa Rais ameunda Wizara ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais inayohusika na Maendeleo ya Vijana. Kwa kweli leo tunaye Waziri wa Vijana Mheshimiwa Joel Nanauka, ninaomba nimpe maua yake, anafanya kazi kubwa na kazi nzuri sana kuwatumikia vijana wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Mheshimiwa Rais ameenda mbali kusema kwamba ataweka washauri chini ya Ofisi ya Rais watakaoshughulikia maendeleo ya vijana. Ninataka niseme jambo moja, katika maeneo ambayo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais yamenigusa sana moyo wangu ni pale Mheshimiwa Rais alipoonesha kwamba anataka uwajibikaji, na

uadilifu Serikalini. Anatamani kuona watendaji wetu wakiwa na nidhamu wakiwajibika na wakiwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hotuba ile, Mheshimiwa Rais amesema: "Ninawaelekeza Mawaziri hadi Maafisa Tarafa wawe karibu na wananchi waende kusikiliza na kutatua kero za wananchi," na watakaposhindwa kufanya hivyo, yeye atachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inanikumbusha kauli ya Baba wa Taifa mwaka 1961 pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema yafuatayo: *"Those of you who have received this privilege, therefore have the duty to repay sacrifices which others have made."* Ninyi ambao mmebahatika kupata fursa hii, mna jukumu la kuhakikisha mnawajibika ili kujitoa kwa wale ambao wamejinyima ili ninyi leo muwe hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwaambie viongozi na watendaji wenzangu, Watanzania tupo 60,000,000, lakini leo wewe umepata heshima ya kuwa Waziri, leo umepata heshima ya kuwa Mkuu wa Mkoa, leo umepata heshima ya kuwa Mkuu wa Wilaya, leo umepata heshima ya kuwa Mkurugenzi, Afisa Tarafa, au Mtendaji Kata, ninataka utambue dhamana ambayo umepewa, una wajibu wa kuhakikisha unarudisha fadhila kwa wale ambao wamejinyima ili wewe uwe hapo kwenye hiyo nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kupitia mabaraza ya kazi anayoyaendesha, ametoa mwelekeo wa namna Serikali itakavyojipambanua. Amesema siku ya leo hapa, watumishi wote wanaofanya kazi kwa mazoea, watumishi wote ambao hawatimizi wajibu wao, na watumishi wote ambao badala ya kuwa suluhu ya kutatua migogoro, wao ndio wanakuwa sehemu ya kuongoza migogoro. Hawa watumishi hawatavumiliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kwenda mbali zaidi na kutaka tu-*review* sheria zetu ili wale ambao wanadhani wakiharibu sehemu moja wana uwezo wa kupelekwa sehemu nyingine hao waweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Hao watu ndio wanaotia doa Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa na nzuri sana, lakini baadhi ya watumishi, baadhi ya viongozi wasioitakia mema nchi yetu, wasiokuwa na utayari wa kulitumikia Taifa letu, ndio wanaomhujumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri ambao mmepewa dhamana, tunawaamini na hatuna mashaka na ninyi. Nendeni mkawasimamie watumishi ili waweze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge ambaye ninawakilisha kundi la vijana, ninatambua ya kwamba changamoto kubwa ya vijana ni ajira, lakini ninataka niwaambie vijana wanaonisikiliza huko mitaani, hakuna nchi duniani ambayo imemaliza tatizo la ajira. Maendeleo ni hatua, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipambanua leo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kupitia hotuba yake kwamba atahakikisha kunakuwa na kongani za viwanda kwenye kila wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia viwanda hivi, vijana watapata ajira, Serikali itakusanya mapato, na nchi yetu itapiga hatua kimaendeleo. Mheshimiwa Rais ameahidi kutoa shilingi 200,000,000,000 kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake. Mitaji hii itaenda kuwakwamua vijana kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Rais ameahidi ujuzi kuhakikisha kwamba, kwa sasa tuna *VETA* 64 kwenye wilaya 64. Ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kila wilaya kwenye wilaya 139 nchini kutakuwa na Vyuo vya *VETA* na vijana

watafungamanishwa na miradi ya kimkakati ili waweze kupata ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameahidi kutakuwa na kampasi kila mkoa ili tunapokuwa na Vyuo Vikuu kwenye mikoa hii, vijana wetu waweze kupata elimu na ujuzi, lakini kuweza kuchagiza uchumi kwenye mikoa husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaomba nihitimishe kwa nukuu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema haya yafuatayo: "Kwa wanangu vijana wa Taifa la Tanzania, nchi hii imejengwa kwenye misingi ya amani na utulivu wa kisiasa; sisi wazazi wenu tungeshawishika kuyafanya mliyoyafanya wakati huu nchi hii isingekuwa na neema na maendeleo mnayoyaona hii leo. Hivyo, ninawasihi wanangu vijana, nchi hii ni yenu, kwa shida zozote zile zinazowakabili, msikubali hata siku moja kushawishiwa kuichoma nchi yenu wenyewe. Msikubali kukata tawi la mti ambalo mmeukalia. Msikubali kabisa. Ninyi ndio walimu na wajenzi wa Taifa hili, ninawasihi vijana, kamwe msiwe wabomoaji wa Taifa lenu." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zainab kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngayiwa Benjamin Lukubha, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

**MHE. KAKULU B. KAKULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyotangulia wenzangu, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa salama, tukikutana tena kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; moja, kwa ajili ya kuyachakata na kuyachambua maoni ya Mheshimiwa Rais ili tukayatafsiri kwa usahihi mbele ya Watanzania waliotuchagua na kuwaaminisha kwamba bado kuna nafasi kubwa ya kuijenga nchi yetu nzuri iitwayo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nikupongeze wewe na Mheshimiwa Spika pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuaminiwa katika nafasi mlizoaminiwa kuhudumia nchi yetu. Sambamba, pongezi hizi ziende kwa Mawaziri wetu walioteuliwa kuhudumia katika Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza pia Wabunge wenzangu waliochaguliwa kuhudumu katika Bunge hili. Nitoe shukrani zangu za dhati kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Mbagala walionichagua kwa kura nyingi kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Ahadi yangu kwao ni kuwahudumia kwa uaminifu kwa uzalendo na kwa utii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajielekeza kwa uchache katika maeneo machache. Kwanza katika kutafsiri maoni ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa kupitia hotuba yake kwa Bunge lako Tukufu. Mheshimiwa Rais alichora mchoro wa uhakika katika maono yake kuhusu sekta ya viwanda na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo hayo, kuonesha kwamba viwanda vyetu ambavyo tunakusudia kuvijenga kupitia kongani zitakazofunguliwa katika kila wilaya na katika kila halmashauri zetu, na namna zitavyoenda kufungamanishwa na sekta yetu ya viwanda ambaye ndiye mlishaji mkubwa sana wa viwanda vyetu na sekta yetu ya usindikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kilimo chetu bado kinategemea sana kilimo cha mkono na kilimo cha kujikimu. Maono ya Mheshimiwa Rais ni kwenda kukitafsiri na kukipa nyongeza na kukiongezea uwezo kilimo chetu ili kiweze kuhudumia viwanda vyetu kwa uhakika, kituhakikishie usalama wa chakula pamoja na kutupatia mapato kupitia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza, sekta yetu ya kilimo kwa sasa inachangia pato letu kwa Taifa angalau kwa 26.3%. Lengo ni kuifanya ichangie zaidi kwa sababu ndiyo sekta inayoajiri watu wengi. Mabadiliko kidogo katika sekta hii angalau ikiwa

katika asilimia nane mpaka 10% ina uwezo wa kupunguza umaskini kwa zaidi ya nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukiunganisha sekta yetu ya viwanda na sekta yetu ya kilimo kwa kuzingatia maono ya Mheshimiwa Rais aliyotupa kupitia hotuba yake, tuna uwezo wa kutoa ajira za kutosha kwa vijana wetu ambao ndio tunakusudia kuwahudumia kwa kweli, kwa sababu ndio wanaounda sehemu kubwa ya nchi yetu kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nichukue nafasi hii kuwaonesha vijana wa nchi hii kwamba bado kuna nafasi ya kuihudumia nchi hii kwa kuitunza na kwa kuitumikia kwa uzalendo. Kilimo chetu pekee tukikifanya vizuri, zile kongani zetu za viwanda katika wilaya zetu 139 na halmashauri zetu 184 tuna uwezo wa kuzalisha ajira za kutosha ambazo zitapunguza presha kubwa iliyopo katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais, tunaenda kufungua Kongani ya Viwanda ya Kwala. Kongani ya Viwanda ya Kwala peke yake itazalisha ajira zaidi ya 600,000. Kongani ya Buzwagi pekee inaenda kuzalisha zaidi ya ajira 300,000. Kongani ya Bagamoyo inakuja, hebu jaribu kufikiria tutakapofungua kongani katika wilaya zote 139, hali ya ajira na mfumuko wa ajira kwa ajili ya vijana itakuwa ya namna gani? Yote haya, kwa vyovyote vile wanufaika wakubwa ni vijana wenzetu ambao ndio tunakusudia wapate ajira za kutosha katika kongani hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwa *speed* ya Mheshimiwa Rais katika kipindi cha miaka mitano ijayo, matarajio yetu tunakusudia kuyaona mabadiliko makubwa kupitia kongani hizi ambazo zitafunganishwa na sekta yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa wasaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Rais kupitia Baraza alililoliteua likiongozwa na Waziri Mkuu, ni kumsaidia Mheshimiwa Rais kuitafsiri barabara ndoto yake hii na maono yake haya ili vijana waweze kupata furaha kwa sababu wanaye Rais ambaye anawaamini,

anawategemea na tunawaamini vijana wote kama walinzi na watetezi muhimu wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwenye jambo lingine muhimu sana hasa katika kipindi cha miaka minne iliyopita ambacho Mheshimiwa Rais wetu ametuhudumia kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa wengi ambao tuna shukrani, kwa kweli Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa, kubwa sana. Kwa mfano, kwenye jimbo langu pekee ninalotoka, katika halmashauri ya Temeke ninayotoka peke yake, zaidi ya shilingi 323,000,000,000 zililetwa katika kipindi cha miaka minne na zimetekeleza na kusababisha mapinduzi makubwa sana katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo ninalotoka peke yake Jimbo la Mbagala vituo vitatu vya afya katika kipindi cha miaka minne peke yake, Hospitali ya Zakhem tunakamilisha kuijenga. Tunaenda kujenga hospitali nyingine kwa ngazi ya wilaya katika kata moja pale Toangoma ya ghorofa sita. Tunaenda kusababisha mapinduzi makubwa kwenye sekta ya elimu kama ambavyo tumefanya katika kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jimbo langu peke yake zaidi ya shilingi 123,000,000,000 zililetwa katika kipindi cha miaka minne. Jimbo moja tu lenye kata sita peke yake, pamoja na kwamba lina wakazi zaidi ya 500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye shukrani kama tulivyo Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, tunao wajibu wa kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumpa moyo, aendelee kuhudumia nchi yetu, kwa sababu tunaamaini katika kipindi cha miaka mitano inayokuja, matarajio makubwa ni kuona mapinduzi makubwa kwenye sekta zote kuanzia nishati, miundombinu, kilimo, na ajira kwa vijana. Yote haya lengo ni moja tu, kuhakikisha uchumi wetu unastawi na uweze kuwahudumia wananchi wetu ambao wanaongezeka kwa kasi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu kwa vijana kama kijana mwenzao, ni kuwaomba wawe wazalendo kwa nchi yetu.

Sisi sote tumetembea safari ndefu kufika tulikofika. Mimi miaka 32 iliyopita nilihamia Dar es Salaam nikiwa na miaka karibu 18. Leo hii tunapozungumza nimeaminiwa na Watanzania wenzangu katika eneo la Mbagala na kuwa mwakilishi wao baada ya kukaa hapo kwa miaka 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nchi yetu ni nzuri, kila mahali ulipo unayo nafasi ya kuhudumia watu. Nchi yetu hii ni kiasi tu kama kijana kupanga maono yako vizuri, kuwa mtii kwa nchi yako, kupenda nchi yako, kufanya kazi kwa bidii, kujituma na kuwa mtii kwa mamlaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyochangia, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge Kakulu kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Ngayiwa Benjamin Lukubha atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye ajiandae.

**MHE. BENJAMIN L. NGAYIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika mjadala wa kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa wakati wa kufungua ama kuzindua Bunge letu la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakupongeza kwa kuteuliwa kwako kuwa Naibu Spika wetu. Pia ninampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa nafasi hiyo ambayo anaitumikia. Nichukue fursa hii pia kuwashukuru wapigakura na wananchi wenzangu wa Jimbo la Kahama Mjini kwa imani yao kubwa waliyonipatia kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni siku njema ambayo tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini ni siku pia ya kumbukizi ya kuzaliwa kwake. Kwa hiyo, tunampongeza na kumwombea maisha marefu huko aliko, aendelee kututumikia

Watanzania kwa moyo wote kama ambavyo ameonesha kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya Mheshimiwa Rais ni hotuba ya kwanza kabisa aliyoitoa tangu tulipomaliza uchaguzi wetu mkuu tangu Oktoba, 2025. Hotuba hii iliakisi na kugusa maeneo karibu yote muhimu ya kisekta katika kuonesha Dira ya Maendeleo ya Taifa letu na kuinua hali ya uchumi kwa mwananchi mmoja mmoja katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi, Mheshimiwa Rais alipogusia kwa mfano, katika sekta ya ujenzi aliposema na ninamnukuu hapa anasema; "Tutaongeza pia bajeti na uwezo wa *TARURA* katika kuboresha barabara za ndani na za vijijini ili kuhakikisha zinapitika mwaka mzima na kuwa wakulima wanaweza kuyafikia masoko kwa urahisi."

Mheshimiwa Naibu Spika, humu Waheshimiwa Wabunge tulimpongeza kwa kumpigia makofi mengi sana, ikionesha kwamba shida kubwa au sehemu kubwa ambayo inatakiwa tuelekeze nguvu zetu ni katika kuboresha miundombinu yetu hasa barabara za ndani na zile za vijijini. Mheshimiwa Rais ameonyesha dhamira hiyo ya kuongeza bajeti kwa *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* hii ikiwa na umri wa miaka minane, kwa kweli imefanya kazi nzuri sana, lakini bado tunatakiwa kuendelea kufanya kazi iliyo bora zaidi na katika kuonesha kwamba tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika adhima yake ya kuboresha hali ya miundombinu yetu ambayo yeye anatamani ipitike kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ninawaomba tu watendaji wetu katika ngazi zote kwamba Mheshimiwa Rais anapohangaika usiku na mchana kutafuta fedha kwa ajili ya maendeleo, basi na sisi tuoneshe ile nia thabiti na dhamira ya kwenda kumuunga mkono katika kusimamia shughuli hizi za maendeleo ili wananchi wetu waweze kufaidika na jitihada hizi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijielekeza katika ukurasa wa 25 wa hotuba ya Mheshimwa katika sekta ya madini, pia Mheshimiwa Rais ameonyesha kutambua mchango wa sekta ya madini katika maendeleo ya Taifa letu. Katika hotuba yake inaonesha kwamba kiwango cha mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa, kiliongezeka kutoka asilimia 6.8 mwaka 2020 mpaka kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameonesha utayari wa kuwaunga mkono na kuwa-*support* wachimbaji wadogo kwa kuwawezesha kuwapatia vifaa vya uchimbaji kama vile vya uchorongaji, lakini na taarifa za jiolojia kuonesha kwamba madini yanapatikana wapi? Kwa wingi gani? Ni madini ya aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaiomba tu pia Wizara yetu ya Madini iende ikasimamie vizuri eneo hili kwa kuhakikisha kwamba ile mikopo ambayo Serikali inaenda kuitoa kwa wachimbaji wadogo, iende basi kwa walengwa ambao kweli wana uhitaji, mikopo isiende kwa wachimbaji ambao tayari wana uwezo wa kujiendesha wao wenyewe na kuendesha shughuli zao za uchimbaji, na tuende tukawaangalie wale vijana ambao wapo katika hali za kati ambazo sasa wanataka kupambana kuweza kuona kwamba wanaongeza tija ya uzalishaji katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba hata asubuhi wakati wa michango ya Waheshimiwa Wabunge walieleza kuhusu masuala ya mirabaha ambapo wachimbaji wanaonekana wanatozwa mirabaha mara mbili pale ambapo wanakuwa wameshatoa mawe juu, lakini pale ambapo wanakuwa wameshachenjua dhahabu na penyewe pia dhahabu inaenda kutozwa mrabaha tena kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Niabu Spika, kwa hiyo, tuende tukaangalie maeneo haya ili wachimbaji wetu, sisi kule usikumani tunaita wasitegemee tu *miganyalo*. *Miganyalo* ni zile posho ndogo ndogo zinazopatikana kwa wachimbaji hawa wadogo wanapokuwa wanachimba katika maeneo yao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa ambazo anazifanya na hotuba hii iende ikawe dira kwa taasisi zote za Serikali, taasisi binafsi, Wizara zote, tuweze kwenda kupita humu ambapo Mheshimiwa Rais wetu ameonesha dira kwamba sasa tunataka kuelekea upande gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngayiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko atafuatiwa na Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sasa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha wote kuwa ndani ya nyumba hii ya mipango na kutunga sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumtakia heri, kumtakia fanaka, kumtakia afya njema, kumtakia weledi na maarifa makubwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika siku yake leo ya kuzaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa lengo moja la kuongea na vijana wa Tanzania, kuwaelezea kwa nini wanapaswa kumwombea na kumlinda kwa wivu mkubwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote wanasiasa hupenda kuwekeza katika vitu ambavyo vinaonekana kwa macho na vinatoa majibu kwa haraka. Ni Tanzania pekee chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama yetu amewekeza kwenye taaluma ambayo haionekani na ambayo matokeo yake hayatokei kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nitaenda kwa ufupi, lakini nitatamani kugusa namna

ambavyo ameikuta elimu ya Tanzania sehemu ilipo na pahala anapoipeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 nilisimama hapa mwanzoni kabisa na nilimwuliza swali Mheshimiwa Profesa Ndalichako kipindi hicho akiwa Waziri wa Elimu, nikamwambia Mheshimiwa Waziri, humu ndani tunasikia taarifa, habari nyingi za kuhusu wale waliofaulu mitihani yao; waliofaulu darasa la saba wakaenda *form one,* waliofaulu *form four* wakaenda *form five*, waliofaulu elimu ya juu ya *form five* na *six* wakaenda vyuoni, vipi wale ambao huwa wanatemwa na mfumo darasa la saba, hawafanikiwi kusonga mbele, wanaishia hapo; *form four* hawafanikiwi kwenda mbele wakaishia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati natafakari majibu ya Mheshimiwa Profesa Ndalichako kipindi hicho Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan nilimsikia kwenye vyombo vya Habari, akiielekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanya mapitia ya mitaala ya elimu na sera ya elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni nini? Mwaka 2021 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuta changamoto kwamba watoto wanaohitimu Darasa la Saba ni takribani 1,900,000. Katika watoto hao, ni watoto takribani 900,000 peke yake wanapata fursa ya kwenda Kidato cha Kwanza. Watoto milioni moja takribani wanabaki mtaani, wanabaki vijijini wanakuwa ni mzigo kwa familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 wakati Serikali inafanya mapitio ya Sera na Mitaala ya Elimu, baada ya maboresho yake na kuanza mapema mwaka jana, 2025, ninavyozungumza sasa, hii habari ya kuwaacha nyuma watoto milioni moja wanaohitimu Darasa la Saba inaisha mwaka huu wa 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2027 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassana ameamuru kupitia mabadiliko ya sera na mitaala, watoto wote wanaohitimu darasa la saba wanakwenda elimu ya lazima mpaka *form four,* ule mzigo wa watoto milioni

moja waliokuwa wanabaki darasa la saba kuanzia mwakani haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie vijana wa Tanzania, wanalo jukumu la kumwombea na kumlinda kwa wivu mkubwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu za kidato cha nne, wanaohitimu ni kati ya wanafunzi 500,000 mpaka 560,000 nchi nzima. Hawa wanafunzi 500,000 wanaohitimu kidato cha nne wanaokwenda kidato cha Tano ni takribani 100,000 mpaka 150,000. Wanafunzi zaidi ya 300,000 miaka hii yote ya nyuma walikuwa wanabaki mtaani, wanabaki kuwa mzigo wa familia na wazazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewekeza kwenye elimu ya kati, amejenga vyuo vya kati vya *VETA*, tunazungumzia ndani ya miaka minne ya uongozi wake, ameshakamilisha na vinatoa mafunzo vyuo 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tulikuwa tunazungumzia vyuo 47 tangu kuumbwa kwa Tanzania. tulikuwa na vyuo vya *VETA* 47. Ndani ya miaka minne ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga na vimeshaanza mafunzo vyuo 33. Tunavyozungumza sasa, Mama ameshatoa shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo 65. Vyuo 64 vya wilaya na chuo kimoja cha mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini anachotazama Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan? Anachotazama ni kwamba dunia imeshabadilika, dunia sasa haimthamini mwanadamu kwa idadi ya digrii alizonazo, inamthamini mtu kwa ujuzi *(competence)*. Wewe umebobea, unao uwezo wa kufanya nini? Kutatua changamoto gani kwenye jamii? Dunia ndiko inapoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuwekeza kwenye elimu ya kati, amejenga vyuo vya kati, amejenga vyuo vya *VETA* bado anatoa

mikopo kwenye baadhi ya *course* kwenye vyuo vya kati. Nataka niwaambie Watanzania wanaonisikiliza, kwamba tunalo jukumu la kumwombea na kumlinda kwa wivu mkubwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye elimu ya juu. Tulikuwa tunazungumzia watoto wanaojiunga na vyuo vikuu takribani 100,000 mpaka 120,000. Tunavyozungumza sasa kwa mwaka ule wa kwanza, acha wanaoendelea na masomo, wanajiunga zaidi ya watoto 205,000. Kwa nini? Kwa sababu miundombinu ya vyuo imeongezeka, wakufunzi, Maprofesa walimu vyuoni wameongezeka, vifaa vya kufundishia vimeongezeka na ufaulu wa watoto kwenye mashule yaliyoboreshwa nao umeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea hapa, watoto wa maskini wamesoma bure kuanzia elimu ya msingi mpaka sekondari mpaka *form six,* sasa wanakwenda chuo kikuu. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwaka 2021, na kwa bahati nzuri, nimekuwa kwenye Kamati ya Elimu, na nimeshuhudia bajeti kila mwaka 2021 humu ndani tulipitisha bajeti ya takribani shilingi bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu pekee.

Meshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza sasa Serikali inatumia na imeshakopesha wanafunzi takribani bilioni 919, mategemeo yangu, bajeti ya mwaka 2026/2027 tutakwenda kwenye zaidi ya shilingi trilioni moja kadhaa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu pekee. Mikopo hiyo inakopesha zaidi ya watoto 250,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka vijana wanielewe kwamba tukisema tunamlinda Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunamaanisha kitu gani? Pamoja na mikopo hiyo ya elimu ya juu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshaona mbali, ameona dunia inataka wasomi, dunia inataka watu wenye ujuzi *(competence),* Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tunavyozungumza sasa anatoa *Samia Scholarship,* anapeleka watoto wa Kitanzania mpaka nje ya nchi. Zaidi ya watoto 5119 mpaka sasa wamepata *scholarship* ya Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, *scholarship* hiyo siyo mkopo, ni *grant,* ni ruzuku, unapewa *for free* ilimradi uwe umefaulu masomo ya sayansi. Takribani shilingi bilioni 30 imeshakwenda huko. Tunavyozungumza sasa, kuna watoto wamekaa *camp* pale Arusha wanapigwa msasa kwa ajili ya kwenda nje ya nchi, kwenda kusoma *course* za sayansi kwenye sayansi, *nuclear science,* wanaenda kusoma kwenye *artificial intelligence,* wanakwenda kusoma zile *course* ambazo tuna upungufu mkubwa au hatuna wataalam nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, haitazami Tanzania kama tunavyoitazama sisi leo hapa. Ameshaona mahitaji ya nchi yetu kwa miaka mingi ijayo, amewekeza kwenye maeneo ambayo yataleta tija,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, malizia.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** …pengine hata kipindi ambacho yeye hatakuwepo katika Kiti cha Urais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Nakutakia kila la heri, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Makofi yanaashiria mchango umesikika vizuri sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye atafuatiwa na Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia jioni ya leo katika hotuba ya Mheshimwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze na kumshukuru Mungu, Muumba Mbingu na Dunia na kila kilichopo,

kwa neema kwa kunipa kibali, watu wa Kigoma Kaskazini kunichagua kwa kura nyingi za kishindo. Niseme nawapenda sana wananchi wa Kigoma Kaskazini, na nipo hapa kuwatumikia kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikiliza Mheshimwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nilimsikiliza vizuri na nimesoma vizuri hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais, kwa mtu yeyote mwenye akili timamu na mwenye kulipenda Taifa lake ilikuwa ni hotuba bora ambayo inaonesha dira ya Watanzania. Sasa Watanzania tunachokitaka, ni utekelezaji wa yale Mheshimiwa Rais aliyoyasema katika hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza katika hoja mbalimbali nikianza na hoja ya kilimo. Ni ukweli usiopingika kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo katika Taifa letu la Tanzania. Asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo, na hata sisi tupo hapa leo wengi, tumesomeshwa na wakulima. Maana yake hatuna budi kama Taifa kuwa na mikakati bora ya kusaidia kilimo chetu, lakini tuwe na mikakati bora ya kupata viwanda ambavyo vitasababisha vijana kupata ajira na kutoka kwenye changamoto ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi hapa katika mazao ya biashara, ndani ya Mkoa wangu wa Kigoma tunalima zao la Michikichi. Malaysia kwa historia zao la Mchikichi walichukua mbegu katika Mkoa wa Kigoma, Kata ya Simbo, leo Malaysia ni nchi ya tatu kwa kuzalisha mafuta yanayotokana na mchikichi, lakini ukija Tanzania zao la michikichi ambalo tunalima sana Mkoa wa Kigoma katika Jimbo langu la Kigoma Kaskazini, bado hatujaona manufaa makubwa yanayotokana na zao la mchikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kwamba, katika dira ambayo Mheshimiwa Rais ametupatia kama Taifa twende tukawekeze katika zao la mchikichi, tukawashawishi wawekezaji waje wawekeze viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma tupo mpakani mwa Congo, tupo mpakani wa Burundi. Warundi, Warwanda, na Wakongo wanaweza wakaja wakachukua mafuta yetu na hata nchi nyingine nasi tukawa nchi ambayo tunasafirisha mafuta kwa wingi kutoka Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, ushauri wangu katika zao la mchikichi ni kwamba mpaka sasa hatuna bodi katika zao la mchikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia zao la pamba tuna bodi, ukiangalia zao la kahawa tuna bodi, lakini zao la michikichi hatuna bodi. Sasa Mheshimiwa wa Kilimo, ambaye yuko hapa ananisikiliza, ni muda muafaka kuhakikisha kwamba, zao hili la michikichi tunapata bodi, ili tuweze kusimamia kwa ukaribu, tuweze kuzalisha kwa wingi na kuwa nchi ambayo tunasafirisha mafuta duniani na maeneo mbalimbali ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie suala zima la afya. Hakuna asiyejua kwamba, afya ni kila kitu kwenye maisha ya mwanadamu. Bila afya hatuwezi kuwa na Taifa ambalo ni imara. Ili tuwe na Taifa imara tafsiri yake ni lazima tuwe na wananchi ambao afya zao zimeimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hotuba ya Mheshimiwa Rais ameonesha dira ya kuanzisha bima ya afya kwa Watanzania wote na ni kiu ni kuhakikisha kwamba, wote tunapata bima ya afya kwa sababu, tukienda kwenye majimbo yetu sisi ni mashahidi, vijijini kuna watu wanapoteza maisha kwa sababu, wamekosa pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu anakwenda hospitali hana bima hana pesa, tafsiri yake ni anaweza akapoteza maisha kwa sababu ya umasikini wake. Kwa hiyo, kama leo tutakwenda katika mpango wa Bima ya Afya kwa Watanzania wote itawasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa natamani sana kupendekeza, inawezekana sana kama Taifa tukaweza kuwatibu Watanzania wote bure, inawezekana kabisa. Kwa mfano, ndani ya chama changu tulitoa *solution* kwamba, katika pato la Taifa

hata tukitenga asilimia mbili pointi tano ya kuweza kuwasidia Watanzania tunaweza tukahudumia Watanzania milioni 11 ambao watapata bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naamini kabisa kama tutajipanga vizuri, na kama Mheshimiwa Rais alivyotuambia Watanzania, natarajia tunakokwenda mbele huduma za afya zitakuwa bora. Tunaposema sema huduma ya afya hatuzungumzii majengo pekee yake, shida ya Watanzania ni majengo na huduma bora ya afya. Sera inasema kila kata kutakuwa na kituo cha afya, lakini sasa kuna maeneo ambayo hata ndani ya jimbo langu, hatuna vituo vya afya, kuna vijiji ambavyo hatuna hata zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani ni fursa, kupitia Hotuba hii ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inatoa matumaini kwa Watanzania tujitahidi. Mawaziri ambao mmepewa dhamana kusimamia hizi Wizara twende tukahakikishe kwamba, tunaboresha huduma bora ya afya. Moja ya kero kwenye afya ni suala la wananchi kuzuiwa kutoa maiti hospitali. Mheshimiwa Rais amesema kwamba, watu wapewe maiti, lakini watafute waende wakalipe deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua nia ya Rais ni njema, kuwasaidia Watanzania, lakini mnaonaje tukawasaidia hata tukafuta kabisa tozo ya kutoa maiti hospitali?

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kwa sababu, leo *imagine,* labda mimi nimefiwa na mume wangu halafu narudi nyumbani, mmenipa mwili nikazike, nina-*stress* za kufiwa, halafu natafuta hela ya kwenda kulipa deni hospitali. Katika hali ya kawaida inahitaji Roho Mtakatifu, lakini siyo kazi rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natamani sana, sisi kama Wabunge, katika hili tuwasidie wananchi ikiwezekana tufute kabisa kodi ya kutoa maiti. Tukiamua tunaweza, kama Taifa, kuwasaidia Watanzania, mtu amekufa... *(Makofi)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiza, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer* Aisha Ulenge.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpe hii taarifa mzungumzaji kwamba, anapokuwa anachangia ajue *the logic behind* bima ya afya. Tutakapokwenda kuingiza bima ya afya, wananchi wote wakawa wanatibiwa kwa bima ya afya *issue* ya maiti kuzuiwa itakuwa haipo. *So,* anatakiwa a-*read between the lines* katika kupata *concept* halisi ya bima ya afya, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiza, taarifa unaipokea? Ahsante.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, taarifa hiyo siipokei na tusichangie kwa mihemko, lengo letu ni kujenga kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametoa hili, lakini kwa ushahidi, leo kuna hospitali ambazo bado watu wanazuiwa maiti. Kwa hiyo, ninapochangia hapa, lengo langu ni jema katika kuhakikisha kwamba, tunawapunguzia mzigo Watanzania na tusilete mihemko wala matabaka ya chama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninazungumzia suala hilo la maiti, kwa hiyo, mimi natamani Watanzania tuwapunguzie mzigo...

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Husna.

**TAARIFA**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Mbunge haruhusiwi kuzungumza hoja ambayo hana ushahidi nayo, kwa sababu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwamba, ndani ya siku 100 hataki kuona maiti inazuiliwa na alitoa maelekezo namna ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo sasa kama Mheshimiwa Mbunge ana ushahidi na hospitali ambayo imezuia maiti ni vizuri akatupatia, ili kuweka takwimu sahihi, nashukuru *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taarifa ya Mheshimiwa Mbunge unaipokea? Muda pia umeisha, umalizie, ahsante.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hiyo siipokei na ninaendelea kusisitiza, lengo langu ni kuhakikisha kwa pamoja, sisi na Mawaziri tumsaidie Mheshimiwa Rais. Hospitali zote ambazo bado watu...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MBUNGE FULANI:** Mnapoteza muda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umeisha, naomba umalizie sentensi ya mwisho.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba unilinde, kwa sababu wameniingilia, naomba uniongezee dakika mbili.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika Taarifa. Hatujamwingilia, sisi hatuna uwezo wa kumwingilia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, Taarifa ni sehemu ya kuchangia.

Mheshimiwa Jacqueline sijakuruhusu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, unapotoa taarifa kwa Mbunge anayechangia, hakuna muda wa ziada. Taarifa ile ni kwamba, unamwongezea au unatoa ufafanuzi kutokana na hoja anayosema. Kwa hiyo, muda umeisha, malizia sentensi ya mwisho Mheshimiwa.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikutumwa na Wana-Kigoma Kaskazini kuja kubishana, nimekuja kujenga hoja. Mwisho ni suala zima ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru kwa sababu, alitoa maelekezo, akina mama wajawazito wanaoambiwa wapeleke beseni, wembe, mpira, mpaka kibana kitovu cha mtoto, sasa ni marufuku. Ni muda wetu kuhakikisha kwamba, hawa akina mama kweli, wakienda hospitali wanapata hivyo vifaa na kupata huduma iliyo bora. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae. Ahsante.

**MHE. JUMA KHAMIS SADIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutuwezesha kufika siku hii ya leo tukiwa na hali ya uzima na afya zetu zikiwa zinaendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii. Ninawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Donge kwa kunirejesha tena kuwa Mbunge wa Jimbo la Donge kwa Awamu ya Tatu sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tutakubaliana hapa kwamba, Mama Samia, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amedhihirisha ndani ya Bunge Tukufu hili

na ulimwengu kwa ujumla kwamba, yeye ni mama bora. Mama wapo wengi, lakini sio kila mama anakuwa mama bora. Mama bora ni yule ambaye anawajali watoto wake, anayewanasihi watoto wake, anayewalea vizuri watoto wake na anayewaonesha njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia Suluhu Hassan hotuba aliyoitoa hapa Bungeni amedhihirisha kwamba, yeye ni kiongozi bora na nina sababu, na kila mmoja ana sababu zake hapa za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukienda uki-*google* na wale waliokwenda vyuo vikuu, sifa za kiongozi bora mojawapo ni kuwa msikivu na nyingine ni kuwa na maarifa, hekima, busara, uvumilivu, ujasiri, uhodari na maamuzi. Zote hizi zinaelezea sifa za kiongozi bora. Ukiangalia hii *speech* ambayo Mama Samia ameitoa hapa amedhihirisha kwamba, yeye ni kiongozi bora. Amewahimiza watoto wake, Watanzania, na wajukuu zake juu ya umuhimu wa kusimamia amani na usalama wa nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika umuhimu wa amani ndiyo kitu pekee, bila ya amani, bila ya usalama, hakuna chochote cha maendeleo kitakachofanyika. Hata hao wataalamu wa mambo ya usalama duniani, wa mambo ya ulinzi duniani, wote wametoa kipaumbele kuhusiana na suala la umuhimu wa usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano. *Realists, liberals,* kila mmoja hapa ana mtazamo wake katika kusimamia amani. *Liberals* wanaamini katika suala la umoja na mshikamano, *cooperation, institution. Realist* wao wanaamini katika *force* kusimamia amani. *Realists,* akina Hans Morgenthau, wanaamini katika kusimamia amani hakuna mbadala, wao wanaamini *force* ndiyo *approach* pekee ya kusimamia amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia, Rais wetu amekuja Bungeni akatuhutubia akawaasa vijana na watoto wake, Watanzania kwamba, changamoto ni wataalamu wanaamini *conflict is unavoidable*. Changamoto hizi na migogoro ni mambo

ambayo hayawezi kuepukika. Je, tunatumia *approach* gani katika kutatua migogoro yetu na matatizo yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Samia *approach* pekee ambayo amewaasa watoto wake katika kutatua changamoto zetu tutumie *diplomatic means,* ndiyo njia pekee itakayotusaidia. Ndiyo maana akawaambia Mawaziri wake atakaowateua na wengine ambao tayari amewateua kwamba, Waziri yeyote lazima awe kiongozi shirikishi, vijana wa Tanzania washirikishwe katika maeneo mbalimbali. Nawapongeza sana Mawaziri walioteuliwa, ni kweli wanamtendea haki mama, wanafanya kama alivyowaagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naseme vijana wenzangu, wengine kwenye ujana tunaondoka huko sasa. Nawaambia vijana, nchi hii ni ya kwenu nyie, usikubali kushawishiwa, ukashawishika kuiharibu nchi yako. Mama anajionesha kwamba, yeye ni mzalendo wa Taifa lake na kila mzalendo wa Taifa lake, mwenye akili timamu, atakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Rais kwamba, lolote liwalo, tusione kwamba, leo sisi Tanzania tuna amani. Wenyewe wanasema ukiona kimeundwa kinaelea, ujue kinafanyaje? Yupo muundaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu huko hawalali kwa kuitunza amani hii. Hii ndiyo *value* ya nchi yetu, kwa hiyo, nimesema nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha anawaasa watoto wake wanasimamia amani, umoja na mshikamano wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni suala la umuhimu wa muungano. Ni ukweli usiopingika, mimi bahati nzuri ninatokea upande wa pili wa Muungano wa Zanzibar, upande wa Zanzibar wote tunakubaliana kwamba, muungano wetu huu unafaida kubwa kwetu na njia pekee ya kutatua changamoto zile za muungano ni kama Mawaziri wetu wanavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia muungano huu, na niseme ukweli, hata ukienda duniani huko kuna nchi nyingi ziliungana, wanatamani na walishindwa ule muungano wao

kudumu. Tanzania pekee mpaka leo hii ndiyo tunaongoza katika muungano wetu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine aliloligusia Mheshimiwa Rais ni suala la kusambaza huduma za jamii, ikiwemo mambo ya ujenzi. Tukubaliane, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dodoma ya mwaka 2010 mpaka 2020 ni tofauti na Dodoma ya Mama Samia leo. Huo ndiyo ukweli. Dar es Salaam ya mwaka 2010, mimi nilikuwa Mbunge hapa toka 2010 mpaka 2020, mimi juzi nimepotea Kisasa. Pale Kisasa nikazungukazunguka wee, naitafuta *Martin Luther,* ile njia ya Waziri Mkuu, nikazungukazunguka maana ilikuwa usiku. Ni kwa sababu, mabadiliko makubwa ambayo alimeyafanya Mama Samia kwa kipindi cha muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukitembea barabarani huko utakuta barabara ya lami mgongo wa ndizi. Natoa mfano, barabara za namna hii unazikuta maeneo machache sana, ni Tanzania na Zanzibar. Mama Samia na Dkt. Husseni Ali Mwinyi wamekuja kufanya mabadiliko makubwa na nikwambie ukweli, unajua watu walivyokuwa wanamwangalia Mama Samia hawakutarajia atakuja kufanya mambo makubwa kama haya ambayo ameyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mama amedhihirishia umma, ameudhihirisha ulimwengu kwamba, mama ni mama. Mama ana maamuzi, ndiyo maana hata ukifuatilia katika *statement* zake unajua hasa huyu ni kiongozi wa aina gani? Huyu ni Amiri Jeshi Mkuu. Huyu ni Mkuu wa Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mimi nimewahi kuwa mwanajeshi. Nataka niseme siyo kila kiongozi huwa ana maamuzi. Mimi nimekaa na viongozi wengi, sitaki kuwataja majina hapa, wengine tulifikia *stage* tukawa tunagombana kwenye vikao, tukaonekana hatuna adabu. Ni kwa sababu, unamkuta hana maamuzi, unamshauri hili hawezi. Mama huyu amekuja kuonesha yeye ni kiongozi wa namna gani? Nataka nikwambie kupata ujasiri wa kutamka lile neno, *who are you? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kila mmoja ana ujasiri wa kuja kulitamka lile neno, tena hadharani, *yes,* kwa sababu, kuna watu wamejiona kwamba wao ndio wababe wa dunia kwamba, wanachokitaka wao ndicho hicho hicho. Mama amekuja, ametuonesha mwanga wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wako. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae. Ahsante sana.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia hoja ambayo iko Mezani ya Hotuba ya Ufunguzi wa Bunge kutoka kwa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kweli, ni bahati iliyo njema, ni tajamara na sudi kupata nafasi ya kuingia hapa katika Awamu ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo jambo rahisi. Sisi sote tunajua tuliyopitia huko, kwa mapenzi yake Mwenyezi Mungu tumeweza kufika hapa kuwawakilisha wananchi wetu. Wananchi wametutuma hapa tusemee changamoto zao, tushukuru kwa tuliyoyapata na tuendelee kuomba tena, ili changamoto za maendeleo zipunguke, ziondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nami nashukuru chama changu kwa imani, pamoja na wajumbe na wananchi wa Kilombero kwa kunipa dhamana hiyo. Kama walivyosema Wabunge wengine, nami nasimama hapa katika Bunge lako Tukufu kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa yale makubwa ambayo ametufanyia na anayoendelea kutufanyia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu, tunaona Mawaziri wakihangaika kila kona chini ya kiongozi wao,

Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, wakipambana katika kuhakikisha nchi yetu inaenda kwa usalama na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana na wananchi wa Kilombero wameniambia, Mheshimiwa Asenga tunakutuma mara ya pili, nenda kashukuru, tulikuwa hatuna barabara ya lami. Hapa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa 28, anazungumzia habari za barabara za lami kwa majimbo ambayo hayajapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunajua adha ya kukosa barabara ya lami na barabara hiyo ilikuwa chini ya Wizara ya Fedha, wakati huo Mheshimiwa Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu alikuwa Waziri wa Fedha, ndiyo ilikuwa barabara pekee iko chini ya Wizara ya Fedha, siyo Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza tuna kilometa 67 za lami tunateleza tu. Wananiambia, Mheshimiwa Asenga nenda kashukuru, kamshukuru Mheshimiwa Rais. Tunawashangaa hao watu wa mjini huko wanavyoleta vurugu, sisi hatutaki vurugu na ndiyo maana Kilombero, tarehe 25 ile, sijui 26, tulikuwa salama na amani. Vijana wa Bodaboda walikuja kwangu, hasa wale pale Msikitini Mjini, wananiambia mwambie *OCD* Mheshimiwa Asenga, Mbunge, sisi hatuna nongwa, kwa nini anatuambia tufunge saa 12?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunataka amani, sisi watoto wa masikini, tukiendesha bodaboda ndiyo tunakula. Tukiendesha bodaboda, tukitoka ndiyo nguo zetu zinafuliwa. Sisi tunalinda amani. Kwa hiyo, wamenituma, kazi yangu kubwa hapa ni kuja kusema ahsante kwa yale ambayo tumeyapata na kusema tunaomba tena kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Wilaya inaundwa sisi hatuna Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya; leo ninavyozungumza na wewe, tunayo hospitali hiyo, na Mheshimiwa Rais ametuletea shilingi milioni 800 tunajenga wodi ya akina mama, wodi ya watoto na wodi ya wanaume. Mwenyezi Mungu ambariki sana Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulisimama hapa katika Bunge lililopita, tukasema umeme unakatika sana. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amezungumzia hiyo, ametuletea shilingi bilioni 25, tumejenga *substation* Kilombero na Mheshimiwa Rais amefika pale, umeme haukatiki tena Ifakara. Mwenyezi Mungu amlinde sana Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamsihi na kumnasihi Rais wetu, Mwenyezi Mungu amjalie kifua kikubwa, kwa sababu Mwenyekiti wangu wa vijana Mheshimiwa Sadifa ametoka kusema hapa; alikuwa Mwenyekiti wetu wa Vijana wa Taifa, tulikuwa tukienda naye, na anatutuma twende tukawatetee Marais waliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mijadala mbalimbali tunamwambia Mheshimiwa Rais asife moyo kwa sababu kuna wananchi hawatampenda wote, lakini hawatampenda kwa hulka zao. Tuliona hivyo kwa mzee wetu Mkapa, yalizungumzwa yaliyosemwa; tuliona kwa mzee Jakaya, amekuwa madarakani anamaliza kipindi chake, maneno yote, mzee anaondoka madarakani watu wanakumbuka mazuri yake kwamba hata kilometa 11,000 za lami alifanya yule mzee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwambia Mheshimiwa Rais, kama walivyosema kwa Rais Dkt. Magufuli, na wanaendelea kusema hana jema, wapo. Sasa sijui kama wanasemea gerezani au wanasemea wapi? Lakini wanaendelea kusema, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli hana jema, pamoja na Mwenyezi Mungu kamchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Samia atafanya atamaliza, kuna watakaomshukuru na hao watakaoendelea kusema maneno yake. Tunamwomba Rais wetu asife moyo, yasimnyong'onyeze, kwamba anakata tamaa, ndizo hulka zetu sisi. Atakapomaliza, mwaka mmoja akija Rais mpya utasikia hakuna kama Samia hapa. Kama tulivyozungumza, hakuna kama Mheshimiwa Dkt. Magufuli, kama tulivyosema hakuna kama mzee Jakaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninasema hapa kumpa moyo Rais wetu, kumwambia akaze buti asonge mbele. Madhali

akijithibitishia yeye ni muislam. Wazanzibar hawa wenzetu katika Muungano ni watu wema kweli. Ukienda Zanzibar mtu anaweza akakupeleka hata kilometa tano anakuonyesha sehemu ambayo wewe huijui. Ni waungwana. Wasivunjike moyo kwa changamoto hizi tunazozipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi na wananchi wa Kilombero hatuwezi kumbeza Rais wetu kwa sababu kuna mtu yuko nje ya nchi huko kasema sijui kuna wizi sijui kuna namna gani? Yeye na familia yake, watu wanaibeza, Rais wetu asivunjike moyo. Rais akisema mtoto wake akae sehemu hapa apate nafasi, maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kama mimi mtoto wa fundi cherehani ninapata nafasi Bunge la kwanza kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu tuko naye kipindi cha tatu, kupewa Unaibu Waziri nongwa mpaka mnaandika huko kwenye mitandao, nongwa! Nchi imeuzwa, wameuza watoto, hivi Abdul leo ukimwangalia na wema wake ule, anavaa *sandals* na kanzu atauza nchi yetu!

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo waliyoyasema wakati wa Ridhiwani hapa, *brother* wangu. Ridhiwani aliambiwa magorofa ya bandari; hata nilikuwa sijui wakati ule kama ya bandari. Nikamwuliza, mzee maghorofa yale mapacha ya kwako kumbe, mimi ninakufa njaa tu hapa! Nitoe bwana. Akasema, uongo tu. Kila mali ya Ridhiwani. Leo kiko wapi? Tunakula pamoja naye *canteen* pale *brother* wangu. Kwa hiyo, akina Abduli hawa Mungu awape nguvu tu, haya yatapita tutasonga mbele pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, niseme kwamba sisi tunataka kufungua Wilaya ya Kilombero, Mkoa wa Morogoro. Tumesaini Barabara ya Ifakara kwenda Malinyi baadaye itakwenda Songea. Tumesaini Barabara ya Ifakara kwenda Mahenge, Lindi, tumesaini Barabara ya Ifakara kwenda Mlimba. Ee, Mwenyezi Mungu ninakuomba umjalie Rais Samia apate fedha barabara hizi zianze, wananchi wetu wapate raha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake amesema kwamba uwekezaji mkubwa wa dola bilioni 42 unakuja katika gesi, tunaunga mkono. Tunaunga mkono uwekezaji wa Bandari ya Bagamoyo iunganishe na Kwala, *SGR* iende katika Bandari ya Dar es Salaam. Tumeokoa shilingi bilioni 256 katika uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulibezwa hapa, tulitukanwa, mjadala ulikuwa nchi nzima kuhusu uwekezaji wa bandari. Leo nani anasema kwamba tumeokoa shilingi bilioni 256? Hakuna. Ninarudia kumpa nguvu Mheshimiwa Rais, ninamwambia akithibitika mbele ya Mwenyezi Mungu jambo hili akiulizwa na Mwenyezi Mungu siku ya hukumu anaweza kujitetea, lina maslahi na wananchi wa Tanzania, alifanye, asirudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wataendelea kupinga na kusema; na madhali Mwenyezi Mungu sio Athumani, tumepata mifano ya nchi nyingine hapo yametokea kama ya Tanzania. Watanzania wameamka sasa, wanasema kumbe nchi yao inachochewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuja Mheshimiwa Rais Kilombero akatuzindulia kiwanda cha sukari. Wananchi wamesema tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa uzinduzi wa kiwanda cha sukari, lakini nikamwambie Mheshimiwa Rais, tunaomba bei ya sukari ichangamke ili wakulima wa muwa tuweze kulipwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninawasilisha katika meza yako hapa, na Waheshimiwa Mawaziri wako hapa, Mheshimiwa Rais alikuja pale. Mheshimiwa Rais alipita na mimi nikachomekea, kwamba, kuna kiwanda cha *Mang'ula Mechanical and Machine Tools,* kikianza kupata mwekezaji vijana wetu wengi watapata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema mbele zako hapa, kiwanda kile kikianza wananchi watapata ajira na vijana wangu watapata ajira. Bunge lililopita Mheshimiwa Rais amenisaidia fedha kupitia *TANESCO,* shilingi milioni 400 ku-*control* mto unaopita Ifakara Mjini, kujenga tuta upande mmoja, kuelekeza

maji Mto Kilombero ili maji yaende katika Bwawa la Mwalimu Nyerere ili tupate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamenituma baada ya kushukuru niseme hapa, bado shilingi milioni 400 za kujenga tuta upande wa pili ili tuendelee kuthamini chama chetu, tuendelee kumthamini Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Asenga. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuungana na Wabunge wenzangu kwa ajili ya hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyokuja Novemba 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kupata kura nyingi za kishindo kupitia wananchi waliomchagua tarehe 29 Novemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Spika pamoja na wewe kwa kuaminiwa na Wabunge kuwa mtuongoze katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwapongeze Wabunge wote waliokuwa ndani ya Bunge hili kwa kuchaguliwa na wananchi na kuaminiwa; tuko mahali hapa kwa ajili ya kujenga Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwashukuru wananchi wa Jimbo la Nsimbo kwa kuniamini tena kurudi tena katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa maono makubwa aliyonayo katika utekelezaji wa kazi mbalimbali za nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu gani? Kwa sababu tumeona jinsi gani alivyoanza. Alikuja hapa akasema, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi utaanza ndani ya siku 100. Tumeona mawaziri kupitia Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na Mawaziri wote kwa kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tumpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika nchi yetu. Tumeona akitembea katika maeneo mbalimbali na kutatua matatizo ya wananchi. Vilevile Mawaziri na Manaibu Waziri tumeona kazi ambazo mnaendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kazi kubwa ya afya iliyofanywa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwatibu Watanzania. Ndani ya mikoa yetu tuna Hospitali za Mikoa, ambazo zimewekwa vifaa vyote ambapo sasa hivi mikoa yote wanajitegemea, hatutegemei tena Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mkoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amehakikisha amejenga hospitali ya rufaa, na kuhakikisha anaweka vifaa tiba, na vifaa vyote muhimu kwa ajili ya Watanzania. Alisema, amefanya na amethubutu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tumpongeze kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ana maono makubwa. Sisi wenyewe ni mashahidi, tumeona vitu ambavyo amevifanya katika nchi yetu kupitia zahanati, na kupitia vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii katika maeneo yetu ya vijijini na vitongojini kuna zahanati na kuna vituo vya afya, wananchi wanatibiwa huko katika maeneo yao ya vijiji, wanajifungua vizuri.

Zamani mwanamke alikuwa anatembea maili sita au saba, lakini sasa hivi hakuna. *Ambulance* zipo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amepeleka *ambulance* kwenye kila eneo la vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja kwenye kipengele kingine cha barabara. Amewezesha *TARURA,* sasa hivi vijiji na vitongoji ameviunganisha, tumejengewa madaraja ambayo hayo yote yalikuwa hayapo, ameyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na amefanya mambo makubwa ambayo hatukuyatarajia. Kwa hiyo, ni lazima leo tumpongeze kwa kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona ni jinsi gani Mheshimiwa Rais ameleta fedha katika halmashauri zetu. Ameleta fedha nyingi ambazo hazikuwepo. Halmashauri ilikuwa haina fedha, lakini leo halmashauri wana miradi ambayo mpaka sasa hivi wanashindwa kuifanya kwa sababu ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono mapana aliyokuwa nayo kwa ajili ya Watanzania. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana haki ya kupata kura za kishindo za 97%. Nni halali yake kwa sababu kazi kubwa imefanyika kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kwenye utalii. Watalii katika nchi yetu walikuwa wanaingia wachache sana. Mimi katika jimbo langu nina Mbuga ya Katavi, kulikuwa hakuna watalii kabisa, lakini kupitia *Royal Tour* ya Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikwenda kukaa porini kutafuta na kuhakikisha kuwa ana-*promote* utalii ili watalii waweze kuja katika nchi yetu ili tupate uchumi mkubwa na mapato makubwa. Sasa hivi tunaona watalii wengi ndani ya nchi yetu ya Tanzania, mapato yameongezeka, na watalii wa ndani na nje wote sasa hivi tunakwenda katika mbuga zetu kupitia hamasa ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hayo yote ameyafanya, tumeyaona na kuyahakikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwenye kilimo, kulikuwa na mazao ya kahawa, tumbaku, na pamba ambayo yalikuwa

yalikuwa yana bei ya chini, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuja na mikakati ya kilimo kupitia mazao ya kibiashara ya pamba, tumbaku, kahawa, pamoja na korosho, leo hii tunaona jinsi wananchi walivyo na furaha na mapato ya mazao hayo ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan amehakikisha kuwa yamekuwa katika hali ya kiuchumi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona ni jinsi gani ambavyo pembejeo, mbolea, na mbegu, zimefika kwa wakati katika maeneo yetu ya vijijini. Sasa hivi mbolea inakwenda mpaka kwenye vijiji, mbegu zinakwenda mpaka kwenye vijiji, mbegu zimeondolewa ushuru, sasa hivi mkulima anapewa mbegu kwa bei nafuu ili aweze kulima kwa ajili ya manufaa na uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Haya yote yalikuwa hayapo, ameyafanya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Leo wananchi wana haki ya kumpa kura zote za ndiyo kwa sababu ameyafanya mambo makubwa na mazito katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona umeme katika nchi yetu ya Tanzania vijiji vyote, sasa hivi tunaelekea kwenye vitongoji. Umeme ulikuwa haupo, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia kuhakikisha vijiji vyote sasa hivi tunaenda kumalizia kwenye vitongoji. Ina maana shughuli za viwanda, shughuli ndogo ndogo, wananchi ndani ya vijiji vyetu na vitongoji vyetu wanafanya shughuli zao kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusimamia amani ya nchi yetu ya Tanzania, kwa sababu ameisimamia na kauli zake tunazion. Hata kama kulikuwa kuna changamoto ambayo imetokea, lakini alipotoa kauli, Watanzania wote wamejitafakari, wameona lile lililotendeka siyo sahihi kwa sababu tumeibomoa wenyewe nchi yetu ya Tanzania. Haya mambo hayakuwepo, wameona uchungu ule wa kukaa ndani, *lockdown* ya siku tano, wanasema loo, kumbe hivi ndivyo ambavyo huwa inakuwa? Wenzetu ndivyo ambavyo huwa wanavyopata taabu, namna hii? Leo hii hatutaweza kurudia tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana walikuwa hawakopeshwi pikipiki, lakini ndani ya halmashauri zetu vijana sasa hivi wanakopeshwa pikipiki, wanakopeshwa 10%, imesimamiwa vizuri, wanapata mikopo, wanafanya shughuli za kilimo, wanafanya shughuli za mashamba kwa mahekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa kipindi cha miaka minne iliyopita. Kazi kubwa na Watanzania wameiona, Watanzania wamethamini, unyenyekevu wake, wamethamini. Ninaomba sisi Watanzania, sasa hivi kilichobaki kwetu ni kuendelea kumwombea Rais wetu maisha marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, ajiandae.

**MHE. KENETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kuunga mkono hotuba hiyo. Pia nichukue nafasi hii kwa dhati niwashukuru wananchi wa Jimbo la Bahi kwa imani kubwa waliyoionyesha kwangu na kunirejesha tena katika kipindi hiki cha pili. Nami ninataka niwahakikishie kwamba nitawatumikia kwa moyo thabiti kabisa kulinda imani ile ambayo wameionyesha kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kile cha miaka iliyopita ambayo amefanya kazi kubwa, na sasa wananchi wameonyesha imani, walimpa kura za

kutosha ili kuweza kuwatumikia kwa kipindi cha miaka hii mitano mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita zaidi katika suala zima la sekta ya kilimo. Mheshimiwa Rais aliweza kutoa nukuu kwamba kilimo ni biashara, mkulima ni mwekezaji. Kupitia katika hotuba yake, aliweza kuainisha zaidi kwamba Serikali ambayo alikuwa anaahidi kwamba ataenda kuchagua watendaji wawe thabiti katika kusimamia, ni vipengele na malengo ambayo ameweza kuyaainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu 75% ya Watanzania ni vijana chini ya miaka 35, lakini kila mwaka *workforce* inayoingia ni kiasi cha Watanzania 800,000 mpaka 1,000,000, inakuwa ni *workforce* ambayo iko tayari kwa ajili ya kuingia kwenye sekta hasa ya kilimo ambayo inaajiri Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake alisema kwamba pamoja na mambo mengine anakusudia kuanzisha kitu kinachoitwa *Youth Investment Window*. Lengo lake kwanza anasema ni kutoa shilingi bilioni 200 ambayo itasaidia katika kuwekeza kwa vijana na wanawake kuingia kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona fedha nyingi zimewahi kuja wakati wa kilimo kwanza na maeneo mengine tukazipeleka kwenye mabenki. Hata hivyo, ninaishauri Serikali kwamba ije na *model* ambayo kweli itasaidia vijana wetu waweze kujiajiri kwenye kilimo. Jambo lingine ambalo Mheshimiwa Rais alisema ni kukuza kilimo kutoka asilimia nne mpaka 10%, ambao ni mkakati wa *ten – thirty*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumebakiwa na miaka mitano tu kufikia 2030. Ninaiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Kilimo wafanye mapinduzi makubwa, na watambue kwamba 85% ya Watanzania bado wanatumia jembe la mkono. Kwa hiyo, ipo haja ya makusudi kabisa kwamba tutoke katika mkwamo ule

ambao mimi ninasema bado upo, sasa tufanye mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kununua matrekta kwa pamoja lakini yapo majembe yanayokokotwa na ng'ombe, hapa tunaweza tukafanya. Tuna viwanda vyetu hapa nchini vinavyozalisha na bei yake ni kuanzia shilingi 160,000 mpaka shilingi 200,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoa kodi zote tukaweka na ruzuku, wananchi wetu wanaweza kununua majembe haya kwa shilingi 80,000 mpaka shilingi 60,000. Lengo lake ni nini? Unaongeza *workforce* ambapo utakuwa umerahisisha wananchi waweze kuzalisha zaidi kupitia majembe yanayokokotwa na ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo ambalo Mheshimiwa Rais amelionesha kwenye hotuba yake ni kufanya kilimo kivutie kwa kuajiri vijana wengi, lakini hawawezi kuwaajiri vijana hawa kwa kupitia jembe la mkono. Huwezi ukawaajiri vijana hawa kwenye kilimo kwa kutegemea mvua na amesema kabisa ni lazima tujikite katika kilimo chaa umwagiliaji pamoja na kilimo cha mbogamboga *(horticulture)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba sana Wizara ya Kilimo kupitia bajeti inayokuja ya Mwaka wa Fedha wa 2026/2027 tuone mapinduzi makubwa sana, hasa ni namna gani fedha zimetengwa kwa ajili ya kwenda kuwaingiza vijana katika sekta nzima ya uzalishaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina fursa kubwa. Sisi tunategemewa na nchi za *SADC* katika kuwalisha chakula, hususan mahindi na mchele. Ipo haja kubwa ya nchi yetu kuweka kipaumbele kikubwa katika kuzalisha. Jambo hili linaenda na Dira ya Taifa ambayo na yenyewe inaongelea habari ya uzalishaji mkubwa wa kilimo. Kwa hiyo, kwenye suala zima la kilimo na nchi yetu tukitaka iajiri watu wengi ni lazima tuweke utaratibu wa makusudi tuweze kupeleka fedha nyingi kwa ajili ya kuajiri vijana kwenye kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Rais anaongea habari ya kukuza viwanda, nami ninataka niseme kwa mkoa huu wa Dodoma, Serikali iangalie Dodoma iwe ni *logistic hub*. Kwanza, tuna miundombinu ya reli ya kisasa *(SGR)* ambapo tutaweza kusafirisha mizigo yetu kwa urahisi hapa, lakini Serikali inajenga kiwanja kikubwa cha Kimataifa hapa Msalato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha kiwanda cha mbolea ambacho kina wafanyakazi kama 2,000 lakini viwanda vikubwa Dodoma bado hatuna. Mji huu ni mji mkubwa, lakini ni mji wa kutegemea mshahara mwisho wa mwezi. Hatuna mzunguko mkubwa wa fedha za viwanda. Ni bora Serikali iweke *scheme* makusudi ya kuweza kuongeza viwanda katika mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja 100%, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa asilimia nyingi za uchaguzi wa Oktoba, 2025. Tunampongeza sana kwa kuaminiwa na wananchi kwa kura nyingi na sisi tunamtakia heri sana katika majukumu yake, na bahati nzuri, leo ninachangia ikiwa siku pekee ya kuzaliwa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia. Nami ninamtakia heri katika siku yake hii muhimu ya kuzaliwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru kipekee sana wananchi wa Jimbo la Busega kwa kuniamini tena kwa mara ya pili kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Nitawatumikia kadiri Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nichangie kidogo maeneo machache juu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwetu iliyokuwa na dira na mpango wa kufika 2030 kama alivyohutubia mahali hapa na tunaamini kabisa Mheshimiwa Rais ataenda kufanya kazi kubwa kwa sababu tumeona mfano katika miaka hii yake mitano iliyopita. Tumeona maendeleo makubwa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Busega tumeona maendeleo makubwa, (vituo vya afya vinne, hospitali ya wilaya imekamilika, mradi wa maji mkubwa, barabara zimetengenezwa, bajeti ya barabara imeongezeka kutoka shilingi milioni 714 mpaka shilingi 2,447,000,000. Hizi ni juhudi kubwa za Dkt. Samia kwa wananchi hususan wananchi wa Busega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Busega wamenituma nimshukuru kwa niaba yao kwa miradi mikubwa kwa hii miaka mitano ambayo alikuwepo. Tuna imani kubwa yale aliyoyaahidi katika hotuba yake yanaenda kufanyika kwa sababu ya namna aliyofanya kwa miaka ile mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niseme kidogo eneo la nishati. Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 29 utaona namna gani amejipanga katika eneo la nishati hasa katika suala zima la umeme. Sasa tuna vitongoji ambavyo vina umeme 39,003 kati ya vitongoji 64,359 vya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ukiangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais amesema ifikapo 2030 vitongoji vyote vitakuwa na umeme na haya yanajionesha sasa hivi. Kwa nini, ninasema yanajionesha sasa hivi? Miradi inayoendelea katika vitongoji vyetu ni vitongoji 2,562 ambavyo miradi yake inaendelea itakayoenda kupatiwa umeme na itakapokamilika, tutakuwa tumebaki na vitongoji takribani 22,000 *plus* ambavyo vitakuwa havina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuona kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia yuko *serious* na kazi, ukitaka kuona Mheshimiwa Dkt. Samia amedhamiria kazi katika eneo la nishati,

kama alivyosema ifikapo 2030 vitongoji vyote vitakuwa na umeme. Sasa tarehe 17 Januari, 2026 tumesaini vitongoji 9,009 kupelekewa umeme katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ongezeko la vitongoji 9,009 ni kubwa sana na vitongoji sasa baada ya mradi huu wa vitongoji 9,009 kukamilika tutakuwa tumebaki na vitongoji 13,785 ambavyo vitakuwa havina umeme. Kwa kasi ya Mheshimiwa Dkt. Samia kama tumeanza mwezi wa 11, ameapa, na leo ni mwezi wa kwanza, ni miezi miwili *plus.* Siku zake 100 tumesaini mkataba wa vitongoji 9,009, maana yake vitongoji 13,785 vilivyobaki sidhani hata kama 2030 itafika ukiangalia katika hotuba yake alivyosema 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kwa kasi hii aliyonayo Mheshimiwa Dkt. Samia inawezekana isifike 2030, vitongoji vyote vitakuwa na umeme kama ambavyo tumeona kasi yake kubwa katika maeneo yetu. Hii inadhihirisha kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia amedhamiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inadhihirisha kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia amedhamiria. Ukisoma dira yetu ya 2050 ambayo imetolewa hivi karibuni, imeonesha ifikapo 2050 mwananchi mmoja atakuwa anatumia *kilowatts* 3,000 kwa mwaka ikilinganishwa na sasa hivi mwananchi moja anatumia *kilowatts 170* kwa mwaka. Ongezeko hili ni kubwa na ukiona hivyo maana yake Mheshimiwa Dkt. Samia amedhamiria kwa wananchi wake katika eneo la nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Dkt. Samia anaingia, eneo la nishati uzalishaji wa umeme katika nchi yetu ulikuwa *megawatts* 1,685. Tunavyozungumza, leo uzalishaji wa umeme sasa umefikia *megawatts* 4,100. Haya ni mapinduzi makubwa na dhamira kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanabusega tunampongeza na tunamtakia heri katika utekelezaji wa haya ambayo tunayapanga kwa miaka ile mitano kufikia 2030. Tunaye Waziri

Mkuu mchapakazi, na tunao Mawaziri, tumeona namna ambavyo wamepokea kazi kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia. Ninaamini watafanya vizuri na kuyafikia yale malengo makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ninataka kusema, ukisoma ukurasa wa 25 mpaka 26 amezungumzia eneo la madini. Tumeona wazi eneo hili pia tumelitengeneza vizuri na tumekua na uzalishaji mkubwa wa madini katika nchi yetu. Katika maeneo ya madini tunaona pato la Taifa limeongezeka kutoka 6.8%, mwaka 2012/2013 mpaka kufikia 10.1% mwaka 2024/2025. Haya ni mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukusanyaji wa maduhuli umetoka shilingi bilioni 173.7 mwaka 2012/2013 mpaka kufikia shilngi trilioni 1.057 mwaka 2024/2025. Haya ni mapinduzi makubwa katika nchi yetu ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia amedhamiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa huko nyuma tulikuwa hatuna mfumo wa kununua dhahabu kupitia *BOT*. Sasa tunavyozungumza leo Mheshimiwa Dkt. Samia ameanzisha mfumo wa kununua dhahabu kupitia Benki yetu ya Tanzania *(BOT)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyozungumza, miezi kama miwili iliyopita, taarifa zilivyotoka tayari tumekusanya tani 16 kwa miezi 14 na hizi ni taarifa za miezi miwili iliyopita. Leo tumefika tani 17 na kufanya nchi yetu sasa itapanda kutoka aliposema *Comrade* Festo pale asubuhi, nchi ya sita. Nchi ya sita ni pale tulipokuwa na tani 16. Ninaamini watakapotengeneza taarifa za sasa, kwa sababu tumeshafika tani 17 tutapanda zaidi hata kuwa wa nne Barani Afrika. Haya yote ni mapinduzi makubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 26 wa hotuba yake, tunaenda kununua mashine ya kuchenjua madini *(multipurpose refinery)* na hii tunaenda sasa kuwasaidia vijana

katika suala zima la kupata ajira. Watapata ajira vijana, lakini uzalishaji wa dhahabu pia utaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie nini faida ya ununuzi wa dhahabu kupitia *BOT?* Bei imepanda na sasa wananchi wanaona ni bora kuuza dhahabu kwa kupitia mfumo wa *BOT* kuliko kuuza dhahabu zao kwa wafanyabiashara wengine kwa sababu bei imeongezeka. Wananchi wetu sasa kama *BOT* siku hiyo hainunui dhahabu, wanaacha kuuza wanasubiri mpaka siku ambapo *BOT* itatangaza mnada wa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maono mazuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia kwa ajili ya wananchi wetu hasa wachimbaji wadogo wadogo wanaonufaika na bei ya dhahabu ambayo inanunuliwa kupitia mfumo wetu wa *BOT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa nje ningepiga makofi kwa ajili ya Mheshimiwa Dkt. Samia ili aone namna gani dhamira aliyonayo na sisi kama Wabunge tunamuunga mkono. Kazi yetu kubwa tumuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Samia, Waziri Mkuu na Mawaziri ili kuyafikia malengo ya Mheshimiwa Dkt. Samia kwenye eneo la nishati na eneo la madini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Simon. Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga ajiandae.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa nafasi na afya njema kuweza kuwepo leo na kuweza kupata nafasi ya

kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu. Pia, ninapenda kutoa shukrani kwa wanananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini ambao wamenipa kura za ndiyo, na kumpa Mheshimiwa Rais Samia kura za kutosha asilimia kubwa sana. Ninapenda kuwapa shukrani za dhati na kwamba nipo hapa tayari kwa ajili ya kuwawakilisha katika miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge letu tarehe 14 Novemba, 2025, ambayo tunaendelea kuichangia au kuitolea maoni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajua kwamba Mheshimiwa Rais wetu, kipenzi chetu na mama yetu ambaye ni hodari sana amesherehekea siku ya kuzaliwa kwake na amesema leo ni 27 ya kijani. Ninaomba tuendelee kumuunga mkono kuhakikisha kwamba tunashiriki zoezi la upandaji miti ambalo linakwenda kuboresha mazingira katika maeneo yetu tunayoishi na tuwape hamasa wananchi wetu ambao tunawawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa ustahimilivu wake, ujasiri wake na ushupavu wake kuipitisha nchi yetu katika kipindi kigumu cha misukosuko na leo ikiwa tulivu hasa kwa kadhia iliyotokea tarehe 29 na tarehe zilizofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tumeona katika hotuba yake upendo wa kweli na ujasiri wa kweli na ustahimilivu wa kweli hasa kwa kuhakikisha kwamba anaendelea kutambua walioathirika kwa kuwapa pole, na vilevile kuwaalika katika azma nzima ya kuja pamoja kama Watanzania kwa njia ya maridhianno na kuendelea kuongea kwa pamoja na kutatua changamoto zetu kwa njia ya majadiliano. Hii ni tunu muhimu sana kulindwa hasa kama jamii moja ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya Uchunguzi, na pengine tuendelee kusubiri majibu yake ili tuweze kuyapokea yale yatokanayo na kuendelea kujenga nchi yetu kwa mustakabali wa kizazi chetu cha sasa na kinachofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa ahadi zake alizozitoa na ambazo ameshaanza kuzitekeleza. Tunaona leo Bima ya Afya kwa Wote inaanza na hasa tunaona upendo wa Rais kwa kuyazingatia makundi ambayo yako kwenye hatari ya kukosa matibabu wakati wanapougua kutokana na changamoto ya kiuchumi hasa wazee wetu wa miaka 60 kwenda juu, watoto wadogo na wakinamama wajawazito ambao tumeona wanaathirika kwa vifo vingi pamoja na wale watoto wachanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo bado nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo ameifanya na uwekezaji mkubwa ambao ameweka kwenye sekta ya afya kwa kuhakikisha kwamba vifo vya wakinamama wajawazito vimepungua zaidi kwa asilimia kubwa sana na vifo vya watoto wachanga na bima ya afya inaendelea kupunguza tatizo hili katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi mikopo kwa wajasiriamali na hii tayari ameshaanza kuitekeleza kwa kutoa zaidi ya shilingi bilioni 10.5. Hii imeendelea kuwa ni hatua kubwa na muhimu ya Mheshimiwa Rais kutekeleza ahadi zake alizoahidi kwa Watanzania wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mikopo ya wajasiriamali ambayo ameitoa kupitia benki mbalimbali imekwenda kuwazingatia wazee/wakinababa wengi ambao wamekuwa wakilalamika katika mikutano yetu mbalimbali kwamba mbona vijana na wakinamama wamepewa kipaumbele? Je, wazee wanazingatiwa wapi? Ninaona hii mikopo imewakumbuka. Kwa hiyo, tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameleta hoja hii na amewazingatia wazee wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia kwa ajira ambazo amezitoa kwa walimu na watumishi wa sekta ya afya. Tunaamini elimu yetu itaimarika. Pia, huduma za afya zitakwenda kuimarika katika maeneo ya vituo vyetu vya afya, zahanati, hospitali zetu za wilaya, hospitali za mikoa na za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niweze kuchangia kwenye sekta ya kilimo kwa uchache. Sekta yetu ya kilimo ni sekta muhimu sana na ni sekta ambayo inatulisha Watanzania wengi lakini pia imeajiri Watanzania wengi. Tunashukuru Mheshimiwa Rais amesema kilimo ni uwekezaji na ni biashara kama biashara nyingine. Maana yake ipate msukumo wa pekee hasa katika kuitengea bajeti na vilevile katika kuiwekea utaalamu wa kutosha ili wananchi waweze kufaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji Mheshimiwa Rais amekizungumzia kwamba ataenda kuongeza ekari za kilimo cha umwagiliaji kutoka 3.46 milioni hadi milioni sita. Hii ni hatua kubwa sana na itakwenda kuajiri vijana wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninapenda kushukuru kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini. Tumepata visima sita ambavyo vimechimbwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ambacho kitakwenda kuajiri wakulima katika zaidi ya ekari 300, lakini vilevile tumepata bwawa kubwa ambalo litakwenda kuwasaidia wakulima wa kilimo cha umwagiliaji kwa vitunguu maji, vitunguu saumu, mahindi na mazao mengine na itakwenda kuongeza uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda pamoja na kuajiri vijana walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la kilimo tunaona Rais amesisitiza umuhimu wa uwepo wa mikopo kwa ajili ya wakulima. Tuna Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo na pia tuna Benki ya Ushirika. Kwa hili kwa kweli tunaipongeza Serikali, lakini tuna maombi hapa kwamba benki hizi zishuke kwa wakulima ambao wengi wako vijijini na ziweze kuwafikia. Hizi benki bado ziko mijini hazijawafikia wakulima walio wengi na hasa wale walio katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia, tumepata ruzuku kwenye maeneo ya mbolea, lakini pia na mbegu. Bado maeneo mengi yamepata kwa bei nzuri sana hasa ile elekezi ya Serikali, lakini tunajua bado tunao wauzaji wa mbegu hizi na wauzaji wa mbolea ambao bado wanaihujumu Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba usimamizi uendelee kuimarishwa ili kuhakikisha kwamba ruzuku ambayo Serikali imeweka kwenye mbolea na mbegu inaweza kuwafikia wakulima bila kuibiwa hasa na matajiri ambao wana tamaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba katika eneo hili la kilimo Serikali hasa Wizara yetu ya Kilimo iendelee kuboresha uwekezaji katika eneo la kuongeza thamani katika mazao ambayo wakulima wetu wanazalisha ili tuzalishe ajira na bidhaa ambazo zinaweza kwenda kuuzwa na zikaweza kuongeza ajira, kutengeneza malighafi kwa ajili ya viwanda, vilevile kuongeza kipato kwa wakulima wetu, lakini pia kuongeza kodi kwa ajili ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachangia eneo la mifugo kwa ufupi sana. Tunajua kwamba nayo ni sekta muhimu sana na wananchi wangu wa Jimbo la Mbulu Vijijini ni wakulima na wafugaji. Mwaka jana, 2025 mwishoni tulipata adha kubwa sana kwa wafugaji wengi sana kupoteza mifugo hasa kutokana na ukame, vilevile magonjwa yatokanayo na kupe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema kwamba Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ameelekeza kwamba tuendelee kujenga kuelekea katika ufugaji wa kisasa ambao unakwenda kusaidia katika uongezaji wa eneo la ufugaji na vilevile kuhakikisha maji yanapatikana kwa ajili ya mifugo. Pia, kuhakikisha kuna majosho ya kutosha katika maeneo ya ufugaji na chanjo kupatikana. Vilevile, kuhakikisha tunakuwa na mifugo iliyo bora ambayo inafugwa na wafugaji wetu ili iwe na tija hasa kwa ajili ya soko la ndani na soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua yako maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wafugaji, lakini yapo maeneo ambayo hayatajatengwa. Yale maeneo ambayo yametengwa, tunaomba Serikali iweze kusaidia sasa kuweka miundombinu muhimu hasa majosho, pia, kuhakikisha *supplies* mbalimbali kwa ajili ya kusafisha ng'ombe, kuchanja ng'ombe na kuwapa utaalam unaofaa ili tuweze kupata mazao yaliyo bora hasa katika eneo hili la mifugo. Vilevile, wafugaji wakumbukwe katika eneo la mikopo kwa sababu ni wazalishaji muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende kwenye eneo la barabara. Ninashukuru sana kwamba Mheshimiwa Rais amezungumza katika hotuba yake na ametoa dhamira ya kweli na hakika kwamba kuna haja ya kuongeza bajeti katika eneo la barabara hasa kwenye *TARURA*. Vilevile, ninaomba na *TANROADS* nayo ikumbukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ni miundombinu muhimu sana hasa katika maendeleo kwa sekta zote na kwa maeneo ya vijijini, wakulima, wafugaji na wajasiriamali hawawezi kuzalisha na kufikisha mazao yao katika masoko bila kuwa na barabara iliyo imara, nzuri na inayopitika majira yote ya mvua na masika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba bajeti ya eneo hili iongezwe na hasa katika jimbo langu. Ninaomba sana ile barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami kutoka Mbulu – Garbabi (kilometa 25), Labay – Haydom (kilometa 25), lakini vilevile kutoka Dareda – Dongobesh, Haydom – Mogitu na Haydom – Singida. Hii ni miundombinu muhimu sana kuunganisha mikoa na wilaya na wananchi wetu watakwenda kufaidi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa upande wa umeme tumepata vitongoji 9,000 na jimbo langu limepata vitongoji 59 na vingine vinaendelea kupata kwa kuwa uhitaji ni mkubwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, malizia.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. Ninapenda kukushukuru wewe na ninashukuru kwa hotuba nzuri ya Mheshimiwa Rais, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel. Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Amos William Maganga. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani ajiandae.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuongea tena mara ya pili katika siku ya leo. Nimefurahi sana kuongea leo ili nami pia niweze kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Siyo hivyo tu, kumpongeza kwa *birthday* yake leo na kweli hata kama hatupo huko, lakini tumemtakia *birthday* njema siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninampongeza sana Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitoe shukrani nyingi kwa Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuingia Bungeni, nafasi ambayo niliipambania kwa miaka 10 bila kupata, lakini sasa nimefanikiwa kuingia Bungeni. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru wanawake wa Dodoma kwa kuweza kuniamini na kunipa kura nyingi sana. Kati ya kura 1,581 niliweza kupata kura 1,524. Kwa hiyo, ninawashukuru sana wanawake wa Dodoma, wameniamini sana na mimi nitawawakilisha vyema Bungeni. Siyo hivyo tu, nitafanya utumishi uliotukuka kuweza kuwatumikia wanawake wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani sana kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais, niliiona ni hotuba ya kiongozi tena iliyo thabiti kabisa, kiongozi mwenye madaraka, lakini upande wa pili ili-*sound* kama hotuba ya mama tena mama mlezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongee maeneo machache ambayo ninamsikia Rais wangu akiongea kama mama. Pale alipoingia tu na kuanza hotuba yake kwa kuonyesha masikitiko yake kwa matukio yaliyotokea Oktoba 29, hiyo ilikuwa ni sauti ya mama. Pia, alipoendelea kuwasamehe wale vijana ambao waliingia kwenye mkumbo hiyo pia ilikuwa ni sauti ya mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, aliongea sasa kama mama, akasema, nikimaliza nafasi yangu sipendi kusemwa kwa majengo, miundombinu, barabara, maghorofa, lakini niache tabasamu kwa Watanzania. Hiyo niliona ni sauti ya mama ndani ya hotuba ya Rais wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilikuwa ni dira yetu ya miaka mitano ambayo tutaifuata na inaenda sambamba kabisa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Niliona Rais ame-*summarize* Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye hotuba fupi aliyoitoa kwenye Bunge lako Tukufu hiyo tarehe 14, Novemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijikite kwenye hotuba hiyo na mawazo yangu niyatoe kwenye uchumi na uwekezaji wa wananchi. Amesema: "malengo yetu ya kiuchumi ni kupandisha kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka 5.6% hadi zaidi ya 7%." Kwa hiyo, alikuwa na maana kwamba *economic growth* yetu itaenda zaidi ya 7%. Pia, akasema kwamba itaongeza ukuaji wa huduma za kijamii ambazo ni muhimu sana, hata tuzo nyingi amepata kwa ajili ya huduma za kijamii, kujenga hospitali, kujenga zahanati mpaka vijijini, kujenga vituo vya afya na kujenga hospitali za rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu hahitaji kutoka mkoa kwenda mkoa mwingine tayari hospitali za rufaa zimejengwa kwenye kila mkoa na hapo moja kwa moja ameokoa maisha ya mwanamke

na mtoto. Hivyo, wanawake tumerefushiwa maisha yetu, hatufi mara nyingi kwa kujifungua au kwa njia ya uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais huyu mwanamke amejipambanua kwa kutujengea vituo vya afya na zahanati kuanzia chini vijijini, kwenye tarafa zetu, kwenye wilaya zetu na hospitali za rufaa zipo kwenye kila mikoa yetu. Hivyo, kongole nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, amejikita katika kujenga miundombinu wezeshi ya kiuchumi. Hapo ndiyo tunaona barabara, madaraja yanajengwa, anafanya uwekezaji rafiki ili tuweze kufanya maendeleo ya kiuchumi. Nami ninampongeza tena Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano. Pia, anasema ataimarisha masoko na mitaji na kuhamasisha uwekezaji wa ndani, anatia moyo Watanzania kuwa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa tunafikiri wawekezaji ni wazungu. Mzungu akija ndio anatetemekewa kuwekeza, lakini sasa hivi tunatiwa moyo wawekezaji wa ndani kuwekeza kwenye viwanda na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Ana kitengo maalumu cha kuwatia moyo wawekezaji wa ndani, lakini akigusa moja kwa moja, ni kutia moyo shughuli zetu za madini, na pia kuwawezesha au kuwadhamini mikopo hao wawekezaji wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme tu ukweli tumaini hili ni kubwa sana kwa wanawake na vijana pamoja na watu wa makundi maalum kwa sababu zile 10% za kila halmashauri bado zinaendelea. Alipotamka hivi tu, nafikiri wanawake na vijana wote tulifurahi. Hilo ni tumaini kubwa sana kwa wanawake wa Kitanzania kwamba tutaendelea kupata hizo 10% za mikopo, na bado ataendelea pia kufanya mifuko yote ya uwekezaji iliyo chini ya ofisi yake ya kiuchumi, yapata mifuko 74, nayo pia itaendelea kuwasaidia wanawake, vijana na makundi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Dodoma sisi tumenufaika sana na hizi 10%. Kwa miaka minne tu wanawake wamepokea

shilingi bilioni 1.6, kwa Dodoma Mjini peke yake. Siyo hivyo tu, tumeendelea kunufaika na mifuko kama *TASAF* na tumeenda kunufaika na mifumo mingine kama *Women Development Funds*. Kwa hiyo, sisi tunaendelea kunufaika na mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutuwazia vizuri wanawake, vijana pamoja na makundi maalum kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ni hilo tumaini sasa la shilingi bilioni 200 ambazo nazo pia zinaenda kwa wajasiriamali wote, lakini wanufaika wakubwa watakuwa ni hao hao wanawake, vijana na makundi maalum pamoja na wazee wameongezwa hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza sana hotuba hii, ina mashiko. Tunawaomba tu watendaji kwenye Wizara mbalimbali na sekta mbalimbali watumie vizuri maneno haya yaliyowekwa kwenye hii hotuba ili wanufaika wawe watu wote ikiwepo wanawake wote hasa wa vijijini. Tukiwa kwenye kampeni, tulipokwenda vijijini, wanawake wengine hawajawahi kusikia na kupata hii mikopo. Hivyo basi, yatengenezwe mazingira rafiki ambayo mikopo hii itaweza kuwafikia wanawake waliopo vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, elimu hiyo ya fedha ambayo tuliongea hata asubuhi iendelee kutolewa mpaka kule vijijini ili wanawake, vijana na makundi haya maalum yaweze kupata elimu ya fedha ili sasa waweze kurasimiwa biashara zao na waweze kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono sana hotuba ya Rais wangu mpendwa kabisa. Mungu ambariki, ampe maisha mema na leo ni *birthday* yake, tunamhitaji akiwa na afya njema aendelee kufanya majukumu yake, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Neema. Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga atafuatiwa na Mheshimwia Emmanuel Peter Cherehani.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nami ninaanza kwa kushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wa Wanasikonge, kwenye hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningeomba kabla sijaendelea, uniruhusu niweze kutoa tathmin ndogo sana ambayo niliiona kwenye jimbo langu nilipotembelea wakati ninawashukuru wananchi kwa kazi kubwa waliyoifanya tarehe 29 Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Sikonge lina jumla ya kata 20, vijiji 71, vitongoji 287 na kwa sasa lina wakazi 372,800 na hii ni kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 pamoja na *projection rate* ya asilimia 3.1 Kwa hiyo, kwa hivi sasa tuko 372,800. Katika jimbo langu hilo niliweza kutembelea kata zote na nilibahatika kufanya mikutano zaidi ya 46. Ninafurahi kusema kwamba idadi ya watu walioongea wao wenyewe kwenye mikutano hiyo walifika 678. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema kwamba kati ya hao watu 678 watu 230, sawa na 34%, waliongelea changamoto ya barabara katika maeneo yao. Vilevile, watu 142 sawa na 21%, waliongelea ufinyu au upatikanaji wa maeneo ya shughuli za kiuchumi katika wilaya yetu ya Sikonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, watu 88 waliongelea changamoto ya maji ambao ni sawa na 13%. Pia 12% sawa na watu 81, waliongelea changamoto ya ujenzi wa zahanati, vituo vya afya pamoja na upatikanaji wa madawa. Hali kadhalika, watu 54 sawa na asilimia nane, waliongelea sekta ya elimu na hasa waliongelea juu ya umaliziaji wa majengo ya shule, uchakavu wa madarasa pamoja na upungufu wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine watu 34 waliongelea mambo mengine ikiwemo utawala bora, athari za wanyamapori, upatikanaji wa mbolea na hususan ya ruzuku, vilevile mawasiliano

na hasa ujenzi wa minara ya simu, hicho ndicho nilichokiona huko jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija sasa kuchangia hoja. Kwanza kabisa, wananchi wa Jimbo la Sikonge wanampongeza sana na wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mambo makubwa aliyowafanyia Wanasikonge. Sisi Wanasikonge ni wakulima, Mheshimiwa Rais amefanya jambo kubwa ambalo hatukulitarajia wala halikuwa katika ndoto zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na shida ya mbolea, lakini Mheshimiwa Rais ametumwagia mbolea ya kutosha na isitoshe mbolea yenyewe kwa bei ya ruzuku, tunamshukuru sana. Kama haitoshi, sisi ni wakulima wa zao la tumbaku, kuna kipindi tumbaku iliyumba kwa sababu tulikosa masoko, lakini Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa. Ametutafutia masoko na sasa hivi tunauza tumbaku yetu kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, mliopo niwaambie tu msimu uliopita, zaidi ya shilingi bilioni 110 zimeweza kuingia pale Sikonge, tufanye nini sasa Wanasikonge? Kweli tarehe 29 Wanasikonge walijitoa kwa wingi na Mheshimiwa Rais amepata zaidi ya 98% kwenye Jimbo la Sikonge. Hizi 98% hazijaja kwa bahati nzuri, wala bahati mbaya, hapana. Ni kwamba yeye mwenyewe alizitafuta kwa sababu alifanya makubwa ndani ya Jimbo la Sikonge. Tunamshukuru sana na Wanasikonge wanampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija katika suala la maji, leo hii sisi kule Sikonge maji ya kutoka Ziwa Victoria yameingia. Bado kuna changamoto ndogo ndogo, lakini wataalam wanasema kwamba ifikapo Februari Wana-Sikonge wanapata maji ya uhakika kutoka Ziwa Victoria. Sasa Wanasikonge tuseme nini? Hivi tungeenda tukampe nani hizo kura kwa mambo haya mazuri aliyotufanyia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la umeme ndiyo usiseme, wachangiaji wamesema. Leo hii Mheshimiwa Rais

anamalizia vitongoji vilivyobaki. Leo katika Jimbo langu la Sikonge nikichukua na hivi ambavyo ametupa sasa hivi siyo zaidi ya vitongoji 50, ndiyo vimebaki ambavyo havina umeme, na ninaamini hata kabla ya 2030 tayari vitongoji vyote vitakuwa vimepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia kusema tena, 98% aliyoipata haikuwa kwa bahati mbaya wala bahati nzuri isipokuwa alizitafuta yeye mwenyewe kwa kazi kubwa aliyoifanya. Tunamshukuru na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija sasa kwenye tathmini hii. Kimsingi kinachoonekana hapa kwa wananchi wa Sikonge, changamoto kubwa namba moja waliyonayo ni barabara katika maeneo yao. Hata hivyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake ukurasa wa 28 amesema waziwazi kabisa kwamba anaenda kuongeza bajeti na uwezo wa *TARURA*. Kwa hali hiyo, sisi Wanasikonge imetupa faraja kubwa sana kwa sababu hii ni changamoto kubwa sana katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Jimbo la Sikonge ni kubwa, ni kubwa sana. Kuna kutoka Makao Makuu ya kata kwenda vijijini, kwa mfano, kutoka pale Sikonge uende Kijiji cha Igalula, ni zaidi ya kilometa 26 kwenda kwenye kijiji. Ni kubwa mno. Kimsingi ni kwamba Jimbo la Sikonge linalingana na baadhi ya nchi jirani. Hivyo tunaomba sasa, *TARURA* watakapokuja na Wizara, waje na *formula*, kanuni nzuri ambayo kwa kweli ile bajeti ita-*reflect* ule ukubwa wa jimbo na mtandao wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana, ninawaomba sana ndugu zangu wa *TARURA*, ndugu zangu wa Wizara, hebu mjaribu kuliangalia hilo, mje na *formula* nzuri ili kusudi tuweze kupata ile bajeti kulingana na mtandao wa barabara jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo vilevile limewagusa sana Wana-Sikonge ni ufinyu wa maeneo ya shughuli za kiuchumi ikiwemo kilimo, ufugaji pamoja na urinaji wa asali.

Ninamshukuru sana leo hii Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na wizara kwa jibu lake zuri la Serikali kwamba Kamati ya Mawaziri imeshapewa hiyo kazi na imeshaifanya hiyo kazi, kinachosubiriwa sasa ni taarifa ili kusudi hawa wananchi waweze kuongezewa maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa, ninaomba sana ile kamati sasa itoe hiyo taarifa ili kusudi hawa wananchi waweze kupata hayo maeneo na hii migogoro midogo midogo ambayo inajitokeza iweze kwisha na watu waendelee na shughuli zao za kiuchumi. Tunaomba sana hilo kwa kweli, wafanye namna hiyo. Wakifanya namna hiyo, kwa kweli sisi hizi changamoto ndogo ndogo watakuwa wametuondolea kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni jambo la maji. Kama nilivyosema hapo awali, tayari hivi sasa tunayo maji ya Ziwa Victoria. Ninawaomba tu ndugu zangu wataalamu na Serikali kwamba ijaribu sasa kuangalia kwa sababu tunaenda kwenye gridi ya Taifa ya Maji na kwa hivi sasa kuna kata tisa za awali katika Jimbo la Sikonge ambazo ndizo zitafaidika na huo mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba, kwa vile sasa zinakuja kuingia kwenye mfumo uliopo, kwenye mtandao wa maji uliopo, kwa kweli tunaamini kuna kata tatu zinaenda kufaidika, na yale maji ni mengi na yana *pressure* ya kutosha na miundombinu ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini kwamba Kata ya Usunga na yenyewe itafaidika, Kata ya Kiloleli na yenyewe itafaidika lakini vilevile na Kata ya Kipanga nayo itafaidika kutokana na huo mradi kwa sababu miundombinu ipo tayari. Maji yakishafika pale ni kuingia tu kwenye ile miundombinu, yanafika na kwenye hizo kata. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba badala ya kuwa na kata zile tisa, sasa tutakuwa na kata 12 na katika zile kata 20, tutabakiwa na kata nane ambazo sasa kwa bajeti ya kuchimba visima, ninaamini wananchi wa Sikonge tutawafikia kwa 100% hata kabla ya 2030.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote ninaendelea kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kibali na baraka zake tele kwa kunirudisha tena Bungeni. Pia, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa ushindi mkubwa alioupata kwa Watanzania, na leo kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni siku yake ya kuzaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Ushetu kwa kuniamini, kwa kunirudisha tena mara ya pili, nami ninaendelea kuwaahidi wananchi wa Ushetu kwamba tuko pamoja na mimi sitawaangusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Spika, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Mawaziri wote mliopata kibali cha Mheshimiwa Rais. Mimi ninaendelea kuwapongeza sana wote, endeleeni kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kwa siku zake 100 hasa kwenye suala la michezo amefanya kazi kubwa sana. Kwenye ukurasa wake wa 36 alisema kwenye kile kitabu ukurasa wa 36 amesema michezo ni uchumi, hatuwezi kupata matokeo makubwa bila kuwekeza. Mheshimiwa Rais amewekeza sana kwenye michezo na leo tumeshuhudia sisi Watanzania, timu yetu ya Taifa imeingia kwenye 16 bora ya Kombe la *AFCON*, isingelikuwa bahati mbaya inawezekana *Taifa Stars* ingeleta kombe hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana walijipanga vizuri, vijana walipewa motisha vizuri na kupitia goli la mama, timu zetu za Simba, Yanga, Azam pamoja na Singida leo ziko kwenye 16 bora. Mheshimiwa Rais ameandika historia kubwa kwenye michezo hapa nchini. Tuendelee kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, tuendelee sana kumsaidia na kumwombea afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa mikopo ya akina mama kwa upande wa Jimbo la Ushetu, kwa siku 100 za Mheshimiwa Rais wetu, tayari shilingi 1,720,000,000 zimetolewa kwa wananchi wa Ushetu ikiwemo wanawake shilingi 836,000,000, vijana shilingi 835,000,000, na wenye ulemavu shilingi 55,000,000 nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye barabara, tulikuwa na changamoto kubwa ya madaraja, toka uhuru yalikuwa hayapitiki. Mheshimiwa Rais ameletwa shilingi 18,600,000,000 kujenga madaraja ya kisasa. Daraja la Ng'wabomba lilishindikana toka uhuru, shilingi 2,900,000,000 tayari limekamilika, lakini pia Daraja la Ubagwe ambalo wananchi wameteseka kwa muda mrefu, shilingi 4,100,000,000 nalo limeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Kasenga pale Ulowa kwenda kwa jirani yangu pale Tabora, shilingi 5,100,000,000 daraja la urefu wa meta 80, ni karibu uwanja wa mpira, nalo limekamilika. Pia, tuna Daraja la Sunga, ndugu zangu wa Ng'hwande pale ni mashahidi, tayari pale shilingi 4,200,000,000 zimewekwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nalo daraja limekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hospitali Mheshimiwa Rais hajatusahau. Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu, shilingi 3,500,000,000 nayo imekamilika na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais ameniletea watumishi. Juzi kwenye siku 100 tayari ajira 131 zimemwagwa kwa wananchi wa Ushetu wakiwemo watumishi wa afya 64 na elimu sekondari 56, tayari wameripoti kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nidhamu ya watumishi kwa upande wa Ushetu ni kubwa sana, wanahudumia vizuri wananchi wetu. Ni pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais. Leo Mheshimiwa Rais anakuja na Bima ya Afya kwa Wote, ninawaomba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwenye hotuba yake na tunanukuu kwamba anakuja na fyekeo kwa wazembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wasiwepo watu wa kwenda kushindwa kuwahudumia wananchi waliolipa bima yao kwa sababu ya uzembe wao na hulka zao. Ninaomba Mheshimiwa Waziri haya yafanyie kazi kuhakikisha tunamsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye suala la kilimo, mwenzangu hapa wa Sikonge amesema wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani, mbolea ya *CAN* ambayo inatumiwa na wakulima wengi hapa nchini ilikuwa imefika shilingi 120,000, leo wananchi wanachukua kwa shilingi 63,000 kwa bei ya ruzuku. *LPK* ilikuwa imefika shilingi 160,000, leo wananchi kote na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wanachukua kwa shilingi 73,000. Mbolea ya *urea* ambayo pia maeneo mengi tunaitumia ilifika shilingi 160,000, leo wanachukua kwa shilingi 73,000. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? Ni mama amefanya kazi ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye kilimo cha pamba, matrekta zaidi ya 800 yamemwagwa. Wakulima wa pamba walikuwa wanalimiwa kwa shilingi 100,000, au shilingi 60,000 kwa heka moja, leo kote wanalimiwa kwa shilingi 30,000 kwa heka moja. Vijana wa *BBT* wamemwagwa kule kuwafundisha, watoke kwenye uzalishaji wa kilo 300 au 500 kwa heka moja, tunaenda kuzalisha kilo 1,000 kwa heka moja kwenye eneo la pamba. Wanunuzi tayari wameshapeleka wataalamu. Kwa hiyo, ninaendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kwenye upande wa tumbaku kama alivyosema ndugu yangu, hali ya uzalishaji ilishuka. Tulikuwa na kilo 240,000, zikashuka mwaka 2015, 2018-2020 zikabaki kilo 68,000, lakini leo zimepanda mpaka kilo 240,000,000

na bei imetoka wastani wa dola 1.75 na sasa ni dola 2.02 na madaraja yetu ambayo wakulima wengi wanayapata *L10F* ni dola tatu, *L1* ni dola tatu, *L20F* ni dola tatu, *C1O* dola tatu, madaraja ya dola tatutatu yameongezeka, ni wastani wa shilingi 8,000/= kwa kilo. Ni historia kubwa ameiandika Mheshimiwa Rais kwenye nchi yetu, lazima tumwombee Mheshimiwa Rais wetu, amefanya kazi kubwa sana kwenye suala la ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumbaku ilifika mahali wakulima wakapangiwa uzalishaji, mwenye uwezo wa kulima eka tano, anaambiwa alime eka mbili, mwenye uwezo wa kuzalisha kilo 10,000, azalishe kilo 5,000. Mheshimiwa Rais aliikataa na leo wakulima wanalima kulingana na uwezo wao. Mheshimiwa Rais ametende mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vyama va ushirika Mheshimiwa Rais tayari kwenye vyama ameanzisha mfumo wa MUVU ambao unasajili wakulima, unasajili vyama vyote. Leo mpaka Mkulima wa Sikonge, Mkulima wa Kigoma, Mkulima wa Songea kwenye upande wa ushirika utamjua yuko wapi? Ana shamba gani? Yuko maeneo gani? Vifaa vya kupima udongo tayari vimepelekwa. Vyama zaidi ya 6,300 vimesajiliwa, wakulima 3,279,000 wote wamesajiliwa kwenye mfumo, tayari wapo kwenye mfumo wa *MUVU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mizani ya kidigiti ambayo huwezi kumwibia mkulima sasa hivi kwenye maeneo ya ushirika, zaidi ya mizani 4,400 imenunuliwa na vyama vya ushirika. Warajisi wote wa mikoa yote ya Tanzania bara wamepatiwa magari. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wanaushirika, historia ya Mheshimiwa Nyerere aliyoiacha, Mheshimiwa Rais ameimaliza. Benki ya Ushirika imeanzishwa na inamilikiwa na wakulima kwa zaidi ya 51%. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la sekondari, sisi Ushetu tumepewa zaidi ya shilingi 1,700,000,000, leo shule zetu za msingi zimekarabatiwa zote. Leo ninachukua hatua kuipongeza

Shule ya Msingi Nyabusaru iliyoko katika Halmashauri ya Ushetu, ni shule ya kata ambayo imewekewa mazingira mazuri na Mheshimiwa Rais ambapo zamani zilikuwa zinadharaulika sana, imekuwa ya kwanza kwenye mtihani wa Darasa la Nne kitaifa kutoka kwenye shule za kata. Mheshimiwa Rais ameweka mazingira popote, na mimi ninawaalika Waheshimiwa Wabunge, shule ile nafasi zipo, leteni watoto wenu, alama zote 300 zilipigwa pale kwenye shule ya msingi. Kwa hiyo, ni kazi kubwa ya mazingira mazuri aliyoiweka Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa sekondari kwenye Jimbo la Ushetu, ni zaidi ya shilingi 6,300,000,000 zimepelekwa kwa Mheshimiwa Rais, shule mpya sita na shule ya watoto wenye vipaji ya shilingi 1,600,000,000 imejengwa na imeshakamilika, watoto tayari wameanza kusoma. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana, nami ninaendelea kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku 100 za Mheshimiwa Rais, wananchi wanaona, ajira zimeongezeka, na juzi tu amemwaga tena ajira nyingine 5,000. Huyu mama jamani, hebu ninaomba tumpigie makofi ya kutosha. Amefanya kazi kubwa mno. Leo ushindi alioupata zaidi ya 97% ni halali yake mama wa watu. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni kama vile alivyosema Mheshimiwa Mbunge moja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye michezo amefanya, kwenye mambo ya ushirika; kwetu sisi wakulima, amefanya; kwenye elimu amefanya; kwenye afya amefanya; kwenye barabara amefanya; na kwenye umeme amefanya. Sasa Waheshimiwa Wabunge leo kwenye umeme mnaona vitongoji vyenu vyote zaidi, kwenye jimbo langu, vitongoji 134 vilivyokuwa vimebakia, leo tayari wakandarasi wako kazini, tushindwe wenyewe. Maji ya Ziwa Victoria tayari shilingi 44,000,000,000 mkandarasi yuko *site* kazi inafanyika. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kusema ni mengi, lakini kubwa sana twendeni tukamsaidie Mheshimiwa Rais, tukawaambie Watanzania nini kimefanyika katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu kwa mchango mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji kwa siku ya leo imekamilika, ninachukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanyika, lakini pia, yako mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo pia wameyasema, Serikali imeyasikia, wataendelea kuyafanyia kazi. Mjadala utaendelea tena kesho hadi siku ya Ijumaa tarehe 30 ambapo utahitimishwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya machache, basi ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.13 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 28 Januari, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*